# Nipashe

Ijumaa Septemba 27, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580034

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Ahukumiwa kifo kwa mauaji kisa kunyimwa supu ya kuku

UKURASA 10




UKURASA 13

# Amwandikia barua DPP afutiwe kesi uhujumu

UKURASA 2




## YALIYOMO

UKURASA WA 2

**WAZIRI LUGOLA AZIPA ANGALIZO ASASI KOSOAJI**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugol,a amezionya asasi zisizo za kiserikali...

UKURASA WA 4

**AJALI YAUA WANAJESHI 2, YAJERUHI WENGINE 20**

ASKARI wawili wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wa Kikosi cha 24 KJ, wamefariki...

UKURASA WA 7

**NIDA KURAHISISHA UTOAJI KITAMBULISHO CHA TAIFA**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), imesema inakuja na mpango madhubuti wa...




Wafanyabiashara Harbinder Sethi na James Rugemalira wakiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza baada ya kesi inayowakabili ya uhujumu uchumi, kuahirishwa mpaka Oktoba 10, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wanaume waongoza matukio ya kujiua

UKURASA 3

## Mbwa, paka 300 wafugwa kwenye nyumba ya serikali

UKURASA 3


**MICHEZO** YANGA YATAMBA HAINA WASIWASI UK.32

**MAONI, KATUNI** UK.6

# Waziri Lugola azionya NGO

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola, amezionya asasi zisizo za kiserikali ambazo zinatumia mwanya wa kukosoa serikali kwa kuitukana na kupotosha jamii.

Lugola alitoa onyo hilo jana, alipokuwa akizindua Ofisi ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) mkoani Dodoma na kampeni ya miaka 25 ya kituo hicho pamoja na uzinduzi wa tuzo ya Majimaji ambayo hutolewa kwa mtu ambaye ametoa mchango mkubwa wa kisheria katika jamii.

Alisema siku za hivi karibuni serikali imebaini kuwapo kwa asasi zisizo za kiserikali ambazo zinatumia mwanya huo kukosoa serikali, lakini badala ya kukosoa wamekuwa wakiitukana.

"Wanaenda mbali zaidi kwa kuipotosha jamii kwa kusema serikali ya awamu ya tano haijafanya kitu, uanaharakati wa aina hii ndani ya asasi zisizo za kiserikali ni uanaharakati usioitendea haki serikali, kwani wananchi wameshuhudia serikali ikijenga miundombinu mingi ya barabara, madaraja ikisomesha wanafunzi bure," alisema.

Alisema pia serikali inahakikisha misingi ya demokrasia na utawala wa sheria vinazingatiwa, hivyo si vyema kuwapotosha Watanzania.

"Kwa hiyo sio vyema wala busara kuwaambia Watanzania serikali haijafanya kitu ilhali watu wanaona na huu ni upotoshaji," alisema.

INAENDELEA UK.8

# Amwandikia barua DPP asamehewe kesi

**Na Hellen Mwango**

RAIA wa Sri Lanka, Abdulazeez Amaan (26), amemwandikia barua Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kuomba kukiri kosa la kusafirisha madini yenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 36 kinyume cha sheria.

Wakati kijana huyo akiandika barua hiyo, DPP amesema watuhumiwa mbalimbali wanaokabiliwa na kesi za uhujumu uchumi wameendelea kumiminika kuomba msamaha na kukiri kosa kama alivyoagiza Rais John Magufuli.

Amaan ambaye pia ni mwanafunzi, alifikishwa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, akikabiliwa na shtaka la kusafirisha madini hayo bila kuwa na kibali cha Kamishna wa Madini nchini.

Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon, alimsomea mashtaka yake mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba.

Wankyo alidai kuwa Septemba 21, mwaka huu, katika Uwanja wa Ndege wa Mwalimu Julius Nyerere, jijini Dar es Salaam, mshtakiwa alikutwa akisafirisha madini aina ya Scapolite yenye uzito wa gramu 996.50, Sperssartite gramu 487, Tanzanite gramu 44, Quarts gramu 126, Citrine gramu 174, blue agate gramu 101.80, Toumarine gramu 16, Aquamarine gramu 14.30 na Supphire gramu 5.04 yote kwa pamoja yakiwa na thamani ya Sh. milioni 36.5 bila kuwa na kibali.

Baada ya maelezo hayo, Hakimu Simba alimtaka mshtakiwa huyo kutojibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza shauri hilo hadi itakapopata kibali kutoka kwa DPP.

Wakili wa Utetezi, Shabani Mlembe, alidai kuwa tayari mteja wake ameshaandika barua kwa DPP ya kukiri kosa hilo, hivyo

INAENDELEA UK.8



Kamishna wa Operesheni wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Billy Mwakatage (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kupokea msaada wa boti ya maokozi uliotolewa na Serikali ya Ujerumani kupitia Mji wa Hamburg. **PICHA: ZIMAMOTO**


Nipashe
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

NAFASI ZA KAZI

MWANDISHI WA HABARI WA KUJITEGEMEA

Gazeti la Nipashe linatangaza nafasi kwa Mwandishi wa habari wa kujitegemea kutoka mikoa yote nchini.

Mwombaji awe na sifa zifuatazo:

1. Awe amefanyakazi angalau miaka mitatu (3) kwenye chombo cha habari
2. Ajue misingi, miiko na maadili ya uandishi wa habari
3. Awe mwenye kujituma na mbunifu katika kutafuta habari

Mwombaji awasilishe maombi yake kupitia barua pepe **nipashe.gazeti@nipashe.co.tz**

Mwisho wa kutuma maombi ni Septemba 30

615421902


# Sensa 2022 kufanyika kidijitali

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Taifa ya Takwimu (NBS), inatarajia kutumia teknolojia ya kisasa yenye uwezo wa kuwahesabu Watanzania wote na kurusha takwimu kwenye satelaiti katika Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika mwaka 2022.

Aidha, mfumo huo utapunguza matumizi ya gharama kubwa kwenye sensa na inatarajiwa kutumia nusu ya Sh. bilioni 15 zilizotumika katika sensa ya mwaka 2012.

Teknolojia hiyo ijulikanayo 'Mobile GIS' inatumia GPRS na kila kitu kitaingizwa kwenye setelaiti ambayo mfumo mzima gharama yake ni kati ya Sh. milioni 38 na 40.

Akizungumza katika semina ya wahariri na waandishi wa habari kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Morogoro na Dodoma iliyoandaliwa na NBS, Mtakwimu Benedict Mugambi, alisema kila taarifa itakayokusanywa kwenye sensa hiyo itawekwa kwenye mfumo wa NBS.

Mugambi alisema katika kukusanya takwimu hizo watatumia kishikwambi (tablets) na simu za mikononi zenye mfumo wa 'android' na kuzirusha kwenye satelaiti na kupeleka taarifa moja kwa moja kwenye mfumo.

"Hii mobile GIS ukiwa na simu yako ya kawaida ya android unaweza kufanya kazi na sisi. Au ukiwa na tablet ambayo ni maalum kwa ajili ya hii kazi, bado unaweza kufanya kazi na sisi. Tofauti ni kwamba hii kishikwambi ni maalum kwa kazi hii hakitakuwa na programu yoyote na haitapokea ujumbe wa simu," alisema.

"Hii ni moja ya kazi ambazo tumefanya Chamwino wakati wa majaribio. Mmoja alikuwa anatumia simu ya kawaida mwingine kishkwambi. Kuna mfumo kila kitu kinaingia hapa na kuna 'tool box' ambayo kuna 'applications' mbalimbali. Sisi wenyewe tumefanya kwa asilimia tano tu na hii 'package' nzima ni kama Sh. milioni 38 hadi 40," alisema.

"Ni ghali lakini inafanya kazi kubwa sana. Enzi zile tulikuwa tunaona milioni 38 ni kubwa sana lakini unaweza kutumia hii Sh. milioni 38 ukapunguza matumizi ya mabilioni ya fedha," aliongeza.

Mtakwimu huyo alisema kazi itakayofanywa na teknolojia hiyo itakuwa nzuri na haitakuwa na gharama na kila Mtanzania atahesabiwa.

"Ile kazi tuliyofanya mwaka 2012 mpaka leo bado tunahangaika nayo pale, 'manual' (ya mkono) ina gharama kubwa sana. Hii teknolojia wadadisi wakianza kwenda kuhesabu watu tunawaona. Magari watakayotumia tunayaona kupitia mfumo huu huu. Hakuna mambo sasa hivi ya kusainishana fedha ukabaki ofisini," alisema.

"Hakuna suala la kusaini (kutia saini) fedha uende sijui Dar es Salaam kusalimia familia. Ukiondoka tunajua umeondoka, gari linatembea tunaliona, kijiji unachoenda tunakiona, umekaa ofisi ya mtendaji, unamaliza kazi tunakuona. Ukizima tu tunakuona na tunakuuliza kwa nini umezima, hivyo hakuna udanganyifu."

Alifafanua kuwa mwaka 2012 watu walikuwa wakijaza taarifa za uongo na matokeo yake watu walikuwa wakilalamika kutohesabiwa lakini kwasasa haitatokea hivyo.

"Hii teknolojia ukiingia kwenye nyumba unaonekana yule ameingia kwenye nyumba. Ukitoka unaacha

INAENDELEA UK.8

## HABARI KITAIFA



Mkurugenzi wa Mji wa Mbinga mkoani Ruvuma, Grace Quintine, akipokea Mwenge wa Uhuru kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa, Gipson Mhagama, ambao ulizindua miradi tisa ya mji huo ya thamani ya Sh. milioni 924 jana. **PICHA: GIFT THADEY**

## Mshtakiwa akana kumsaidia Malinzi

**Na Hellen Mwango**

MHASIBU wa zamani wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Nsiande Mwanga (29), amedai mahakamani kuwa hakuwahi kumsaidia aliyekuwa Rais wa shirikisho hilo, Jamal Malinzi, kupata fedha yoyote. Amedai kuwa sababu fedha zilizokuwa zikitolewa ni kwa ajili ya matumizi mbalimbali halali katika shirikisho hilo.

Mwanga alidai hayo jana wakati akijitetea dhidi ya mashtaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa fedha Dola za Kimarekani 173,335. Ushahidi wa utetezi huo unasikilizwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu mbele ya Hakimu Mkazi Maira Kasonde. Akiongozwa na Wakili Utetezi, Richard Rweyongeza, Mwanga alidai alijiunga na TFF Aprili Mosi, 2016 na hakuwa anafahamu kwamba shirikisho hilo walikuwa wanamtafuta mtu anayehusika na kodi.

Alidai kabla ya kujiunga na shirika hilo, alikuwa hawafahamu Malinzi na aliyekuwa Katibu Mkuu wa TFF, Celestine Mwesigwa.

Mwanga alidai alipojiunga na shirikisho hilo alipata barua ya ajira iliyomwelekeza kazi zake ikiwamo kufanya kazi atakazopewa na mwajiri wake.

INAENDELEA UK.26

# Mbwa, paka 300 wafugwa kwenye nyumba ya serikali

**Kelvin Innocent na Dotto Charles**

UONGOZI wa Manispaa ya Temeke, umebaini nyumba yake iliyomilikishwa kinyemela kwa mtu mwingine kutumika kufuga zaidi ya mbwa na paka 300.

Paka na mbwa hao wametengenezewa vyumba maalum vya mbao vya kulala ndani ya nyumba hiyo ya kisasa, huku wakiwa na watu wa kuwahudumia.

Aidha, wanyama hao wana eneo maalum la kucheza lenye matairi yaliyopakwa rangi mbalimbali na bustani nzuri.

Viongozi hao juzi walijikuta katika wakati mgumu kuingia ndani ya nyumba hiyo kwa kuwa walinyimwa ruhusa hadi waombe kibali, jambo ambalo lilizua mabishano baina yao na meneja anayesimamia eneo hilo na kulazimu kuingia kwa nguvu.

Nyumba hiyo mali ya Manispaa ya Temeke, iliyoko Oysterbey mtaa wa Mawenzi Kitalu namba 823, inasadikiwa kuuzwa kinyemela tangu mwaka 2000.

Baada ya Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Lusubilo Mwakabibi, na viongozi wengine wa kamati ya ulinzi na usalama kuingia ndani ya nyumba hiyo, walielezwa kuwa nyumba hiyo inamilikiwa na watu waitwao Ngowi na Miriam.

"Wewe ni Mtanzania?" Aliulizwa dada aliyejitambulisha kama ni msimamizi wa eneo hilo na kujibu: "Ndiyo mimi ni Mtanzania ila ninapaswa kujiridhisha kama

INAENDELEA UK.25

# Wanaume waongoza matukio ya kujiua

**Na Beatrice Shayo**

WATAALAMU wa afya ya akili nchini wamesema wanaume wanaongoza zaidi katika matukio ya kujiua kuliko wanawake kutokana na matatizo yao kuyaficha hali inayosababisha msongo wa mawazo na kuchukua hatua hiyo.

Wameeleza kuwa vitendo vya wanaume kujiua ni mara tatu zaidi ya wanawake.

Wakizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, wataalamu hao akiwamo Daktari Bingwa wa Afya na Magonjwa ya Akili Dk. Praxeda Swai, walisema kuna umuhimu wa kuchukua hatua kunusuru vifo vya watu kujiua.

Kadhalika, wanaume wameshauriwa wanapokuwa katika hali ya msongo wa mawazo ni vizuri wakalia badala ya kukimbilia kujiua.

Dk. Swai alisema kwa mujibu wa takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO), watu 800,000 hujiua kila mwaka duniani huku kila sekunde 40, mtu mmoja hujiua.

"Sio kwamba mtu anajiua kwa bahati mbaya, anakuwa anajua kile anachokifanya kwa sababu kuna mambo yamemfanya afikie uamuzi hao na kuona hawezi kuendelea na maisha," alisema Dk. Swai.

Alisema mtu anayefanyiwa vitendo vya unyanyasaji na anayeugua magonjwa sugu yupo katika hatari ya kujiua kutokana na kuwa kwenye mateso ya muda mrefu.

Dk. Swai alisema dalili za mtu anayetaka kujiua zinaweza kugundulika kwa vitendo vyake, vikiwamo vya kuonyesha kuchoka na maisha na matamko yake.

"Utamuona anaaga watu, kukata tamaa, hawezi kuvumilia tena maisha, kugawa vitu vyake ama kuandika wosia kwa ghafla," alisema. Alisema anapoonekana mtu wa dalili hizo sio vizuri kuachwa peke yake, anatakiwa kufuatiliwa na kuongea naye kwa upole na kuonyeshwa upendo, kumjali na kumshauri.

"Mtu kama huyo usimchukulie kuwa amekosa ujasiri wa kuishi, mpe moyo na kumshauri apite kwa wataalamu wa afya kwa kuwa wengi wao tumewasaidia,"

INAENDELEA UK.25


## TARIME DISTRICT COUNCIL

### INVITATION FOR SUPPLY OF ONE (1) PORTABLE (LIGHTDUTY) DRILL RIGS

### TENDER NO. LGA/067/2019/2020/G/01

1. The Tarime District Council invites sealed tenders from eligible bidders for Supply of One (1) Portable (Light Duty) Drill Rigs:-
2. The Bidding will be conducted though National Competitive method of procurement as specified in the Public Procurement (Goods, Works, Non-Consultant services and disposal of public Assets by Tender) Regulations, 2013 and is open to all Bidders as defined in the Regulations unless otherwise stated in the Bid Data Sheet
3. Interested eligible bidders may obtain further information from and inspect the Bidding Documents at the Office of the Secretary Tender Board, Tarime District Council, P.O.BOX 16, Tarime from 8.30 am to 3.30 pm on Mondays to Fridays inclusive except on public Holidays.
4. A Complete of Bidding Documents in English may be purchased by interested Bidders on the submission of written application to the address above upon payment of a non refundable fee of Tshs.100,000/= (Tanzania shillings One Hundred thousand only). Payment should be through bank NMB DED-TARIME A/C. No.30410001496.
5. All bids in one original plus two copies, properly filled in, and enclosed in a plain envelope should be sent to the address below, The Secretary, Tarime District Council Tender Board, and P.O.BOX 16 Tarime at or before 10th October, 2019 at 10.00 am Local time. Bidds will be opened promptly thereafter in public and in the presence of bidders representatives who chose the attend in the opening at the Tarime District Council Head Quarter at Bomani area.
6. Late bids, electronic bids, and bids not received, bid not read out in public at the bid opening ceremony shall not be accepted for detailed evaluation irrespective of the circumstance.

**Apoo C. Tindwa**
**DISTRICT EXECUTIVE DIRECTOR**
**TARIME.**

215435902

# Ajali yaua wanajeshi 2, yajeruhi wengine 20

**Na Joctan Ngelly,**

KIGOMA

ASKARI wawili wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) wa Kikosi cha 24 KJ, wamefariki dunia na wengine 20 kujeruhiwa, baada ya gari walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kupinduka eneo la Hifadhi ya Katavi Mkoa wa Katavi.

Kaimu Mganga Mkuu Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kigoma (Maweni), Dk. Lameck Mdengo, alisema jana alipokea miili hiyo na majeruhi 20 ambao wamelazwa wodi namba saba , na hali zao zinaendelea vizuri.

Mdengo alisema baadhi ya majeruhi hao wamevunjika mikono na miguu, na wamepewa huduma ya kwanza na wamepelekwa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma/Ujiji Baptisti kwa ajili ya kupiga picha (x-ray) kutokana na X-ray ya Hospitali ya Rufani kuharibika.

Aliwataja waliyofariki dunia ni Bakari Mohamed Juma (38) na Rashidi Abed Mwimbe (28).

Pia aliwataja waliyojeruhiwa ni Bulati Abineli Chuma, Mutahidi Bakari Yusufu, Osca Aizaki Lyimo, Peter Anjero Kibasa, Ramadhani Hamisi Ally, Selemani Mohamed Nyangali, Saidi Iddi Kisogoli, George Aloyce George, Ezekieli John Ntinginya na Abdu Abduli Majura.

Majeruhi wengine ni Shabani Shabani Lyimo, Edimudi Emiliani Lyamtema, Hamisi Amad Bakari, Edward Sekijori Mshana, Onesfori Gerald Mhalwike, Rubeni Lucas Mpanda, Gofrey Alekizanda Kalinga, Jackson Ndoli Mlelwa, Maiko Samuel Samuel na Habuduel Shabani Shabani.

Alisema askari hao walikuwa wakienda kwenye shughuli zao za kikazi Mkoa wa Katavi, na chanzo cha ajali ni gari kuifeli break na kuacha njia na kupinduka.

Kamanda wa polisi Mkoa wa Kigoma, Martini Otieno, alipoulizwa na Nipashe kuhusiana na ajali hiyo kwa njia ya simu, alisema yeye yuko safari.

# JPM ateua M/kiti, wajumbe Bodi ya Ushauri

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Dk. Leonard Chamriho kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Ushauri ya Uwekezaji wa Mapato ya Mafuta na Gesi (Portfolio Investment Advisory Board).

Dk. Chamriho ni Katibu Mkuu wa Uchukuzi katika Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano.

Taarifa iliyotolewa jana na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, ilisema pamoja na uteuzi wa Mwenyekiti, Rais Magufuli amewateua wajumbe wanne wa bodi hiyo. Iliwataja wajumbe hao kuwa ni Casmir Kyuki (Katibu Mtendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria) na Dk. Suleiman Missango (Mkurugenzi wa Utafiti wa Uchumi na Sera wa Benki Kuu ya Tanzania - BoT).

Wengine ni Safiel Msomvu (Kaimu Meneja Uwekezaji wa Shirika la Maendeleo ya Petrol Tanzania -TPDC) na Dk. Mussa Budeba (Mhadhiri wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam – UDSM).

Taarifa hiyo ilieleza kuwa uteuzi wa Dk. Chamriho na wajumbe hao umeanza juzi Septemba 25.



Dereva wa bodaboda akiwa amebeba mzigo wa mkaa katika eneo la Ubungo Shekilango, jijini Dar es Salaam jana, unaomfanya ashindwe kuona nyuma kitendo ambacho ni hatari kwa usalama wake barabarani. **PICHA: JOHN BADI**

# Tasac yafuta ushuru usafiri majini

**Na Gidion Msabula,**
TUDARCo

SHIRIKA la Wakala wa Meli Tanzania (Tasac) limepiga marufuku na limeondoa tozo za ushuru wa forodha kwa mamlaka za usafirishaji wa majini zilizokuwa kero kwa huduma hiyo.

Utekelezaji huo unafanyika chini ya kifungu Na 4 cha Sheria ya Wakala wa Meli Tanzania ya mwaka 2017 Ibara ya 14 kutokana na agizo kutoka kifungu 12(1)(d) cha ibara ya sheria ya viwango na tozo katika sekta ya usafiri wa majini nchini.

Kwa mujibu wa tangazo lilitolewa kwenye vyombo vya habari, tozo hizo nane ni kati ya dola za Kimarekani 15 na 150. Kufutwa kwa tozo hizo kumetokana na kugundua kuwapo kwa tabia ya baadhi ya watoa huduma za usafiri wa majini kutoza tozo kwa kiwango kikubwa na kujipangia viwango vya kutoza wanapotoa huduma bila uthibitisho kutoka kwa mamlaka na bila mahitaji ya sheria husika.

Kwa mujibu wa tangazo hilo, kuna malalamiko mengi kutoka kwa watoa huduma kutoa majina yasiyo sahihi ya tozo za ushuru wa forodha ulioidhinishwa kwa kiwango ambacho kinasababisha kuwachanganya wateja.

Aidha, mamlaka hiyo imesema watoa huduma wote wa usafirishaji majini wanatakiwa kukataa kutoa tozo za ushuru wa forodha ambazo hazijaidhinishwa na mamlaka hiyo.

Pia Tasac imesisitiza kuwa endapo kutakuwa na ukiukwaji wa agizo hilo, hatua kali za kisheria zitachukuliwa ikiwamo kusimamishwa kutoa huduma au kunyang'anjwa leseni.

Aidha, tangazo hilo limebainisha kuwa watoa huduma wanatakiwa kuripoti kwa Tasac kama itatokea wanatakiwa kulipa ushuru wa forodha usioidhinishwa.



Mkuu mwenza wa mradi wa 'Women at Web Tanzania', Asha D. Abinallah, akiongea katika shughuli ya majadiliano juu ya ushirikishwaji wa jinsia na jinsi ya kuondoa pengo lililopo katika ulimwengu wa kidigitali. Shughuli hiyo iliwakutanisha washiriki wanawake ishirini pamoja na wanaume wachache wenye uwezo mkubwa wa kutumia mitandao ya kijamii wakiwa ni wadau muhimu, na wenye uwezo mkubwa wa kujadili mada husika ili kuweza kuweka misingi ya mpango mkakati wa kuhakikisha tatizo la 'mgawanyiko wa kidigitali' unapungua ama kuisha kabisa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Simbachawene awaondoa watumishi NEMC bandarini

**Na Enock Charles**

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), George Simbachawene, ameagiza kuondolewa mara moja kwa wakaguzi wawili wa bandari kutoka Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC) baada ya kuwapo kwa malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusiana na suala la vifungashio vya plastiki vinayokuja na bidhaa mbalimbali kutoka nje.

Akizungumza jijini Dar es Salaam baada ya kufanya ziara ya kushtukiza katika bandari ya Dar es Salaam juzi, Waziri Simbachawene alisema kumekuwa na changamoto nyingi ikiwamo suala la vifungashio na suala la mifuko mbadala pamoja na kanuni ziko wazi na zimebainisha vifungashio vya plastiki zinavyoruhusiwa na zisivyoruhusiwa.

"Kanuni ya 9 imebainisha vifungashio vya plastiki vinavyoruhusiwa ni ile inayotumika kwa ajili ya huduma za afya, bidhaa za viwandani, sekta ya ujenzi, sekta ya kilimo, vyakula, usafi na udhibiti wa taka.

Mnakwamisha biashara za watu hasa hawa wanaoingiza bidhaa za viwandani kama nguo. Ukishaondoa kifungashio kwenye nguo mpaka ifike dukani kutoka bandari itakua nguo kweli?" alihoji Simbachawene.

Mbali ya agizo hilo, Waziri Simbachawene alisema mkanganyiko huo unatokea

INAENDELEA UK.8

# Wafugaji wafurahia kufutwa mapori

**Na Mwandishi Wetu**

WAFUGAJI wamepongeza uamuzi wa serikali kufuta mapori ya akiba 12 ambayo yatagawanywa kwa wananchi na kuruhusu usajili wa vijiji 920 ndani ya hifadhi.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti juzi, baadhi ya wadau wa sekta hiyo walisema uamuzi huo wa serikali unalenga kumaliza migogoro iliyodumu kwa muda mrefu na kusababisha matatizo ikiwamo mapigano ya wakulima na wafugaji.

Mkurugenzi wa Mtandao wa Wafugaji Tanzania (Pingos Forum), Edward Porokwa, na Katibu Mtendaji wa Chama cha Wafugaji Tanzania, Magembe Makoye, walisema kwa kiasi kikubwa utapunguza au kumaliza migogoro mingi iliyowafanya wafugaji kuonekana wakimbizi nchini mwao.

Porokwa alisema uamuzi huo ni mzuri ingawa ulipaswa kufanyika mapema ili uendane na mabadiliko ya Sheria ya Wanyamapori ya mwaka 2009.

"Sheria ilimtaka waziri husika kufanya tathmini ya mapori ambayo hayajaendelezwa na ndani ya mwaka mmoja kuondoa yale yasiyo na sifa ya mapori tengefu, lakini jambo hilo halikufanyika," alisema.

Kwa mujibu wa Porokwa, uamuzi huo utasaidia kuondoa dhuluma kwa jamii za wafugaji, kufuta mapori tengefu kwenye maeneo ya vijiji, mita 500 (baffer zone) ndani ya vijiji, ambako wafugaji wanapigwa wakikutwa kwenye maeneo hayo wakiambiwa ni maeneo ya hifadhi na hivyo kuwa ni ukiukwaji wa haki za binadamu na kuzua malalamiko mengi.

Alisema ingawa hawajajua majina ya vijiji na mapori husika, matarajio ya wengi ni kuleta mafanikio na kwamba wananchi wanaweza kushiriki uhifadhi kwenye maeneo ya pembezoni na kwingine badala ya kuonekana maadui.

Aidha, alisema uwapo wa mpango wa matumizi bora ya ardhi kwa vijiji ni habari njema na kilio cha muda mrefu ambacho kinakwenda kuwa suluhisho ya migogoro ya ardhi.

Kuhusu migogoro mikubwa iliyopo kwenye eneo la Longido, alisema asilimia 80 ya

INAENDELEA UK.8

## Kesi ya Rugemarila, Sethi kutajwa Okt. 10

**Na Hellen Mwango**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imepiga kalenda kesi ya uhujumu uchumi inayowakabili wafanyabiashara wawili, Harbinder Sethi na James Rugemarila mpaka Oktoba 10, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Kesi hiyo imetajwa jana mbele ya Hakimu Mkazi, Vick Mwaikambo, baada ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, anayesikiliza kesi hiyo kuwa na udhuru wa kikazi.

Upande wa Jamhuri ukiongozwa na Mwendesha Mashtaka wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), Leonard Swai ulidai kesi hiyo upelelezi wake bado haujakamilika na aliomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu alisema kesi hiyo itatajwa Oktoba 10, mwaka huu na washtakiwa walirudishwa rumande.

Katika kesi ya msingi washtakiwa hao, wanakabiliwa na mashtaka 12 ya uhujumu uchumi ikiwamo kula njama, kujihusisha mtandao wa uhalifu, kighushi, kutoa nyaraka za kughushi, kujipatia fedha kwa njia za udanganyifu, kutakatisha fedha na kuisababisha hasara ya Dola za Marekani 22, 198,544.60 na Sh. 309,461,300,158.27.




Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Wanaouza maji mijini waanze kumulikwa

**MAJI** ni hitaji la msingi kwa watu wote bila kujali wanaishi mijini au vijijini. Shida ya huduma hiyo ya maji kwa watu wengi inaanza msimu huu wa kiangazi.

Hiki ndicho kipindi kinamama wengi wanaanza kupata tatizo la msongo kwa ajili ya maji. Hii ni kutokana na ukweli kuwa visima ni vifupi, mito na mabwawa hukauka kutokana na kiangazi kikali ambacho wakati mwingine huchukua kati ya miezi minne hadi sita kuanzia Oktoba hadi Machi.

Tunaona kuwa huu ndiyo wakati wa kuliangalia tatizo la maji kwenye miji na hata vijijini ili mamlaka zinazoshughulikia upatikanaji wa huduma hii zibuni mbinu za muda mrefu pamoja na mfupi kumaliza tatizo hilo.

Wakazi wengi wa Dar es Salaam ambao hawana miundombinu rasmi ya maji watakubaliana nasi kuwa msimu huu ndicho kipindi chenye changamoto kubwa ya 'stress za maji'.

Yapo baadhi ya maeneo ambayo wananchi hunywa maji ya madimbwi, visima vifupi na hata maji ya mabwawani au matopeni ambayo yametuama kwa muda mrefu tangu msimu wa masika ulipomalizika Mei. Hupata taabu kuanzia mwezi Oktoba kutokana na jua kali, ukame na upepo ambao unakausha vyanzo hivyo. Hili linafahamika kwa kina na mamlaka za maji.

Ndiyo maana tunataka kupendekeza ufumbuzi wa muda mfupi kwa baadhi ya maeneo ambayo hayana maji ili wananchi wapate huduma hiyo na kuepukana na kipindupindu, kuhara, taifodi na maradhi ya ngozi.

Tunapenda kushauri kuwa kama ambavyo mamlaka za kudhibiti usafiri hutoa vibali kwa wasafirishaji kusaidia huduma za usafirishaji mwisho wa mwaka, mamlaka za maji ikiwamo Dawasa kwa Dar es Salaam, isajili kampuni binafsi zinazotambulika kisheria kuwapatia wananchi maji kwa bei elekezi.

Tunasema bei elekezi kwa vile maji hayo yanauzwa na Dawasa kwa bei isiyowaumiza wafanyabiashara hao, hivyo nao wanawajibika kuwauzia wananchi kwa bei ambayo haitawaumiza.

Licha ya kuwapo kwa magari binafsi yanayosambaza maji mijini tunaona umuhimu wa kuangalia suala la viwango na usafi wa vyombo vinavyotumiwa kubeba na kusambaza maji hayo. Tunasema hayo kwa sababu, tunaona kuwa matangi meupe ya lita 1,000 yanayotumiwa kuuza maji mijini hasa Dar es Salaam, hakuna anayefahamu usalama na usafi wake hivyo ni wakati wa Dawasa na Shirika la Viwango (TBS) kuandaa maelekezo ya matangi salama na yenye kiwango kwa ajili ya kuuza maji kwa wateja wa mitaani.

Tuna wasiwasi kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara wanaweza kukurupuka na kuuza maji bila kuzingatia viwango hali ambayo inatatiza afya za walaji ambao kutokana na tatizo la huduma hiyo hawana pa kukimbilia.


Mathalani, matangi hayo yanaingizwa nchini kupitia bandarini na mengi yalikuwa yanatumiwa kuweka kemikali, pengine nyingine ni za sumu kwani hakuna anayefahamu, lakini ndivyo vyombo vinavyotumiwa kusambaza maji mitaani, Dawasa na kwingineko inawahakikishiaje wateja usalama wao?

Tunaona kuwa haitoshi kuwaruhusu watu binafsi kuuza maji wakati hakuna wa kudhibiti ubora, ndiyo maana tunashauri kampuni rasmi zisajiliwe na kuuza maji mitaani kwenye vyombo vyenye viwango badala ya kuwaacha wafanyabiashara kuendelea na vurumai zinazofanyika sasa.

Tunaishauri Dawasa na mamlaka nyingine mijini kuwa karibu na wananchi msimu huu wa ukame ili kutatua changamoto zao kutokana na ukweli kuwa msimu wa kiangazi na ukame unaanza na kuleta matatizo ya maji kwa wengi.

Tunatoa wito kwa Wizara ya Maji na Umwagiliaji kuangalia upya biashara ya magari binafsi yanayouza maji mitaani ili kulinda afya za walaji.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima

# Itakwisha lini shida basi kujaza mafuta ina abiria?

Na Amri Lugungulo

**SIKU** zote tumezoea kusema ajali haina kinga. Katika sura ya kwanza kuanzia kwenye msingi wa methali, ni kweli wakati mwingine kuna yasiyozuilika kuhusu ajali.

Pia katika sura nyingine, uhalisia unaturudisha katika sura ya pili, kwamba tusiegemee katika methali, bali tudodose macho, masikio na hisia zetu katika haya kupata uhalisi ulikosimama mahali hatari iliko ya mafuta ya petroli.

Kwa kweli serikali na baadhi ya watu binafsi, wamekuwa wakikemea tabia ya baadhi ya madereva, husussani wa mabasi ya abiria ambao huingia kwenye vituo vya mafuta wakiwa wamebeba abiria bila ya kujali kitendo hicho ni hatari au la.

Kumeshashuhudiwa si mara moja au mbili ajali na watu wanalalamika, pia majanga. Serikai nayo imeingilia ikitumia mamlaka yake, kuagiza vituo vyote vya mafuta nchini kwamba ni marufuku kuweka mafuta, basi likiwa na abiria. Sharti lake washuke kwanza.

Imekuwa hadithi ya agizo likifanyiwa kazi katika 'siku mbili tatu' na kuendelea katika namna ileile ya tabia iliyokuwapo zamani.

Kwetu sisi wenye umri mkubwa, hatuoni mabadiliko ya namna yoyote kadri miaka inavyosonga. Inaniuma sana, nikijua namna ajali hizo zinadhuru. Ni juzi tu tuna ushuhuda madhara yatokanayo na ajali za namna hii, kwa kile kilichotokea mjini Morogoro na tunaweza kufuatilia mengineyo mahali pengine.

Kitendo hicho kinaleweka ni hatari kwa kuwa unapotokea mlipuko wa mto wakati gari hilo likinyonya mafuta, bila shaka ajali kuna hatari kubwa ya kufa watu kwa moto unapotatokea.

Jamani, ifahamike kuwa ajali hiyo inaweza kupata kinga kama madera na wauza mafuta wangekuwa na busara ya kikabili uhalisia.

Busara hiyo ingeweza kupatikana iwapo upande wa madereva wataamua kwenda kituoni bila ya kuwa na abiria, kwani hata ajali ikitokea inakuwa katika mazingira ya ama nafuu au walau inazuilika.

Kwa upande wa wauza mafuta, ni vizuri nao wakawa na mwongozo katika kila kituo kwa dereva atakayeingiza gari akiwa na abiria, asipewe mafuta hadi hapo atakapowashusha abiria ili awe mbali na balaa hilo.

Hata hivyo, dereva ni vyema awe na busara zaidi kuhakikisha anaingia kituoni bila ya kuwa na abiria, badala ya kusababisha usumbufu kwa abiria, akiwashusha ili apate fursa ya kunyonya mafuta.

Bila ya shaka ushauri huu utakuwa miongoni mwa njia ya kuepuka ajali za moto, pindi sehemu kubwa ya jamii inatambua ajali ya moto na hatari zake zinaendelea kushuhudiwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Endapo madereva na wauza mafuta kituoni, wataonekana kusababisha ajali kama hiyo, watakuwa wanawajibika nayo.

Utataratibu pindi utakapozingatiwa, naamini 'ajali itakuwa na kinga' isipokuwa watoa huduma ndio chanzo cha ajali na kutegeua usemi huo.

Mara nyingi kumekuwapo ajali kama za moto, ambazo husababishwa na kukosa umakini. Chonde chonde Watanzania tuwe makini kuepuka ajali zinazoweza kudhibitiwa.

Ni wadau wote wakiwemo abiria, vyombo vya sheria na wamiliki wa vituo vya mafuta kuzuia ajali kama za moto ambazo ni janga kubwa linalosababisha vifo na vilema vya kudumu.

Ni tabia iliyozoeleka kwa madereva wengi nchini, kwamba hawajali kelele za umma, viongozi na abiria wao. Wanajihisi wao ndio wao.



Mmoja wa majeruhi ambao ni askari wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kikosi cha 24KJ, waliopata ajali baada ya gari lao walilokuwa wakisafiria kuacha njia na kupinduka, eneo la Hifadhi ya Katavi mkoani Katavi, baada ya kufikishwa katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kigoma Maweni jana. **PICHA: JOCTAN NGELLY**

# Nida kurahisisha utoaji Kitambulisho cha Taifa

**Na Romana Mallya**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (Nida), imesema inakuja na mpango madhubuti wa kutengeneza vituo maeneo yenye watu wengi kuendana na kasi ya usajili wa laini za simu kabla ya Desemba 31, mwaka huu.

Pia, imetoa msisitizo kwa Watanzania kuwa kitambulisho cha Taifa ni muhimu kwa sababu ndicho kinachotumika katika usajili wa mambo muhimu.

Akizungumza katika kipindi cha asubuhi cha East Africa Redio, Msemaji wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa NIDA, Thomas William, alisema kuwa, matumizi ya vitambulisho ni mapana na mwitikio wa uhitaji nao ni mkubwa.

"Mfano Mkoa wa Dar es Salaam eneo la Kawe idadi ilikuwa ni kubwa kwa sababu laini za simu zinasajiliwa kabla ya Desemba 31, mwaka huu, Nida tumeamua kuongeza vituo kwa sasa kipo Bunju (Wilaya ya Kinondoni) Mbagala, Changombe Usalama (Wilaya ya Temeke).

"Tunakuja na mpango madhubuti kuhakikisha kwamba tunatengeneza vituo mbalimbali kwenye maeneo yenye watu wengi Mkoa wa Dar es Salaam ili tuwahudumie wananchi bila shida," alisema. Kuhusu umuhimu wa kitambulisho hicho, William alisema Nida inamtaka Mtanzania apeleke vielelezo vikiwamo vyeti vya shule.

"Kama una vyeti vya darasa la saba, sekondari, sekondari ya juu, kama hivyo huna leta hata leseni ya bodaboda, tupe hata TIN namba, au kama una hati ya kusafiria tuletee, kama ni Mzanzibar tunahitaji kitambulisho cha mkaazi, ili tuweze kujua kweli unakaa Zanzibar," alisema.

Alisema Nida imeweka wigo mpana ili kumtambua mtu kwa sababu bila vielelezo hawawezi kujua huyo ni nani na matokeo yake akapewa asiyestahili.

"Vitu hivi tumeviweka na huwa tunasisitiza ni vizuri wananchi wawe na nyaraka, mfano ukienda Rita (Wakala wa Usajili Ufilisi na Udhamini), hawana ukomo wa kusajili tukio la kizazi, ingawa mtu akizaliwa anapewa tangazo la kuzaliwa, ni vizuri mtu kuwa na vielelezo vya kuthibitisha zile taarifa zake," alisema na kuongeza:

"Lazima tufanye uchujaji wa taarifa za watu ili tuhakikishe taarifa hizi zinatumiwa na mifumo mingine ili mambo yaende sawa."

Kuhusu kitambulisho cha mzazi mtu anapotaka kitambulisho cha taifa, alisema miaka hiyo hakukuwa na utaratibu wa kutoa cheti cha kuzaliwa ndiyo maana Nida imetoa wigo mpana.

"Vielelezo hivi siyo kila mtu atakuwa navyo kwa mfano huwezi kumbana mtu niletee hati ya kusafiria, mtu yupo nchini hajawahi kutoka kwenda nje na hana sababu ya kwenda, lakini ndiyo maana tukasema tuweke wigo mpana wa kumtambua mwombaji.

"Vielelezo hivyo tunaviomba kwa kadiri anavyokuwa navyo vingi tunahitaji, lakini siyo lazima awe navyo vyote tulivyotaja. Tunavihitaji vingi kwa sababu vinamsaidia mwombaji mwenyewe," William alisema na kuongeza:

"Kwa mfano sasa hivi mimi na wewe kwa umri wetu, labda unataka kuomba au kubadilisha kazi, kutoka hapa kuja serikalini, ili uajiriwe serikalini lazima uwe na kitambulisho cha taifa au namba ya utambulisho wa taifa.

Alisema mtu anapoweka taarifa zake ni sawa kutunza kwenye benki kwa sababu Nida ina kanzi data inayotunza taarifa za watu.

"Wakati mwingine vinaweza vikawa nje ya hivyo vinavyohitajika kwa sababu Idara ya Uhamiaji ambayo wanahoji uraia wanaweza wakaja hata nje ya hivyo wakataka taarifa za bibi yako kama hawajajiridhisha na uraia wako, inaweza ikawa nje ya yiambatisho nilivyovitaja," alisema.

Kuhusu gharama ya vitambulisho alisema kinatolewa bure kwa Mtanzania kwa mara ya kwanza, lakini mtu akipoteza au kukiharibu atalipia Sh. 20,000.

# Mamlaka zaagizwa kupanga bei ya gesi

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, ameziagiza mamlaka zote zinazohusika na upangaji wa bei ya gesi asilia kufanya mapitio na kuja na bei mpya itakayozinufaisha pande zote.

Alitoa maelekezo hayo hivi karibuni kwa nyakati tofauti wakati wa ziara ya kiwanda cha kutengeneza vigae cha Goodwill na kiwanda cha kufua vyuma cha Lodhia, vyote vya Wilaya ya Mkuranga, mkoani Pwani.

Pia, alitoa mwezi mmoja kwa uongozi wa Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), Mamlaka ya Udhibiti wa Nishati na Maji (Ewura), Mamlaka ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA), Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali pamoja na wataalamu wa wizara, kufanya mapitio ya bei za gesi viwandani ili ziwawezeshe wawekezaji kuzalisha kwa tija.

Kwa mujibu wa waziri huyo, kumekuwa na malalamiko kutoka kwa wawekezaji mbalimbali wenye viwanda hivyo kuwa gharama ya gesi asilia iko juu na kuiomba serikali iangalie uwezekano wa kuipunguza ili wazalishe kwa tija zaidi.

"Lengo la serikali ni kujenga mazingira rafiki ya uwekezaji ili kuvutia wawekezaji zaidi kuwekeza nchini hivyo naagiza muanze mara moja kufanya mapitio ya bei husika. Mje na bei linganifu ili kila upande unufaike," alisema.

Aliwataka wataalamu kuangalia kwenye nchi nyingine zenye gesi asilia kabla ya kufanya uamuzi. "Sasa, kadiri unavyokuwa mbali kutoka kwenye eneo la kuchakata gesi, ndivyo gharama inavyoongezeka. Bei ya gesi kwa yule aliye karibu na eneo la uchenjuaji haiwezi kulingana na aliye mbali."

Bei ya sasa ya gesi asilia inaanzia Dola za Marekani 4.7 hadi 7.72 kwa uniti moja.

# Wakutana kujadili mabadiliko tabianchi

**Na Romana Mallya**

WASOMI na wadau kutoka nchi mbalimbali wamekutana jijini Dar es Salaam kujadili namna ya kutatua changamoto za mabadiliko ya tabianchi na jinsi jamii kukabiliana na tatizo hilo.

Akifungua jana kongamano la kimataifa la kijiografia lijulikanalo kama GAT, Katibu Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Dk. Leonard Akwilapo, alisema jiografia ni maisha kwa kuwa inaangalia, kilimo, afya, ajira na maisha ya kila siku.

Kongamano hilo la siku tatu linafanyika Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Kigamboni na limekutanisha wadau kutoka Afrika Kusini, Ethiopia, Nigeria, Zambia na wenyeji Tanzania

Akizungumza kwenye kongamano hilo, Dk. Akwilapo alisema jamii inavyopambana na mazingira ndivyo inavyochangia katika kukuza uchumi wa nchi husika.

Mkuu wa MNMA, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema pamoja na majukumu mengine ya chuo, wanawajibika kufanya utafiti.

"Kupitia kongamano hili wadau wanapata fursa ya pamoja ya kujadili kuonyeshana namna ya kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika jamii kutokana na mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Alisema mabadiliko ya tabia nchi ni changamoto katika sekta zote hivyo kukutana kwa wataalam hao watatoa mapendekezo ya namna ya kukabiliana nazo.

Naye Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Mkwawa, Dk. Evaristo Haule, alisema GAT imejikita kufanya kazi na watafiti na wana taaluma katika masuala ya jiografia.

Alisema wamo watunzaji wa wanyama, utunzaji wa maliasili, uchumi wa viwanda na masuala ya mabadiliko ya tabianchi.

# Simbachawene awaondoa watumishi NEMC bandarini

INATOKA UK. 5

kutokana na watumishi kukosa uweledi wa taaluma au kazi wanazofanya. Hivyo kupelekea watumishi hao kufanya kazi kwa kubahatisha na kukosa ufanisi katika utendaji kazi wao na kuchangia usumbufu hasa kwa wafanyabiashara wanaoingiza bidhaa mbalimbali za viwandani nchini kutoka nje.

"Kama mtu ni mhandisi wa maji basi apangwe sehemu itakayoendana na taaluma yake.

Kuna watu wenye taaluma kama sheria, ufungashaji na nyingine nyingi ambazo wangeweza kufanya kazi hii kwa ufanisi.Msingi wa sheria ni kufanya maisha ya wananchi wanaoitumia kuwa mazuri na si vinginevyo," alisisitiza.

Aidha, Waziri Simbachawene aliagiza watumishi kutoka NEMC kitengo cha ukaguzi bandarini kufanya kazi saa 24 wakishirikiana na watumishi kutoka taasisi nyingine za serikali ili kuongeza nguvu kazi katika suala zima la ukaguzi wa mizigo inayoingia nchini.

"Ufanisi wa bandari upo kwenye utoaji na uingizaji wa mizigo ndani na nje ya nchi. Ikibidi nguvu kazi iongezeke ila wale wenye taaluma zinazoendana na kazi hii ili ifanyike kwa haraka na uhakika."aliongeza waziri.

Alisema kanuni zimebainisha mtu yeyote anayeingiza nchini, anayesafirisha nje ya nchi au anayezalisha vifungashio vya plastiki ambavyo havijazuiwa na kanuni hizi, anatakiwa kuhakikisha vifungashio hivyo vinakidhi viwango vya ubora vilivyowekwa na Shirika la Viwango Tanzania (TBS).




Ofisa wa Huduma kwa Wateja wa Benki ya NBC, Oswald Kashasha (kulia), akiendesha usajili wa kidijitali kwa mmoja wa wateja wa benki hiyo, jiijini Dar es Salaam jana. Kampeni ya kuhamasisha huduma hiyo imezinduliwa rasmi jana. Wanaoshuhudia ni Mkuu wa Tawi la Kati la benki hiyo, Mariam Kombo (kushoto). Habari Uk. 21. **MPIGAPICHA WETU**

# Waziri Lugola azionya NGO

INATOKA UK. 2

Aidha, alisema wamebaini kwamba inapotokea haki kuminywa ndipo milipuko ya kwamba kuna kuvunjika haki ya binadamu hutokea.

"Rai kwa kituo mwendelee kufanya kazi kwa weledi bidii na moyo wa kujituma ili kuhakikisha Watanzania wenye shida mbalimbali wanafikiwa na kutatuliwa shida zao kwa misingi ya sheria na taratibu za nchi na haki inaambatana na wajibu, hivyo ni vyema tunavyohubiri haki za binadamu, tuhubiri pia na wajibu wa kila raia," alisema.

Kangi alisema anatamani siku moja lianzishwe shirika lisilo la kiserikali linalohubiri na kutetea suala la wajibu kikatiba.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema kituo hicho kitahakikisha mipango ya serikali inatekelezwa kwa urahisi kwa kuwaandaa wananchi kutambua wajibu wao.

"Tunaamini kwamba jamii inayoheshimu na kulinda haki za binadamau pia itaheshimu wajibu na kufanya kazi kwa bidii na kuendeleza amani na ushirikiano wa umoja wa kitaifa," alisema.

Alisema kituo hicho kinaadhimisha miaka 25 ya kuanzishwa kwake na kimeunga mkono jitihada za serikali za kuifanya Dodoma kuwa makao makuu ya nchi kwa kufungua ofisi yake jijini humo.

# Amwandikia barua DPP asamehewe kesi

INATOKA UK. 2

wanaomba tarehe ya karibu ili kufanya utaratibu unaotakiwa kwa mujibu wa sheria.

Baada ya maelezo hayo, Wakili Simon alidai kuwa upelelezi wa shauri hilo umekamilika na hawana pingamizi na maelezo ya upande wa utetezi.

Hakimu Simba aliahirisha kesi hiyo hadi leo itakapokuja kwa ajili ya kutajwa na kukamilisha taratibu.

0000

WAZIDI KUMIMINIKA

Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, amesema washtakiwa wanaotuhumiwa na kesi za uhujumu uchumi, wameendelea kumiminika kuomba msamaha na kukiri kosa kama alivyoagiza Rais John Magufuli.

Nipashe jana ilipomtafuta DPP Mganga ili kujua hadi sasa ni watuhumiwa wangapi waliojitokeza na kiasi ambacho kinatarajiwa kukusanywa baada ya watu hao kuitikia wito wa Rais Magufuli, alisema kwa wakati huo idadi yao hana kwa sababu bado hajawahesabu.

"Sijawahesabu walioitikiwa wito, ila wanaendelea kujitokeza," alisema na kuhusu kiwango cha fedha ambacho kinatarajiwa, alisema: "Kiwango siwezi kukijua kwa sababu hata idadi yao hapa sina."

Baada ya maagizo ya Rais John Magufuli aliyoyatoa Jumapili, siku iliyofuata, Mganga alieleza utaratibu ambao watuhumiwa hao wanatakiwa kuufuta.

Rais Magufuli wakati akiwaapisha viongozi mbalimbali wa serikali aliowateua wiki iliyopita, alisema watuhumiwa hao kama wako tayari kuomba msamaha, kukiri makosa yao pamoja na kurudisha fedha walizotakatisha, wasikilizwe na hata kusamehewa.

# Wafugaji wafurahia kufutwa mapori

INATOKA UK. 5

wilaya ni mapori tengefu, vijiji zaidi ya 23 vipo ndani ya pori tengefu na ni vijiji vilivyosajiliwa.

Aidha, alisema asilimia 65 ya Wilaya ya Simanjiro ni mapori tengefu, na kwamba uamuzi huo utawamilikisha wananchi ardhi na wapange matumizi endelevu ya kunufaisha pande zote.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Wafugaji Tanzania, Makoye, alisema Rais John magufuli amethubutu kufanya jambo ambalo siyo rahisi, na kwamba maeneo ya hifadhi yanapotengwa yanalindwa kisheria tofauti na maeneo ya wananchi.

"Wafugaji wamehangaika kwa miaka mingi kwa ajili ya malisho, wahifadhi wanahitaji kwa ajili ya hifadhi, wawekezaji kwa ajili ya uwekezaji ila wafugaji ndio wanyonge kwa kuwa wanafukuzwa na kukosa ardhi na ndiyo sababu ya kuhamahama," alisema.

Kwa mujibu wa Makoye, mahitaji ya ardhi yamewafanya kuwa wakimbizi kila mahali wanahamahama na kufukuzwa, huku hitaji lao kubwa likiwa ni kupata maeneo kwa ajili ya malisho.

"Mapori tengefu mengi walishayaacha na kuna shughuli za binadamu zinaendelea na wananchi wamejenga makazi kwa kuwa hayajaendelezwa na walipowakuta wananchi waliwachomea nyumba," alisema.

Makoye alisema kinachosubiriwa ni kuyatambua mapori yaliyofutwa kama ni mapya au ya zamani ambayo tayari wananchi walishaishi humo, na kwamba kama yatakuwa ni mapya itasaidia kwa kuwa wafugaji watapata ardhi.

Aidha, alisema kwa sasa nguvu kubwa inaelekezwa kuwaelimisha wafugaji kufuga kisasa na kuwa na ufugaji endelevu ambao utawawezesha kutumia eneo litakalotengwa na siyo kuwa kero kwa wengine.

"Tunaomba watendaji wa serikali wawe wakweli kwa Rais kwamba hayo ni maeneo mapya au ni yale ambayo tayari wanaishi humo, kama ni mapya ambayo yaliachwa bila kuendelezwa basi itakuwa ni habari njema zaidi kwa wafugaji," alisema Makoye.

# Sensa 2022 kufanyika kidijitali

INATOKA UK. 2

alama ili kesho yake unaanzia hapo. Ukianzia sehemu nyingine tofauti na hapo 'system' inakukataa hadi urudi ulipoishia kuhesabu,"alisema.

Kadhalika, alisema katika mfumo huo wakuu wa mikoa, wabunge na viongozi wote watakaokuwa wanawajibika kwenye sensa wataunganishwa na kufuatilia kila hatua na kutoa maoni yao kulingana na zoezi litakavyokuwa likifanyika.

Alibainisha kuwa sensa ya mwaka 2022 ikikamilika NBS itakuwa imefanya kazi kubwa kwa Taifa kwa kuwa hakuna Mtanzania atakayeachwa bila kuhesabiwa.

Sambamba na hilo, mtakwimu huyo alisema matumizi ya teknolojia hiyo yatapunguza idadi ya watu wa kutenga maeneo kutoka 130 waliohusika mwaka 2012 hadi 25 ambao watakuwa katika timu tano kwa mwaka huo.

"Sensa ya mwaka 2012, tulitenga maeneo ya kijiografia 100,008 ambapo eneo moja ni mtu mmoja ndivyo ilivyo principle lakini mwaka 2022 tunatarajia kuna maeneo 200,000 hivyo wadadisi wa kuhesabu watu wataongezeka hadi 200,000 na itakuwa ni rahisi watafanya kazi kwa urahisi, idadi ya kaya zimepunguzwa wakati ule kulikuwa na kaya 100,"alisema.

## HABARI KITAIFA

# JPM amteua Mwinyi kuongoza MUHAS

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amemteua Rais mstaafu, Alhaji Ali Hassan Mwinyi, kuwa Mkuu wa Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS).

Mwinyi ameteuliwa kuendelea na wadhifa huo kuanzia juzi.

Rais Magufuli pia amefanya uteuzi wa wenyeviti wanne wa bodi za taasisi mbalimbali.

Kwanza, Rais Magufuli amemteua, Prof. Mayunga Nkunya kuwa Mwenyekiti wa Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania (TCU).

Prof. Nkunya anachukua nafasi ya Prof. Jacob Mtabaji ambaye muda wake umemalizika. Prof. Nkunya ni Katibu mstaafu wa Baraza la Vyuo Vikuu vya Afrika Mashariki (IUCEA).

Pili, Rais Magufuli amemteua, Prof. Idrissa Bilali Mshoro kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Rural Water Supply and Sanitation Authority - RUWASA). Prof. Mshoro ni Profesa wa Uhandisi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Rais Magufuli pia amemteua, Prof. Elias Tozo Bisanda kuwa Mwenyekiti wa Bodi wa Tume ya Taifa ya Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO). Prof. Bisanda anashika wadhifa huo kwa kipindi cha pili.

Kadhalika, Rais Magufuli amemteua Prof. Apollinaria Pereka kuwa Mwenyekiti wa Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (DIT). Prof. Pereka anashika wadhifa huo kwa kipindi cha pili.

Taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi John Kijazi, imeeleza kuwa uteuzi wa wenyeviti hao ulianza juzi.



Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Kangi Lugola (kulia), akikata utepe kuzindua rasmi Ofisi ya Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), katika eneo la Area D, jijini Dodoma jana. Wengine ni Mwenyekiti wa Bodi ya Kituo hicho, Prof. Geoffrey Mmari (kushoto) na Mkurugenzi Mtendaji wa kituo hicho, Anna Henga. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kanyasu: Bodaboda zitumike kudhibiti wasafirishaji wa mkaa

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Waziri wa Maliasili na Utalii, Constantine Kanyasu, amewataka watendaji wa Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) waanze msako kwa kutumia bodaboda (pikipiki) ikiwa ni mbinu mpya ya kukabiliana na wananchi wanaosafirisha mazao ya misitu kwa kutumia baiskeli na pikipiki.

Amesema watumiaji wa vyombo hivyo wamekuwa wakikwepa kulipa kodi na tozo stahiki na hivyo kuisababishia serikali kupoteza mapato yake.

Kanyasu alitoa agizo hilo jijini Dodoma wakati akifungua kikao maalumu cha utendaji ambacho kimewakutanisha viongozi wa TFS kuanzia makao makuu hadi ngazi ya wilaya.

"Anzeni kufanya doria kwa kutumia pikipiki kama ilivyo kwa Jeshi la Polisi linavyotumia pikipiki kuwanasa baadhi ya watuhumiwa," alisisitiza Kanyasu.

Kanyasu alisema pikipiki na baiskeli zimekuwa zikisafirisha magunia ya mkaa ambayo ni mengi yanayoweza kusafirishwa na lori. Katika mkutano huo, Kanyasu aliwaonya watendaji hao waache kutumia vizuizi ikiwa pamoja na kufunga kamba barabarani kwa ajili ya kuwakamata waendesha pikipiki na baiskeli waliobeba mkaa hali inayopelekea wahalifu kuanguka na kuumia wakati wakijaribu kukimbia ili wasikamatwe

Badala yake aliwataka watendaji hao watumie pikipiki katika kupambana nao ili kuwaepusha na madhara wanayoweza kuwapata watuhumiwa hao endapo watatumia vizuizi barabarani.

"Ninyi mmepitia mafunzo ya Jeshi USU ni lazima mwende sambamba na njia wanazozitumia wahalifu, anzeni kutumia bodaboda kama wao wanavyotumia," alisisitiza Kanyasu.

Aliongeza kuwa usafirishaji huo kwa njia ya pikipiki na baiskeli lazima udhibitiwe kwa kutumia mbinu rafiki za kuwanasa bila kuwasababishia madhara waendeshaji wa vyombo hivyo.

Aidha, Kanyasu ametoa onyo kwa wasafirishaji mkaa wanaotumia pikipiki na baiskeli kuwa waache mara moja la sivyo hawatasalimika.

Kwa mujibu wa mwongozo wa uvunaji endelevu wa mazao ya misitu ya asili wa mwaka 2015, vyombo vinavyoruhusiwa kusafirisha mazao hayo ni vyenye magurudumu manne.

Katika hatua nyingine, Kanyasu aliwataka watendaji wa TFS waelekeze nguvu zao zaidi katika kuzuia miti isikatwe badala ya kukimbizana na wasafirishaji wa mazao ya misitu ikiwa tayari mazao yapo barabarani.

"Nawakumbusha kazi yenu ya msingi ni kulinda misitu isiharibiwe na sio kuacha misitu iharibiwe ndipo muanze kukimbizana na wasafirishaji haramu huko barabarani."

Aliongeza kuwa katika jamii kumekuwa na hisia kuwa kukata miti sio kosa ila linakuwa kosa pale unaposafirisha.

Kanyasu alisema pikipiki na baiskeli vimechochea kwa kiasi kikubwa uharibifu wa misitu, ambapo kwa mujibu wa taarifa zinaonyesha kuwa mkaa husababisha upotevu wa wastani wa hekta 372,000 za misitu kila mwaka.

Alisema uvunaji huo hupoteza walau asilimia 1.1 ya eneo lote la misitu nchini.

# Wasichana 600 warejeshwa shule

**Na Dege Masoli,** TANGA

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Brac Maendeleo Tanzania, limewarejesha shuleni wanafunzi wakike 600 waliokuwa nje ya masomo kutokana na changamoto mbalimbali ikiwamo hali duni za kiuchumi ndani ya familia na mimba za utotoni.

Meneja wa mradi wa elimu na uwezeshaji wasichana wa Shirika hilo Mkoa wa Tanga, Manoah William, alisema hayo kwenye warsha ya siku mbili ya waandishi wa habari iliyoandaliwa na shirika hilo kwa ajili ya kueleza shughuli zake na kujenga uhusiano mzuri na vyombo vya habari.

Manoah alisema tangu kuanza mradi huo mwaka 2015 jumla ya wanafunzi 600 kati ya 1,500 waliofikiwa wakati wa utafiti na uhamasishaji kwa watoto walio nje ya shule waliweza kurejeshwa madarasani na kuanza masomo.

Manoah alisema licha ya kazi ya uhamasishaji huo mkubwa, lakini baadhi ya wasichana hawajakuwa tayari kusoma licha ya gharama kulipiwa na shirika hilo. Alieleza kuwa katika kuhakikisha wasichana hao wanaenda shule, shirika limejenga madarasa 12 mapya na ya kukarabati, huku wakiajiriwa walimu 140 pamoja na wasimamizi wa vituo hivyo 35.

Naye Meneja wa Mawasiliano wa Brac Maendeleo Tanzania, Emma Mmbaga, alieleza kuwa shirika hilo limejigawa kiutendaji katika aina mbili likiwamo la Brac Maendeleo Tanzania linalojihusisha na masuala ya elimu na Brac Finance lililojikita kwenye utoaji wa mikopo kwa wanawake.

Mmbaga alisema pamoja na miradi hiyo ya elimu na mikopo, shirika hilo linatekeleza sera ya ulinzi kwa mtoto ili pamoja na mambo mengine liweze kuzingatia haki yao kwa mujibu wa maelekezo ya kimataifa.

Kwa upande wa ulinzi wa mtoto, alielezea baadhi ya kanuni, taratibu na sheria zinazosimamia ulinzi huo katika masuala yanayohusu habari kuwa ni pamoja na kuzingatia ridhaa ya mlengwa kuhusiana na taarifa zake, kuangalia mavazi ya mtoto husika kama yamezingatia maadili.

# Sitta: Wanawake ni viongozi 'supa'

**Na Yasmine Protace**

MBUNGE wa Urambo mkoani Tabora, Margareth Sitta, amesema katika nyanja mbalimbali za uongozi, wanawake wamefanya vizuri kutokana na kujiamini na kuthubutu.

Sitta aliyasema hayo jana, katika Tamasha la Jinsia lililokuwa likizungumzia ushiriki wa wanawake katika nafasi za uongozi.

"Katika nyanja mbalimbali tumeona wanawake wakifanya vizuri kutokana na kujitambua kwao na kuthubutu," alisema Sitta.

Aliongeza kuwa wanawake wakiwezeshwa wanaweza hata kuleta mabadiliko makubwa katika sehemu wanazoshika nafasi za uongozi.

Alisema ni wajibu wa wanawake kwenda mbele na kutorudi nyuma kwa kujitosa kugombea uongozi wa maeneo mbalimbali.

Alisema ushiriki wao utasaidia kuwapo kwa ushawishi mkubwa katika kuleta mabadiliko na maendeleo.

Akizungumzia kuhusu idadi ya wanawake bungeni alisema kuwa kila mara inaongezeka kila panapofanyika uchaguzi.

Alisema wanawake wakiwa wengi bungeni kutakuwa na umoja wa kupaza sauti kwa pamoja.

Aliongeza kuwa kuwapo na idadi kubwa ya wanawake bungeni kunasaidia hata kufuatilia bajeti zinazohusu masuala ya wanawake na bajeti zenye mlengo wa kijinsia.

Aliongeza kuwa wanawake wanatakiwa washirikiane na wanaume ili waweze kuwaunga mkono pale wanaposimama kugombea nafasi yoyote.

Katibu Mkuu Taifa Umoja wa Wanawake Tanzania(UWT), Amina Makilagi, alisema yeyote akitaka kuwa kiongozi sifa kuu ni kujitambua.

Alisema kuwa kiongozi bora ni yule ambaye anaanza kwa kugombea nafasi za chini baada ya kushika nyadhifa mbalimbali ndiyo anagombea nafasi za juu.

"Ukianza na nafasi ya nchini ukaenda nafasi ya juu itakusaidia kuitumikia kutokana na kuwa ulianzia chini na unakuwa unaelewa mambo mbalimbali ya jamii," alisema Makilagi.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na watumishi wa Halmashauri za Mafinga Mji na Mufindi, akiwa katika ziara ya kikazi mkoani Iringa jana. **PICHA: OWM**

# Ahukumiwa kifo kwa kuua aliyemnyima supu

**Na Said Hamdani,** LINDI

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mtwara, imemhukumu kunyongwa hadi kufa Mohamedi Omari (45), iliyompata na hatia ya kumuua kwa kukusudia Andrew Ndemba, kwa madai ya kumnyima supu ya kuku.

Omari maarufu Mang'oro ni mkazi wa Kata ya Chikonji katika Manispaa ya Lindi, alihukumiwa na Jaji Mfawidhi wa Mahakama hiyo, Paul Ngwembe, baada ya ushahidi uliotolewa dhidi yake kuthibitishwa bila shaka kuwa alitenda kosa hilo.

Baada ya Jaji Ngwembe, kumtia hatiani, mshtakiwa aliulizwa kama ana neno litakaloishawishi mahakama isimpe adhabu kali kutokana na kutiwa hatiani.

Aidha, alijitetea kwa kuiomba isimpe adhabu kali akisema ni mkosaji wa mara ya kwanza, lakini pia anayo familia inayomtegemea akiwamo mke na mtoto na alifanya hivyo kutokana na kupitiwa na shetani.

Wakili wa Serikali, Emmanuel John, aliiomba mahakama impe adhabu kali ili iwe fundisho kwake mshtakiwa na watu wengine walio na moyo usio wa kibinadamu dhidi ya wenzao.

Jaji Ngwembe akitoa hukumu katika kesi hiyo namba 48/2016, alimhukumu kunyongwa hadi kufa licha ya utetezi wake.

Mwanzoni ilielezwa mahakamani hapo na wakili wa serikali, Emmanuel John, kuwa Mang'oro alifanya mauaji hayo Aprili 07 mwaka 2016 usiku, baada ya Ndemba, aliyekuwa akiitwa kwa jina la utani Mtanzania kukataa kumnunulia supu ya kuku.

Alisema siku hiyo ya tukio, Mang'oro akiwa ameongozana na mpenzi wake walifika nyumbani eneo inapouzwa supu ya kuku na kumkuta Mtanzania na rafiki yake aitwaye Barnaba wakiendelea kunywa supu hiyo.

Mfungwa huyo alimwomba amnunulie supu lakini alimjibu kuwa hana fedha.

John alisema majibu hayo yalimchukiza mshtakiwa Mang'oro, ndipo mzozo ulipoanza huku akimpa kauli za vitisho kuwa atamwonyesha.

Mtanzania alilipiga teke sufuria la supu, kisha kuondoka eneo lile akiwa na rafiki yake mwingine Issa Abdallah, kuelekea nyumbani kwao wakitumia baiskeli.

Alisema wakiwa wanaelekea nyumbani kwao, Mang'oro alichukuwa panga na kwenda kuwavizia njiani akijificha eneo ambalo walikuwa wanapita mara kwa mara na walipokaribia aliwasimamisha.

Hata hivyo walipomtambua waliongeza mwendo lakini katika kukimbia huko Ndemba au Mtanzania alidondoka.

Wakili wa serikali alisema kitendo cha Mtanzania kudondoka kulitoa nafasi kwa mshtakiwa kumshambulia kwa kumkatakata na panga maeneo mbalimbali ya mwili wake, ikiwamo kichwani na kupoteza damu nyingi na mwisho kufariki maisha yake.

Alisema mshtakiwa aliacha kumshambulia baada ya kuona watu akiwamo Issa Abdallah kufika eneo la tukio na kuanza kumkaripia.

Aliangusha panga kukimbilia nyumbani kwake, lakini usiku huo alikamatwa na polisi na taratibu za kumfikisha mbele ya sherria zilianza hadi alipohukumiwa jana.

# Watendaji, viongozi Saccos wapandishwa kizimbani

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), mkoani Lindi, imewafikisha mahakamani viongozi wawili wa chama cha kuweka na kukopa cha Walimu Saccos, kujibu mashtaka ya ubadhirifu.

Walimu Saccos iliyoko katika Manispaa ya Lindi, wanadaiwa kufanya ubadhirifu wa Sh. milioni 40, mali ya chama hicho.

Washtakiwa hao ni mtunza fedha, Nawe Makota (49) na katibu wake, Gaudensia Shada (46) waliofikishwa mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, James Karymah na kusomewa mashtaka na Mwanasheria wa Takukuru, Peter Camilius.

Akiwasomea mashtaka yanayowakabili, Camilius alidai kwamba washtakiwa hao ambao ni watumishi wa umma na viongozi wa chama hicho, walifanya ubadhirifu huo mwaka 2013.

Mwanasheria huyo wa Takukuru alidai kuwa licha ya ubadhirifu huo wa Sh. milioni 40 wanakabiliwa na kosa la pili la matumizi mabaya ya madaraka waliyokabidhiwa na wanachama wao.

Camilius aliiambia mahakama hiyo kwamba washtakiwa wote kwa pamoja wamefanya makosa na wanastahili kushtakiwa.

Wawili hao walikana makosa wanayoshtakiwa nayo na hadi Nipashe inaondoka mahakamani, walikuwa bado hawajatimiza masharti ya dhamana ikiwamo hati ya mali isiyohamishika na bondi ya Sh. milioni 20.

Kesi ya washtakiwa hao namba 16/2010 imepangwa kufikishwa tena mahakamani hapo Oktoba 8, mwaka huu.



Wadau wa kilimo wakiwa kwenye mkutano mkuu wa mtandao wa vikundi vya wakulima Tanzania (MVIWATA), uliofanyika mjini Babati mkoani Manyara juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# China kuwekeza kiwanda cha risasi

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

SERIKALI imewahakikishia wawekezaji kutoka China mazingira wezeshi kwenye uchimbaji madini ya 'grafaiti' (risasi), wakati wanapojiandaa kujenga kiwanda kwenye mji mdogo wa Mirerani, ulioko mkoani Manyara.

Pamoja na hakikisho la mazingira wezeshi, aidha imewataka kufuata sheria, kanuni na taratibu za uwekezaji.

Ofisa madini mkazi wa mkoa wa kimadini wa Simanjiro, Daudi Ntalima, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wawekezaji wa madini hayo kutoka China wanaotarajia kujenga kiwanda hicho.

Ntalima aliwahakikishia mazingira mazuri ya uwekezaji huo ila aliwaasa kufuata sheria na kanuni za uwekezaji za Tume ya Madini na sheria za nchi.

Alisema katika uwekezaji wa kiwanda cha kuchakata madini ya 'grafaiti' kwa wageni hao wa China wanachotarajia kujenga, utakuwa na manufaa kwa taifa na jamii ya Mirerani.

"Kiwanda hicho kitatoa ajira pia kwa wakazi wa Mirerani nchi itafaidika kwa kulipwa kodi na tozo nyingine," alisema Ntalima.

Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, James ole Millya, alisema Wachina hao awali walifika Msumbiji ili kuwekeza ila wakapendezwa na Tanzania.

Katibu wa chama cha wachimbaji madini mkoa wa Manyara (Marema), Tariq Kibwe, alipongeza jitihada za Ntalima kutoa ushirikiano kwa wawekezaji hao wa China.

"Wachina wameshiriki mazungumzo hayo ya uwekezaji huo na kuahidi kufuata sheria za nchi na kanuni na sheria zinazohusiana na madini ikiwamo kulipa kodi," alisema Kibwe.

Wawekezaji hao wa China waliambatana na mjiolojia Godfrey Machumu, ambaye atashiriki kwenye utafiti wa madini hayo ya grafaiti.

Madini hayo hutumika kutengeneza vitu mbalimbali ikiwamo betri za simu, za tochi na risasi inayotumika kwenye penseli.

# Shule binafsi zaililia serikali

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WADAU wa shule binafsi wameiomba serikali kuwapatia walimu wa kutosha kama wanavyofanya kwa shule za serikali ili kupunguza uhaba wa walimu katika masomo mbalimbali unaozikabili shule nyingi.

Hayo yalisemwa jana na mkurugenzi wa shule ya mchepuo wa Kiingireza ya Lady of Mercy, iliyopo Kimandolu mkoani Arusha, Helen Msuya, wakati akizungumza katika mahafali ya darasa la saba.

Alisema kuwa, shule binafsi zimekuwa zikikabiliwa na changamoto kubwa ya upungufu wa walimu bora, kwani walimu wengi wakishahitimu vyuo huchukuliwa na serikali.

"Tunaiomba serikali itusaidie na sisi shule binafsi kutupatia walimu kwani wote tunatimiza wajibu katika kuhakikisha kila mtoto anapata haki ya elimu. Hivyo hatuna budi kushirikiana katika kutatua changamoto mbalimbali zinazotukabili kwa pamoja," alisema Msuya.

Aliongeza kuwa kutokana na kukosekana utaratibu wa shule hizo kupangiwa walimu na serikali mara nyingi zimejikuta zikikabiliwa na uhaba wa walimu.

Aidha, alitaja changamoto nyingine inayowakabili kuwa ni ukosefu wa fedha za kuendesha shule hizo kwani ni gharama kuziendesha na kuiomba serikali kuwapatia ruzuku kwa ajili ya kugharamia uendeshaji ili kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili.

"Kwa kweli shule nyingi tumekuwa tukiendesha kwa mikopo, hivyo inakuwa ni changamoto kubwa sana katika kugharamia uendeshaji kutokana na wazazi wengi kusuasua ulipaji wa ada na mwisho wa siku, kujikuta tunapata hasara katika hili tunaomba sana serikali itusaidie kuweza kufikia malengo yetu," alisema Msuya.

Aliongeza kuwa, shule hiyo imekuwa ikifundisha wanafunzi katika kujiamini tangu wakiwa wadogo katika kuwaandaa kisaikolojia ili waweze kusimama wenyewe na hatimaye kujiajiri na kuondokana na changamoto ya ukosefu wa ajira.

Edgar Mosha aliyekuwa mgeni rasmi katika mahafali hayo ambaye ni Mwenyekiti wa Bodi ya Shule, aliwataka wanafunzi hao kuongeza bidii katika masomo yao na kuacha kubweteke kwani kumaliza darasa la saba si mwisho wa elimu.

## Umeme kukatika sasa kuwa historia

**Na Woinde Shizza,** ARUSHA

SHIRIKA la Umeme (Tanesco) limejipanga kuwa hadi ifikapo mwaka 2025 tatizo la ukatikaji wa umeme mara kwa mara litakuwa limeisha na wateja wao watakuwa wamesahau kero hiyo.

Hayo yalisemwa juzi jijini Arusha na Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa Tanesco, Mhandisi Raymond Seya, wakati akiongea na waandishi wa habari baada ya kufunga semina ya kuwajengea uwezo wahandisi wa matengenezo, mameneja wa shirika hilo wa mikoa na kanda.

Alisema siku za nyuma kulikuwa na tatizo la kukatika umeme mara kwa mara, lakini kwa sasa limepungua sababu ya kuboresha miundombinu katika sehemu mbalimbali na umeme haukatiki mara kwa mara kama ilivyokuwa hapo awali.

Alisema lengo la shirika ni kuboresha zaidi utoaji wa huduma na kuzitoa kwa viwango vya kimataifa ili usikatike bila sababu.

Seya alisema mkakati wa kutekeleza hayo umeanzia katika kikao hicho, ambacho wanaamini ni sehemu ya mwarubaini wa tatizo hilo.

"Dhima kamili ya semina hii ni kuhakikisha wahandisi hawa wanadhibiti suala la kukatika umeme kwa sababu umeme unavyokatika hata kwa dakika moja, ni hasara kubwa sana inayopatikana kwa serikali kwani inakosa fedha au kodi inayotokana na uzalishaji," alisema Seya.

Aliongeza: "Kwa upande wa viwanda vyetu navyo vinapata hasara kwa mfano kiwanda cha kutengeneza plastiki umeme ukikatika ghafla kama wanaendelea kuzalisha wanakuwa wameharibu bidhaa zao zilizokuwa kwenye hatua mbalimbali za uundwaji. Hii ni changamoto ambayo pia inawafukuza wawekezaji," alisema.

Aidha, alisema katika mkutano huo wamejadili na kuwapa mafunzo ya wiki mbili juu ya kumaliza tatizo la kukatika kwa umeme na wametoka na makubaliano ya kuhakikisha umeme haukatiki ovyo.

Mhandisi Seya alisema kuwa wanataka kuhakikisha kila mwananchi anapokea na kunufaika na umeme wa uhakika, lakini pia katika mkakati wa Tanzania ya viwanda hauwezi kufanyakazi kikamilifu kama umeme utakuwa si wa uhakika.

Aidha, alisema kama umeme hautakatika mara kwa mara pia Tanzania itawavutia wenye viwanda kuja kuwekeza nchini na wakija kuwekeza serikali itaongeza mapato na ajira zitaongezeka kwa wananchi.

Kwa upande wa Meneja Mwandamizi wa Usambazaji wa Tanesco, Mhandisi Mahende Mgaya, alisema Wazungu wameweza kumaliza tatizo la kukatika umeme katika nchi zao na kwa Afrika pia nchi ya Misri imeachana nalo hivyo wanaamini na Tanzania wakisimama imara wanaweza kufuata nyayo hizo.

Alisema kuwa kitu kinachosababisha matatizo ya kukatika umeme kwanza ni miti kuwa karibu na miundombinu ya umeme kwa hiyo watasafisha njia zote za umeme na kubadilisha nguzo zote ambazo zimeoza na kuweka mpya na kubadilisha viungio au vifaa vyote vya kuunganisha umeme ambavyo vimechoka na kuchakaa.

## Mradi washauri uwekezaji ujuzi

**Na Mwandishi Wetu,** SIHA

MRADI wa mkulima mbunifu unaotoa elimu ya kilimo na ufugaji nchini, umeshauri serikali na wadau wa sekta hiyo kufikiria upya kuwekeza zaidi kwenye ujuzi na ubunifu katika mnyororo wote wa thamani kama inataka kujitosheleza kwa malighafi za viwandani.

Akizungumzia umuhimu wa uwekezaji huo kwa Wilaya ya Siha, Ofisa mwandamizi wa mradi huo na Mhariri Mtendaji wa Jarida la Mkulima Mbunifu, Ayub Nnko, alisema bado wakulima wa Tanzania hawajajikita sawa sawa kwenye maeneo hayo, hali ambayo inachangia kukosa fursa za masoko ya kimataifa.

"Wakulima sasa ni vyema wakate bima ya mazao kwa ajili ya ulinzi wa athari za mabadiliko ya tabia nchi na serikali iwekeze katika tafiti ili kupata taarifa zinazoshawishi vijana kutumia fursa za kilimo.

"Pia ili kufikia lengo la kuifanya Tanzania kuwa ya uchumi wa viwanda kama ilivyo sera ya serikali kwa sasa, tunaishauri serikali kurejesha vyuo vya shamba darasa katika kila kijiji kote nchini, lakini taasisi za kifedha nazo zibanwe kuongeza mikopo kutoka asilimia 8 hadi angalau kufikia asilimia 25 kwenye sekta ya kilimo."

Pamoja na mambo mengine, Nnko ametaka sera ijayo iweke masharti ya mkulima kunufaika kwa asilimia 50 ya thamani ya mazao yake sokoni. Alisema kwa sasa yako mabadiliko ya kimtazamo katika sekta ya kilimo ambayo kama serikali itayatilia maanani, hakika ni mtaji mkubwa zaidi ya rasilimali fedha.

"Ukiachilia mbali ushauri huo tunaoutoa kwa serikali, wakulima wenyewe kwa upande wao tunawahimiza kufuatilia taarifa za masoko katika kuwekeza kwenye zao husika," alisema Nnko.

Amesisitiza kwamba kwa kuwa kilimo hakihitaji usaili, ila utayari na maandalizi ya kunufaika na fursa lukuki za mahitaji ya nchi, kuna kila sababu mwaka ujao wa fedha 2020/21, serikali ikaweka kipaumbele cha kwanza katika sekta ya kilimo kwa vile ndiyo inaajiri wananchi wengi zaidi.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Uendeshaji wa Kampuni ya Usambazaji wa pembejeo za kilimo ya Amka Feader Ltd, Goodluck Makupa, ameishukuru serikali kwa kupunguza vikwazo na tozo 54 katika mnyororo wa thamani, akidai kuwa uamuzi huo utaongeza tija katika uzalishaji wa kilimo.

# Kigwangallah kuongoza watu mashuhuri kupanda Kilimanjaro

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Hamisi Kigwangallah, kesho ataongoza makundi ya watu maarufu na viongozi mbalimbali nchini kupanda Mlima Kilimanjaro kwa siku sita kwa ajili ya kutekeleza kampeni ya Kili Challenge.

Watu maarufu akiwamo msanii wa Bongo Flava, Nassib Abdul a.k.a Diamond na meneja wa wasanii wa muziki nchini, Hamisi Shaban (Babu Tale) ni miongoni mwa waliojitokeza kuunga mkono kampeni hiyo.

Jana, Waziri Kigwangallah na baadhi ya watu waliojitokeza kuunga mkono kampeni ya Kigwangallah ya Kili Challenge 2019, walianza mazoezi mafupi ya kuzoea hali ya hewa ili kujiweka sawa kutekeleza kampeni hiyo.

Kigwangallah atawaongoza watu hao kupanda mlima huo hadi kufika kilele cha Uhuru chenye urefu wa mita 5,895 ambao ni urithi wa asili wa dunia.

Akizungumzia maandalizi hayo, Waziri huyo alisema: "Ili kuzoea hali ya hewa tumekutana na vegetation (uoto) mbili tofauti ambapo kule chini tumekutana na msitu mnene ambapo unazunguka kote katika hifadhi ya Mlima Kilimanjaro.

"Lakini tulipofika kwenye urefu wa mita 2,500 hivi uoto ukaanza kubadilika na uoto wake ni kama ule uoto unaouona Ulaya."

Kilele hicho ndicho kivutio kikubwa kwa watalii kutoka mataifa mbalimbali kutokana na kufunikwa na theluji. Katika Hifadhi ya Taifa ya Mlima Kilimanjaro, kuna njia sita za kupanda hadi kileleni na njia iliyo rahisi na iliyo maarufu zaidi ni ile ya kuanzia lango la Marangu ambako ndiyo makao makuu ya hifadhi.

Malango mengine ni Machame, Lemosho, Lendrosi, Umbwe, Rongai na Mweka.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Kapteni mstaafu George Mkuchika (kulia), akizungumza na watumishi waandamizi wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC), jijini Dar es Salaam juzi, wakati wa kikao kazi chenye lengo la kuhimiza uwajibikaji kwa watumishi wa chuo hicho. **PICHA: UTUMISHI**

# Mgogoro wa ardhi kifamilia tishio

**Na Mwandishi Wetu,** HAI

MGOGORO wa familia moja wa kugombea ardhi kati ya mama na watoto wake wawili wa kiume, umezuka katika Kijiji cha Kyuu, Wilaya ya Hai, huku ukidaiwa kuhatarisha amani.

Mama wa watoto hao ambaye ni mjane aitwaye Mariamu Awe (72) na wanawe wako katika mgogoro wa kugombea mipaka wa shamba la familia.

Habari zilizopatikana kutoka kwenye kikao cha usuluhishi kati ya serikali na familia hiyo, zinaeleza kuwa mama huyo anadai kutishiwa maisha na wanawe.

Watoto hao (majina yao yamehifadhiwa), wanaishi katika Kitongoji cha Maiputa, wilayani Hai. Pamoja na mambo mengine, inadaiwa kuwa watoto hao wanamlazimisha mama yao kuwagawia kiasi cha Sh.700,000 ambazo ni fedha iliyotolewa kama mahari kwa dada yao.

Akizungumza katika kikao hicho cha usuluhishi, mjane huyo alisema watoto wake wamekuwa wakimtishia maisha na hivyo kujikuta akiishi kwa wasiwasi.

Alisema chanzo cha ugomvi ni kugombea mpaka ya shamba na kwamba mume wake kabla ya kufariki dunia, alimwonyesha mipaka ya wanawe, lakini mmoja wao ameamua kuvuka mipaka na kujiongezea kinyemela.

"Mume wangu alifariki mwaka 2015 na alimwonyesha huyo kijana wangu mkubwa sehemu yake ya kujenga ikiwamo mipaka ya eneo hilo, lakini ameacha sehemu yake na kusogeza na nilipomuuliza ndiyo ukazuka ugomvi.

"Huyo mwingine yeye tunaishi nae hapo nyumbani, lakini amekuwa akiungana na kaka yake, hivyo kunitukana na kuniambia niende kwetu, lasivyo watanichoma na kisu. Sasa naomba serikali inisaidie mimi ni mjane nilitegemea watoto hao lakini imekuwa sivyo," alisema mjane huyo. Hata hivyo viongozi wa eneo hilo wakiambatana na Ofisa Tarafa wa Masama, Mashariki, Nsajigwa Ndagile, walipofika eneo lenye mgogoro alijitokeza Mwenyekiti mstaafu wa kijiji hicho, Benson Ndosi, na kusema mpaka halali ni wa huyo mama na kijana wake ndiyo anavuruga mpaka.

Kwa upande wake, Ndagile ambaye alikuwa katika kikao hicho ambacho kilishindikana kumalizika, alimtaka mwenyekiti huyo kusaidia kufikisha jambo hilo katika vyombo vya sheria ili jambo hili liweze kupatiwa ufumbuzi

Mkuu wa Polisi Wilaya ya Hai, (OCD) Lwe lwe Mpina, alipoulizwa kama kuna malalamiko kuhusu jambo hilo yameripotiwa, alisema hana taarifa ya jambo hilo, lakini alimtaka mwenyekiti wa kijiji hicho kumpeleka katika kituo hicho mama huyo mjane.



Ukurasa 19

Nguvu ya soko la mafuta ghafi uchumi duniani imefika ukomo



Ukurasa 18

Vita Chunya ya kuwapata watoto 4200 waliokwepa shule wakiajiriwa



Ukurasa 15

## Mgomo wa marubani wamtia hasara mwajiri


# BUFE

Ijumaa Septemba 27, 2019

Nipashe

BIASHARA, UC... FEDHA




# Takukuru haishikiki Barani Afrika, 'shamba darasa' la udhibiti uchumi

**Na Mary Geofrey**

TANZANIA imetajwa ni nchi pekee yenye Mahakama Kuu Kitengo cha Kushughulika na Kesi za rushwa, kati ya nchi 49 wanachama wa Umoja wa Afrika ya Ushauri wa Masuala yanayohusu Rushwa (AUABC).

Mwenyekiti wa Bodi ya AUABC, Begoto Miarom, anatoa tathmini ya awali katika mkutano wa wajumbe watano wa bodi hiyo kutoka nchi mbalimbali waliofika nchini kutathmini kupambana na rushwa.

Mkutano huo uliwakutanisha na wadau wa sekta binafsi kwa lengo la kufanya tathmini ya mkataba wa kupambana na rushwa unavyotekelezwa nchini.

INAENDELEA UK.16

UCHUMI

## Habari katika picha



Ukurasa 17

Nguvu ya soko la mafuta ghafi uchumi duniani imefika ukomo Ukurasa 20

UCHUMI

DK. DOROTHY GWAJIMA

# Mzito Tamisemi ‘aliyetapikia ny watendaji wake walioinyanyap

- Kwa hatua awapa somo kwanini ipo • Aiingiza halmashauri darasa
- Awadadavulia mtaji wao ‘kutumbuliwa’



Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa (Tamisemi), Dk. Dorothy Gwajima (aliyezungushiwa duara), alkifurahia jambo na kinamama wa wilayani

**Na Elizabeth Zaya**

UNAPOZUNGUMZIA Mfuko wa Maendeleo ya Jamii(Tasaf), moja kwa moja unagusa hisia za Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Serikali za Mitaa na Tawala za Mikoa (Tamisemi), Dk. Dorothy Gwajima. Huyo hafichi kutofaurtahishwa na watumishi wa umma wanaounyanyapaa mfuko huo.

Inakuwaje mpaka anafikia hisia hizo? Ni pale alipogundua katika ziara yaie maalum mkoani Pwani, siku chache zilizopita, akibaini kasumba ya baadhi ya watumishi wa ngazi tofauti za halmashauri kunakotekelezwa miradi, wanauyanyapaa, kana kwamba hawahusiki nayo.

“Walengwa wa Tasaf ni wa serikali na huo mpango ni wa serikali na lengo la Rais John Magufuli ni kuwainua wanyonge, pia kufikia malengo ya Tanzania ya Uchumi wa Kati na ya Viwanda. Kushindwa kuwasaidia wananchi hao unakuwa unarudisha nyuma mipango ya nchi,” anasema Dk. Dorothy.

Anasema katika maeneo mbalimbalia alikotembelea kuangalia miradi, bado kuna tatizo la watumishi na wataalam katika nyanja tofauti kujiona hawahusiki na mpango huo wa Tasaf.

> **“Lengo ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema na wanaendelea kuendesha shughuli za kiuchumi.**

Dk. Dorothy anaelimisha majukumu ya utumishi wa umma si kukaa tu ofisini pekee, bali ni pamoja na kwenda maeneo wanakoishi wananchi kuwatembelea, kusikiliza na kutatua changamoto zinazowakabili.

“Tuna wataalamo wa mifugo, kilimo na maofisa ustawi wa jamii katika kila halmashauri. Hawa ndiyo wangefanya kazi ya kuwatembelea hawa walengwa, kuwasikiliza, kuwapatia elimu ya ufugaji ili wafahamu namna bora ua ufugaji au namna bora ya kuendesha kilimo chao,” anasema.

Naibu Katibu Mkuu anaendeleza masikitko yake akifafanua: “Wakisikia kwamba ni walengwa wa Tasaf, wanaona kwamba hawahusiki nao.”

“Tasaf ni taasisi kubwa na siyo ya mtu mmoja, hivyo kunahitajika ushirikiano katika kuwahudumia walengwa waliopo katika Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini na kuwasaidia katika shughuli na mi-



# yongo’ baa

## a la uongozi



Kibiti. **PICHA ZOTE: ELIZABETH ZAYA**



radi mbalimbali wanayofanya,” anasema.

**ALICHOKIONA**

Dk. Dorothy anaeleza kiu yake alipotembelea na kukagua, kutathmini na kuangalia changamoto za Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini unaosimamiwa na Tasaf, akieleza dhana haishii kuwauga mkono, bali hata kuwatembelea walengwa.

“Lengo la mpango wa Tasaf si kuwatajirisha Watanzania masikini, lakini angalau kuwashika mkono kuwaondoa katika hali ngumu zaidi wanayokuwa nayo.

“Nimetembea nimeona umesaidia sana, kwa sababu kupitia hicho kidogo wanachopewa walengwa, wameanzisha miradi midogo midogo kwa ajili ya kujiongezea,”anasema.

“Nimewatembelea na nikaona kwa macho yangu wanafuga, wanalima na wengine ambao walikuwa wanaishi kwenye nyumba mbovu, wameboresha nyumba zao, wanaishi na kulala katika mazingira mazuri.

“Ukiwatembelea wakianza kukuelezea, kuna baadhi wanajitahidi anafuga, lakini kuku wanapofikia katika hatua nzuri ambayo anaweza akauza, wanapatwa na ugonjwa wanakufa. Kwa hiyo wanarudi nyuma tena.

“Masikitiko yangu ni kwamba kwa nini wanafiwa na mifugo wakati tunao wataalamu ambao wamekaa tu maofisini?” anahoji Naibu Katibu Mkuu, anayetamka hayo kutokana na ushuhuda toka kwa walengwa, baada ya kusikiliza shida na mafanikio yao.

“Tuna wataalamu wa mifugo, kilimo na maafisa ustawi wa jamii katika kila halmashauri. Hawa ndiyo wangefanya kazi ya kuwatembelea hawa walengwa kuwasikiliza, kuwapatia elimu ya ufugaji ili wafahamu namna bora ya ufugaji au namna ya kuendesha kilimo chao. Lakini wakisikia ni walengwa wa Tasaf, wanaona hawahusiki nao

Anakumubsha nafasi ya Tasaf kuwa taasisi kubwa, hivyo kunahitajika ushirikiano kuwahudumia walengwa. Anawaagiza viongozi wa maeneo yote panakotekelezwa mradi na hasa wataalamu wa fani kama kilimo, ufugaji na afya, kuhakikisha wanaenda vijijini waliko walengwa kuwapatia elimu wanazohitaji.

“Lengo letu ni kutaka watoke katika hali ya umasikini. Kwa nini tusishirikiane kuwashika mkono? anahoji na kuendelea: “Twende tukawape elimu ya mifugo yao isife, tuwape elimu ya kilimo, tusiwaachie Tasaf makao makuu peke yao, kila mtu ajipangie ratiba ya kuwasaidia,”

**DARASA LA UONGOZI**

Ni ushuhuda wenye ukakasi dhidi ya Tasaf, uliomfanya Dk. Naibu Katibu Mkuu kufikisha mbali mtazamo wake arudi darasani kupekua makabrasha yake ya kisomi kuwafunda vakiwafunda watendaji wa serikali.

Akiwa mkoani Pwani katika Halmashauri ya Wilaya Kibiti, anawaambia wasisubiri kusukumwa, bali watawaliwe na utashi kwamba “bila ya kuwahudumia wananchi wake anapungukiwa na hajakamilika kuwa kiongozi.”

“Ni jambo la kushangaza sana, eti wewe ni kiongozi katika halmashauri, uwe mkurugenzi au mtaalamu, halafu katika eneo lako una wananchi wenye uhitaji unasaidiwa asilimia karibu 90, halafu wewe badala ya kufurahia na wewe mwenyewe kuongeza jitihada zako kusaidia panapobaki, eti napo unashindwa.

“Hivi mtu kama wewe tunakufanyaje? Watu kama hawa ndiyo wanamrudisha nyuma kuwa Rais (Dk., Magufuli), anajitahidi a kukimbia kuwaletea Watanzania maendeleo, lakini kuna baadhi ya watu wanaomvuta kwa nyuma.

“Hawa ndiyo wale ambao kutokana na uzembe wao kama malengo yalitakiwa kutimia mwaka huu, wanasababisha yanasonga mbele zaidi. Ifike mahali tuache kufanya kazi kwa mazoea, maana kiongozi wetu ametuonyesha njia tayari,” anasisitiza Dk. Dorothy

**ALIPOTUA MSOGA**

Mbali na Tasaf, Dk.Dorothy alitembelea miradi mingine ya serikali mkoani Pwani, ikiwamo ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Kibiti na Hospitali ya Msoga, iliyoko Chalinze inayoendekea kuimarishwa kuwa na hadhi ya wilaya, akifafanua kwamba serikali imedhamiria kuhakikisha inaboresha hospitali zote 67 za wilaya, kupunguza adha ya wananchi.

Anasema lengo ni kuhakikisha wananchi wanakuwa na afya njema na wanaendelea kuendesha shughuli za kiuchumi.

Kuhusu Hospitali ya Msoga, Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, anaipongeza serikali kujenga hospitali hiyo itakayowasaida wakazi wanaozunguka maeneo hayo, pia watumiaji barabara kuu ipitayo jiran, hasa katika matukio ya ajali.

“Tunafahamu kwamba hii ndiyo itakuwa hospitali kubwa karibu na barabara. Kwa maana hiyo, si kwamba itahudumia wakazi wa msoga na maeneo yanayoizunguka, pia wanaotumia barabara kubwa, maana ‘juzi juzi’ ilitokea ajali na majeruhi walileta na kutibiwa hapa. Kwa hiyo tunaamini ni msaada mkubwa,”anasema Ridhiwani.

***Mwandishi wa makala hii alikuwa katika ziara ya Naibu Katibu Mkuu - Tamisemi, mkoani Pwani.***

# Mgomo wa marubani wamtia hasara mwajiri



Ndege ya Shirika la Ndege Uingereza.



Rubani wa shirika hilo. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**Mwandishi Wetu**

SHIRIKA la Ndege la Uingereza (British Airways), limesema halitarajii kufikia malengo yake ya kibiashara katika mwaka uliopo wa fedha, kwa sababu ya mgomo wa marubani wake.

Marubani hao waligoma kwa madai ya masilahi mbalimbali wakimsukuma mwajiri wao kupitia chama chao cha marubani ndani ya shirika.

Ni mgomo uliochukua siku mbili na kuligharimu shirika Paundi milioni 121. Sasa kukwepa janga hilo, tena wanaendesha mazungumzo na chama cha marubani

Mgomo uliotokea Septemba 10 mwaka huu ukihusisha marubani tisa na mwingine ulipangwa kufanyika leo, lakini umeahirishwa.

Ikifafanua namna walivyopata hasara, shirika limesema ni kupitia abiria kushindwa kuomba nafasi ya safari mapema, hali inayopoteza wateja wake.

Hiyo inaenda mbali kwa kampuni kuathirika kupitia hisa zake kushuka thamani, kwa wastani wa asilimia 3.7

Chama cha Marubani wa Uingereza (Balpa), kimesema hadi wanachama wake kufikia katika mgomo ni hatua ya mwisho baada ya mazungumzo ya kina na kero kutoka kwa menejimenti ya shirika.

Marubani hao waliomba nyongeza ya mishahara na wakapatiwa ongezeko la asilimia 11.5 walioahidiwa na Shirika la Ndege la Uingereza ndani ya miezi mitatu, lakini wamekataa.

Hata hivyo, mwajiri aliwajibu kwamba kwa sasa ilikuwa katika wakati mgumu wa kifedha. Haya hivyo kuna mabadiliko walau ya ‘kupumua’ katika biashara na faida wastani wa asilimia tisa.

Mtendaji Mkuu wa Chama cha Marubani Uingereza Willie Walsh, anasema huenda watachukua hatua zaidi.

UCHUMI

# Takukuru haishikiki barani Afrika, 'shamba darasa' la udhibiti uchumi

• Watathmini:Mahakama Rushwa mfano • Foleni ya nchi 49 inasimama ya kwanza • Brig. Mbung'o aanika safari ya 'taa kijani'

INATOKA UK.13

Anasema katika mahojiano na asasi za umma na vyombo mbalimbali vinavyotekeleza mradi huo, walibaini mkataba huo unatekelezwa vizuri nchini hasa suala la kuwa na Mahakama ya Rushwa, ambayo hazipo katika nchi nyinginezo.

"Tumekuja Tanzania kwa ajili ya kufanya tathmini ya jinsi nchi hii inavyotekeleza mkataba wa Umoja wa Afrika (AU) wa kuzuia na kupambana na rushwa.

"Katika tathimini ya awamu, yapo mambo tumeyabaini yanayofanywa na nchi katika kupambana na rushwa na mazuri tuliyoyaona tutayatolea mapendekezo yatumike katika nchi nyingine, kwa sababu kila nchi ina mifumo na taratibu zake za kutekeleza mkataba huu," Miarom anasema.

Miarom anasema, kabla ya kuja nchini walipokea ripoti za nchi wanachama na walizipitia na wanatembelea kila nchi kufanyia tathimini ripoti watakayoiwasilisha katika bodi hiyo.

Anasema kuhusu tathimini waliyofanya, wataenda kufanyia kazi na kutoa ripoti itawayowasilishwa Tume ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambna na Rushwa (Takukuru).



Jengo la makao makuu ya Takukuru. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

### TANZANIA INAFANYA NINI?

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Brigedia Jenerali, John Mbung'o akifungua mkutano huo anasema ni mara ya kwanza kufanyiwa tathimini ya utekelezaji wa mkataba huo.

Anasema katika tathimini waliyoanza kuifanyia kazi nchini Septemba 9 mwaka huu, inaonyesha Tanzania imepiga hatua kubwa katika utekelezaji mkataba huo wa kupambana na rushwa.

Brigedia Mbung'o anasema nchi imekuwa ikitumia njia mbalimbali kushirikisha jamii katika mapambano hayo dhidi ya rushwa na kuifanya ipige hatua kufanikiwa zaidi.

Kaimu Mkurugenzi huyo anasema, Tanzania ilitia saini mkataba huo Julai mwaka 2003 na Takukuru kwa upande wa Tanzania Bara na Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (Zaeca) na kutekelezwa na baadhi ya taasisi.

Anasema baadhi ya taasisi zinazotekeleza mpango huo ni Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mitaa (NAO), Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na Jeshi la Polisi, vyombo vya habari, mashirika yasiyo ya kiserikali.

Mengine ni Idara ya Mahakama, Msajili wa Vyama vya Siasa na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC),

> **"Kumekuwa na ongezeko la idadi ya Watanzania wanaoamini kuwa serikali inafanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa, kutoka idadi ya asilimia 37 mwaka 2015 hadi asilimia 71 mwaka 2019.**


Rais Dk. John Magufuli, alipotembelea makao makuu ya Takukuru na kutaarifiwa shughuli zao.

Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Taifa ya Huduma ya Mashitaka na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki.

Anasema kupitia mkataba huo, kila nchi mwanachama ikiwamo Tanzania, inawajibika kutekeleza malengo makuu matano yaliyoainishwa na kufanyiwa tathimini ya namna wanavyotekeleza.

Brigeda Mbung'o anataja malengo wanayotekeleza, ni kukuza na kuimarisha mifumo ya uzuiaji, uchunguzi, utoaji adhabu, pamoja na kutokomeza rushwa katika nchi wananchama.

Pia, anataja malengo mengine ni kukuza ushirikiano kati ya nchi wanachama, ili kuhakikisha mifumo ya ushughulikiaji kero ya rushwa inatekelezeka.

Kwa mujibu wa Kaimu Mkurugenzi huyo, pia wanaratibu sera na mifumo ya kisheria ya kuzuia na kupambana na rushwa, kati ya nchi wananchama na kukuza maendeleo ya jamii kiuchumi. kwa kuondoa vikwazo katika shughuli za kiuchumi, kijamii, kiutamaduni, zikiwamo za kisiasa.

Lingine lililoainishwa ni kuweka miundombinu ya kukuza uwazi na uwajibikaji katika kisimamia shughuli za umma na jukumu la kufanya tathimini na ufuatiliaji kwa mujibu wa mkataba huo kwa nchi wanachama ni la bodi.

"Ikumbukwe Tanzania ni mwenyeji wa ofisi za Makao Makuu ya Bodi hii muhimu ya kuzuia na kupambana na rushwa barani Afrika. Ofisi zake zipo jijini Arusha," anasema Brigedia Jenerali Mbung'o.

Anataja la nne katika mkataba huo, inazitaka nchi wanachama kuharamisha matendo mbalimbali ya rushwa katika sheria zao, kama vile kutoa na kupokea rushwa, limbikizo la mali, utakatishaji fedha haramu, matumizi mabaya ya mamlaka na kuchepusha fedha au mali za umma.

"Hata hivyo nina furaha kuujulisha umma kwamba, Tanzania imefanikiwa kwa kiwango kikubwa kutekeleza matakwa yaliyoainishwa katika ibara zote za mkataba huo," anasema Mbungo.

Yaliyotekelezwa

Katika kupambana na vitendo hivyo, Brigedia Mbung'o anasema serikali imetunga sheria za kuharamisha matendo hayo, ikiwamo ya Kuzuia na Kupambana Mwaka 2007.

Pia, kuna sheria ya kuwalinda watoa taarifa na mashahidi wa makosa ya jina ya mwaka 2015; Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Mwaka 2011, iliyorekebishwa 2016 na Sheria ya Uhujumu Uchumi ya Zanzibar, mwaka 2004.

Anasema Sheria ya Gharama ya Uchaguzi ya 2010; Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015; na Sheria ya Upatikanaji wa Taarifa, 2015.

Brigedia Jenerali Mbung'o. anasema sasa wanaweka ushirikishwaji wadau wa sekta binafsi katika mapambano hayo na wameanzisha Mahakama ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi.

"Katika hatua ya kufanya tathimini hii, wajumbe wa bodi wamekutana na watumishi wa Takukuru na kukutana na wadau kutoka serikalini na katika sekta za umma zinazotekeleza mkataba huu," anasema.

### TATHMINI ILIVYO

Mnamo Septemba 9 mwaka huu, ujumbe huo ulianza kufanya tathimini kwa kukutana na wadau mbalimbali, ikianza na Jaji Mkuu na Katibu Mkuu Ikulu, anayesimamia Utawala Bora na Maboresho.

Brigedia Jenerali Mbung'o, anasema walishakutana na Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi na wadau, wanaotekeleza mkataba huo upande wa Zanzibar na asasi za kiraia.

"Hii yote ni katika kujiridhisha kutoka katika sekta zote juu ya hali ya utekelezaji wa mkataba huu kwa nchi ya Tanzania," anasema Brigedia Jenerali Mbung'o.

Anasema, hivi sasa taifa limesifika kwa namna linavyopambana na rushwa na tathimini nyingi za kitaifa na kimataifa zilizofanyika kupima hali ya ruhswa, akiamini majibu ya tathimini iliyofanywa na AUABC itakuwa na matokeo chanya.

"Rai yangu kwa kila mdau wa mapambano dhidi ya rushwa kuendeleza mapambano katika eneo lake la mamlaka, kwa lengo la kuhakikisha inaondokana na rushwa na kuwa na uchumi imara wenye kuwaletea wananchi wake maendeleo," anasema Brigedia Jenerali Mbung'o.

### MJUMBE TAKUKURU

Mjumbe na Mkurugenzi wa Uzuiaji Rushwa Takukuru, Sabina Seja, anasema asasi za kiraia zina jukumu kubwa katika kupambana na rushwa, hasa ikizingatiwa zina njia nyingi ya kufikia jamii.

Anasema rushwa ya ngono ni miongoni mwa ajenda ambazo wanapokea mapendekezo yake wanapokutana na wadau mbalimbali, wakati wa kufanya tathmini na wanayafanyia kazi.

Sabina anafafanua kwamba, wanategemea zaidi wadau kutoa maoni yao katika kuifikia jamii katika kupambana na rushwa katika nchi hizo na kufikia malengo tajwa.

Aidha wadau wa sekta binafsi walioshiriki mkutano huo, walipendekeza kuwapo uwekezaji wa kutosha kwa vijana na makundi mbalimbali yanayptekeleza mpango huo wa kupambana na rushwa.

### TAIFA LILISHANG'AA

Takukuru iko katika rekodi ya kuwahi kutajwa ya kwanza kati ya nchi 35 za Afrika, katika kipengele cha juhudi za serikali katika mapambano dhidi ya rushwa, mwaka huu.

Aliyekuwa Mkurugenzi Mkuu wa Takukuru, Diwani Athumani, anasema mafanikio hayo yaliainishwa katika taarifa ya utafiti wa kupima hali ya rushwa iliyotolewa Julai 11 mwaka huu na taasisi za kimataifa zinazofanya tafiti, zilizoainisha Tanzania imefanya vizuri katika maeneo mawili.

Anataja maeneo hayo ni utendaji mzuri wa viongozi wa serikali ya sasa na kukuza imani ya wananchi kwa serikali yao, kutokana na jitihada za kuzuia na kupambana na rushwa kitaifa.

"Kumekuwa na ongezeko la idadi ya Watanzania wanaoamini kuwa serikali inafanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa, kutoka idadi ya asilimia 37 mwaka 2015 hadi asilimia 71 mwaka 2019," Athumani anasema.

Pia, utafiti unaonyesha idadi ya wananchi wanaofikiri kuwa rushwa imeongezeka nchini ni ndogo kwa asilimia 10 ikilinganishwa na idadi ya asilimia 66 iliyoona hivyo mwaka 2015.

Anasema, utafiti umeonyesha idadi kubwa ya Watanzania wanaiamini serikali yao katika mapambano dhidi ya rushwa na wanaona vitendo vimepungua.

Takwimu zinaonyesha, imani imeongezeka kutoka asilimia 13 mwaka 2015 hadi kufikia asilimia 72 kwa mwaka 2019.

# Biashara katika picha



Mkurungenzi Mkuu wa Mauzo wa Kampuni ya Bomet, Martin Hu, akimtangaza Msanii nyota wa Bongo Fleva, Nasibu Abdul maarufu kama Diamond, kuwa Balozi wa bidhaa mpya ya sabuni aina ya Nice One, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**


Mkazi wa Jiji la Dar es Salaam, akiendesha baiskeli iliyosheheni trei za mayai wakati akisaka wateja katika eneo la Sinza Mapambano, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: SABATO KASIKA**


Wachuuzi wa chumvi na sabuni wakilazimika kukaa chini ya mitaro, baada ya kupanga biashara zao pembeni ya barabara katika eneo la Mbezi Mwisho, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. **PICHA: MIRAJI MSALA**

UCHUMI

# Vita ya kuwapata watoto 4200 waliokwepa shule wakiajiriwa

## • Mzizi mashamba tumbaku, migodini • Timu ya DC, NGO, wanunua mazao



Wanafunzi wa shule mbalimbali za msingi kutoka kata za Lupa Tingatinga, Mtande na Mtanila wilayani Chunya katika Mkoa wa Mbeya, wakiandamana huku wamebeba mabango yenye ujumbe mbalimbali wakati wa maadhimisho ya Siku ya Kupinga Utumikishwaji wa Watoto. **PICHA: NEBART MSOKWA**

**Na Nebart Msokwa,** aliyekuwa Chunya

TANZANIA ni taifa mwanachama iliyoridhia Mkataba wa Kimataifa wa Umoja wa Mataifa unaopinga utumikishwaji wa watoto.

Pia nchini kuna baadhi ya sheria zinazopinga utumikishwaji watoto, ikiwamo Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini ya mwaka 2004 na Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009, inayoainisha baadhi ya ajira hatarishi ni pamoja na migodini, shambani na za uvuvi na Sheria ya Elimu.

Sheria zingine zinazopinga utumikishwaji wa watoto nchini ni pamoja na sheria ya elimu inayotafsiri kuwa ajira kwa watoto zinawanyima haki ya kusoma shule na sheria ya kazi na mahusiano kazini ambayo ina kipengele kinachopinga utumikishwaji wa watoto.

Ikirejewa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, inatajwa kati ya maeneo yenye kiwango kikubwa cha utumikishwaji watoto na kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la Winrock International, kwa kushirikiana na serikali, kuna zaidi ya watoto 4200 wanaotumikishwa wakiwa kwenye mazingira magumu.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya hiyo, Theresia Mwendapole anasema watoto wanatumikishwa zaidi ni kwenye sekta kuu mbili, ambazo ni kilimo na uchimbaji madini ya dhahabu, ndio shughuli kuu za kiuchumi.

Anasema kupitia utafiti waliofanya, walibaini watoto wanaotumikishwa migodini wapo 632 na waliobaki wanaishi kwenye mazingira magumu na kutumikishwa kwenye shughuli za kilimo.

> **“Kupitia utafiti waliofanya, walibaini watoto wanaotumikishwa migodini wapo 632 na waliobaki wanaishi kwenye mazingira magumu na kutumikishwa kwenye shughuli za kilimo.**

“Watoto wanaotumikishwa kwenye shughuli mbalimbali za uzalishaji mali wapo kwenye kundi la watoto 4,239 wanaoishi kwenye mazingira magumu, lakini sekta zinazoajiri zaidi watoto ni kilimo na uchimbaji wa madini,” anasema, huku akidokeza kuwapo hatua zinazoendelea kuwaondoa watoto hao.

### CHANZO NINI?

Baadhi ya wazazi wanadai kuwa chanzo cha utumikishwaji watoto wilayani humo kukosa elimu ya haki za watoto pamoja na umaskini wa kipato, kwa ngazi ya familia.

Mmoja wa wazazi, Mtindo Mustafa, mkazi wa Lupa Tingatinga, anasema baadhi ya wazazi hawaoni umuhimu wa watoto kwenda shuleni na hivyo wanawatumia kwenye shughuli za uzalishaji mali.

Anashauri, ili kuondokana na hali hiyo, kinachohitajika zaidi ni elimu kwa jamii kuhusu haki za watoto zilizoainishwa kisheria, kuwekwa katika vitendo ili watambue wanachokifanya ni kukiuka sheria.

Shirika lisilo la kiserikali la Winrock International, hivi sasa limeanzisha mradi maalumu wa kuwaondoa watoto wanaotumikishwa kwenye mashamba ya tumbaku unaojulikana kwa jina la Prosper Umoja na ukitarajiwa kuwa muarobaini wa kukomesha utumikishwaji huo.

Meneja wa Mradi, Christopher Luyenga, anasema utakuwa wa miaka miwili na unatekelezwa katika mikoa mitatu inayozalisha tumbaku, ambayo ni Tabora, Mbeya na Songwe. Ulianza kutekelezwa nchini mwaka 2018 na utafikia tamati 2020.

Anasema mradi unatarajiwa kuwafikia zaidi ya watoto 600 katika mikoa hiyo na kuwaondoa kwenye maeneo walikoajiriwa, kuwarejesha shuleni na kutoa vifaa vyote vya masomo, kwa wanaotoka katika mazingira magumu.

Luyenga anasema, mradi wilayani Chunya, unatekelezwa kwenye kata tatu za Mtanila, Mtande na Lupa, ambako ndiko kilimo cha tumbaku kinafanyika zaidi.

Anasema, mbali na kuwapatia vifaa watoto wanaoishi kwenye mazingira magumu, pia mradi unalenga kufuatilia mahudhurio ya watoto hao shuleni kujiridhisha hali ya utumikishwaji kama inakoma au la.

“Tumetoa mafunzo kwa walimu sita kutoka kwenye hizi kata, namna bora ya kuhamasisha mahudhurio ya wanafunzi shuleni, ili kuhakikisha wanapenda shule kuliko kwenda kwenye shughuli za kujitafutia kipato ambako ndiko wanatumikishwa,” anasema Luyenga.

Vilevile, mradi umezijengea uwezo kamati za ulinzi na usalama wa mama na mtoto katika vijiji vinavyohusika na mradi pamoja na kutoa mafunzo ya ujasiriamali na vikoba kwa wanawake 180, ili kuwainua kiuchumi na kuepuka kuwatumikisha watoto wao.

Meneja huyo anasema, ili kuhakikisha mradi unafanikiwa, wanatekeleza kwa kushirikiana na kampuni tatu za ununuzi wa tumbaku zilizoko kwenye maeneo hatarishi kwa mtoto.

### SIKU YA MTOTO

Juni 12 Mwaka huu, wananchi wa Wilaya ya Chunya waliungana na taasisi mbalimbali kuadhimisha siku ya kupinga utumikishwaji wa watoto duniani ambayo, yaliandaliwa na Shirika la Winrock International na kufanyika katika Kata ya Lupa Tingatinga.

Ni maadhimisho hayo yaliyopambwa na maandamano ya zaidi ya wanafunzi 2,000 kutoka shule mbalimbali za msingi kutoka kata za Lupa Tingatinga, Mtande na Mtanila, waliobeba mabango yenye ujumbe mbalimbali kupinga utumikishwaji wa watoto.

Baadhi zilisomeka: Kupata elimu ni haki yangu; Mtoto ni Msingi wa taifa Endelevu, tumtunze na tumuendeleze; Watoto tunahitaji mazingira bora ya kujifunzia; Hatua kali zichukuliwe kwa wanaowatumikisha watoto; na Lazima hatua zichukuliwe kukomesha utumikishwaji watoto.

Pia, kuna mabango ya tukio hilo yalionyesha hali ya utumikishwaji watoto na takwimu mbalimbali kama vile: Sekta ya Kilimo imeajiri watoto milioni 108; watoto milioni 73 wanafanyishwa kazi hatarishi; watoto milioni 75 wanafanyishwa kazi bila malipo; na watoto milioni 152 duniani kote wanatumikishwa.

Mbali na mabango ya wanafunzi, pia maadhimisho hayo yalipambwa na kwaya ya vijana wa Kata ya Lupa, walioimba nyimbo za kupinga utumikishwaji wa watoto huku zikihamasisha kuwalinda.

Baadhi ya nyimbo zilizoimbwa na kwaya hiyo zilibeba kuwa na ujumbe kama: Tunaiomba serikali iwachukulie hatua kali wanaowatumikisha watoto kwenye shughuli za tumbaku; Wazazi na walezi tuwapende watoto wetu na tuwawezeshe kutimiza ndoto zao; na tuwapatie kwanza watoto wetu elimu bora’.

### MKUU WILAYA

Mkuu wa Wilaya Chunya, Maryprisca Mahundi, analipongeza shirika la Winrock International, kwa mapambano ya kupinga utumikishwaji wa watoto na kuwaelekeza wanaoajiri watoto kwenye shughuli hizo, kuacha mara moja, akiwaambia mkono wa sheria umeandaliwa dhidi yao, kwami unathiri afya na mfumo wa elimu kwa watoto.

Maryprisca, aliwataka wakazi wa wilaya hiyo kuwa na shughuli mbadala za kuwaingizia kipato, ili kuondokana na umasikini unaopelekea watoto wao kwenye shughuli hatarishi.

BIASHARA

# Apaishwa na Sido darasa, mkopo laki tano kuanzia

**Na Renatha Msungu,** Dodoma



Mkurugenzi wa Unique & Superior Bakery, Sella Mkisi akikagua mikate iliyokuwa tayari. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

UNAPOULIZA ni nini hasa? Anajibu kwamba hiki ndicho kimemfanya kupiga hatua moja kwenda nyingine. Huyo ni mjasiriamali Sella Mkisi, Mkurugenzi wa asasi ya Unique & Superior Bakery ya jijini hapa, inayojishuhusisha na kutengeneza vitafunwa na kusambaza katika maeneo ya ndani na nje ya jiji la Dodoma.

Katika sura moja ni kama hadithi, lakini ukweli unabaki kutoka ushuhuda wa matendo ya mjasiriamali Sella, anasema mafanikio yake yametokana na juhudi za Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (Sido), ikichangia kwa kiasi kikubwa kumtoa hatua moja kwenda nyingine, kiuchumi.

Amefanyaje mpaka kufikia hatua hilo? Ni baada ya kupeleka wazo lake kutaka kujifunza kutengeneza bidhaa kadhaa kama mikate na maandazi, akitumia fursa ya uwekezaji katika maeneo mbalimbali ambayo mkoa umeyaainisha.

Ni maeneo ambayo wajasiriamali wanayoyaona kila penye furasa za kimasoko wanazoweza kuzimudu, ndizo wanaweza kuingia kwenye ushindani wake kimataifa, kadri siku zinavyosonga mbele, kujitokeza kuwekeza.

Anasema, wazo la kutengeneza vitafunwa; mikate, maandazi na keki, ghafla lilionekana lulu, baada ya kuongeza ujuzi kutoka Sido, walikompatia mafunzo na akakopeshwa fedha Sh.500,000 zikiwa ni mtaji wa kutengeneza bidhaa hizo alizoongezewa ujuzi na akawa anaziuza katika sehemu mbalimbali, ndani na nje ya Dodoma.

Sella anaiambia Nipashe kwamba, jambo kubwa katika kufanikisha dhamira inaanzia uthubutu na hutoa zao kila mafanikio katika mazingira ya ujasiriamali na biashara, akiweka angalizo ni muhimu kutambua hasa anachotaka kukifanya katika uwekezaji wake.

### UZOEFU WAKE

Sella anasema, alianza kazi hiyo akiwa na mtaji wa Sh. 500,000 tu, lakini ndoto ilimuongoza kufikia kilele cha kuwa mjasiriamali mkubwa katika bidhaa ya mikate na maandazi anayofanya, hivi sasa anajinasibu inapendwa na wateja wengi wa kila siku.

"Ni vigumu kuamini hiki ninachosema, lakini ni ukweli nashauri vijana wenzangu kuwa na uthubutu wa kile wanachofikiria kufanya wafanye wasisite," anasema Sella.

Hivi sasa Sella ametoa mtazamo kwa wengi katika jamii katika namna taifa linaelekea uchumi wa kati wa viwanda, ni wajibu vijana wengi kuweka uthubutu kama wa Sella, katika kujitosa kwenye ujasiriamali wanaofikiria kutumia fursa zinazotangazwa katika maeneo kama jiji la Dodoma, badala ya kubweteka na ndoto ya kusubiri ajira.

> **"Alipoanza na mtaji mdogo wa mkopo hakukata tamaa na badala yake, alikaa chini kuona anachotakiwa kukifanya, kulingana na pesa aliyokopeshwa na mwezeshaji wake Sido.**

Katika hilo, Sella anapanua wigo wa fikra kwamba, wanaoingia katika ujasiriamali wajielekeze katika kusaka mikopo inayotolewa na taasisi mbalimbali nchini, kufikia lengo linalohitajika.

### UWEZESHAJI ALIYOUPATA

Mkurugenzi Sella, anasema katika mafanikio, hawezi kuisahau Sido Dodoma, kwa sababu ndio taasisi ya kwanza iliyomuwezesha kuchukua mkopo wa kwanza na kumfanya apige hatua aliyo nayo sasa, kwani alishirikiana nayo kwa miongozo na wazo la ujasiriamali.

Sella anasema wao wajasiriamali wana kila sababu ya kuendelea kufanya kazi na Sido, kwa sababu bado wanahitaji anachokiita 'sapoti' yao kufikia wanakopahitaji.

Anasema, alipoanza na mtaji mdogo wa mkopo hakukata tamaa na badala yake, alikaa chini kuona anachotakiwa kukifanya, kulingana na pesa aliyokopeshwa na mwezeshaji wake Sido.

### CHANGAMOTO & MATARAJIO

Changamoto inajulikana siku zote ni pacha wa mafanikio. Sella anasema, mojawapo ni riba kubwa ya mikopo waipatayo kutoka taasisi za fedha katika mikopo yao kwa wajasiriamali, kitendo kinachowafanya wengi wakimbie kutokana na kushindwa kurejesha madeni.

Anasema, hiyo ni changamoto kubwa inayowakatisha tamaa wajasiriamali katika maeneo mbalimbali, hata baadhi wanashindwa kusonga mbali.

Pia, anataja changamoto ya gharama ya upatikanaji vifaa vya ujasiriamali, zikiwamo mashine kama za kukandia unga na ukataji silesi za mikate. Kwa mujibu Sella, moja ya matarajio yake ni kuwa mfanyabiashara mkubwa, atakayetoa ushindani katika Soko la Afrika Mashariki, linalojumuisha wajasiriamali kutoka nchi za ukanda huo.

Rai yake katika sura ya maboresho ni kwamba, hata hivyo amesema ni vema taasisi za mikopo kuwakopesha vifaa vya ujasiriamali badala ya fedha jambo analoamini litasaidia kuwainua wajasiriamali.

### UELIMISHAJI VIJANA

Sella anasema, vijana wanapaswa kuwa mstari wa mbele katika kushiriki mafunzo mbalimbali ya ujasiriamali, yatakayowasaidia kujua mbinu za 'kutoka' katika ujasiriamali wanaofikiria kufanya, kwa sababu tayari wana upeo wa elimu ya vyuo waliopata, wakichanganya na ujasiriamali, anaamini mengi yanaenda sahihi.

Anasema, elimu ya ujasiriamali ni muhimu na hasa ukizingatia taifa linakwenda katika uchumi wa kati wa viwanda, hivyo ni vyema kuchangamkia fursa za uwekezaji kupitia wazo la biashara, ambayo inaifanya isonge mbele, ikiwamo kujiinua kiuchumi kupitia ujasiriamali.

Sella anasema, hakuna sababu ya kubweteka na badala yake kupanua mawazo, ikiwamo kuchangia taasisi zinazojihusisha na utoaji mafunzo ya ujasiriamali, jambo ambalo litasaidia vijana kuingia katika ushindani wa kuwekeza katika ujasiriamali mbalimbali ambao wanahitaji kufanya.

Anashauri umuhimu wa kwenda sambamba na kauli ya serikali hivi sasa, inayoweka msisitizo katika dhana ya uwekezaji na ni muda muafaka kwa vijana kuchangamkia fursa hizo nadra 'kutokea' katika maeneo mbalimbali ikiwamo kushiriki mafunzo au semina za ujasiriamali.

Ushauri anaotoa kwa vijana wenzake, ni kwamba wasibweteke kusubiri ajira, badala yake watengeneze mawazo na kuyafanyia kazi kupitia wataalamu mbalimbali wanaojihusisha kutoa mafunzo ya ujasiriamali kwa jamii.

Anasema, vijana wengi hivi sasa wanakuwa na woga na nasaha zake ni wabadili hisia zao.

### OFISA SIDO

Ofisa Maendeleo ya Biashara wa Sido, Crispin Kapinga, anasema wamefanikiwa kuwainua wajasiriamali wengi, hususani wanaozingatia masharti wanayoelekezwa kupitia ujasiriamali wanaofanya, hasa kwenye kwenye kanuni za biashara.

Kapinga anasema, lengo la Sido ni kuona wajasiriamali wa Dodoma wanasonga mbele na kuingia katika soko la ushindani kimataifa, ikiwamo kushiriki maonyesho ya biashara, kupitia bidhaa bora watakazoleta ushindani.

Anasema Sido imeendelea kuwapa mchango mkubwa katika utafutaji masoko, ushauri wa uendelezaji biashara na vitu mbalimbali vinavyowafanya wapige hatua katika sekta ya biashara.

UCHUMI

# Nguvu ya soko la mafuta ghafi uchumi duniani imefika ukomo



Mitambo ya kusafisha na kuhifadhi mafuta nchini Saudi Arabia. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Nimi Mweta**

HISIA za kitaaluma na kisiasa katika nchi nyingi duniani, ni kuwapo mafuta ya petroli na gesi ndiyo kila kitu. Sasa dunia ilikofika, hilo limepitwa na wakati.

Ingekuwa nyakati zilizopita, dunia ingekuwa katika mtafaruku mkubwa kutokana na kuvurugwa kwa biashara ya mafuta, baada ya vikwazo kuwekwa dhidi ya Iran, kwa upande fulani Venezuela na hivi karibuni kupigwa medani ya mafuta ya Saudia.

Bei ilipanda kiasi, ikashuka katika soko la kimataifa ambayo hasa ni bei elekezi kwa mafuta ambayo hayajauzwa.

Nguvu ya mafuta ilionekana miaka ya 1973 hadi 1974, ambazo bei zilipanda mara tatu, tena kwa viwango vikubwa na kubadili sura ya uchumi wa viwanda duniani.

Wakati mafuta ghafi yakiwa 'bei poa' nchi za Magharibi zilinunua mafuta na kuzalisha bidhaa za viwanda, huku viwanda vikubwa zaidi vikihitaji wafanyakazi wengi au nishati kubwa kwao. Bei ilipanda mara tatu, kisha ikapanda tena kwa kasi, ikabidi viwanda vingi vikubwa vihamishiwe katika nchi zinazoendelea, zenye nguvu kazi 'poa.'

Bei ya mafuta na uchumi wa dunia pamoja na mpangilio wa siasa za kimataifa, ni vitu vimekuwa vikiandamana tangu nyakati hizo. Taratibu mazingira yakabadilika kiasi kwamba sasa mafuta ni bidhaa kama nyingine.

Kuna umuhimu mkubwa wa kimkakati au kimfumo kwa jumla, kwani kuharibika biashara hiyo kutasababisha mvurugano usio wa kawaida, ila kilichokadilika ni uwezo wa nchi moja au kundi la nchi kuitingisha dunia, kwa kufanya uamuzi kuhusu bei, kama ilivyokuwa awali.

> **Badala yake kuna vita zisizoisha Yemen, Syria, Palestina, Irak, Lebanon na majimbo ya wa-Kurdi katika nchi kadhaa, na sasa mzozo unaelekea vita kamili.**

Isitoshe, kuzuia kiasi kikubwa tu cha mafuta kutouzwa nje, kwa mfano vikwazo dhidi ya Iran, halafu Saudia isimamishe mauzo ya mafuta nje kutokana na shambulio, na bei isipande kwa haraka kote duniani, imekuwa jambo lililoshangaza wengi.

Ingekuwa enzi mafuta ghafi yalikuwa 'bidhaa mfalme' duniani, kushambuliwa kwa Saudia na kupoteza nusu ya uwezo wake wa kuzalisha, ungeleta mtafaruku wa haraka zaidi ya 'dodosa dodosa' inauyoendelea hivi sasa nchini Saudia na Marekani.

Wakati Iraq inavamiwa na Marekani mwaka 2003 baada ya shambulio kubwa la Septemba 11, 2001 nchini Marekani, sehemu kubwa ya wachambuzi wa waliafikiana kuwa dhamira ya Marekani ni kukamata mafuta ya Irak. Ni kutokana na mizozo ya jadi kuhusiana na utaifishaji visima, n.k.

Wakati hivi sasa kuna hatari kuzuka vita ya wazi kati ya Iran na Marekani kupitia Saudia, hakuna mchambuzi katika vyombo vya kimataifa, hasa wasemaji wa utawala wa kimapinduzi wa Iran, anayetamka 'Marekani inamezea mate mafuta ya Iran.'

Hata hivyo, katika miongo iliyotangulia mapinduzi ya Kiislamu nchini humo mwaka 1978/79 mafuta nchini Iran, yalikuwa yameshikwa na kampuni za Marekani na kuondoa hali hiyo, ilikuwa moja ya sababu za watu wengi nchini Iran kuunga mkono mapinduzi.

Hivi sasa yapo masuala ya kiitikadi na kiusalama zaidi Mashariki ya Kati na uwekezaji, si ubinafsishaji visima.

**TRUMP & UWEKEZAJI**

Mpangilio huo wa uwekezaji ndiyo uliojitokeza katika mwelekeo wa utawala wa Rais Donald Trump wa Marekani, kuhusu amani ya Mashariki ya Kati, kuacha kutafuta jawabu la nchi mbili na kuangalia uchumi.

Rais Trump kupitia mashauri wake na mkwewe, Jared Kushner, anataka ukanda wote wa Mashariki ya Kati ujengewe mazingira ya kiSADC, yaani nchi hizo zijione kama jumuiya ya uchumi ya kikanda, kwani jitihada za kisiasa kutafuta suluhisho la mizizo iliyopo katika nchi zote hazifiki kokote.

Badala yake kuna vita zisizoisha Yemen, Syria, Palestina, Irak, Lebanon na majimbo ya wa-Kurdi katika nchi kadhaa, na sasa mzozo unaelekea vita kamili.

Wasiwasi ulitanda katika masoko ya mafuta ghafi duniani na masoko ya fedha baada ya shambulio la 'droni' zenye silaha dhidi ya medani kuu ya kuchimba na kuhifadhi mafuta Mashariki ya Saudi Arabia karibuni.

Ilikuwa kumbukumbu ya mashambulizi ya Septemba 11, mwaka 2001 nchini Marekani, iliyolenga kitega uchumi muhimu cha World Trade Centre. pamoja na makao makuu ya Jeshi la Marekani, Pentagon.

Ni miaka 18 imepita sasa, hatari za mashambulizi na uharibifu wa vitega uchumi na maeneo muhimu ya uchumi zimehamia Mashariki ya Kati. Saudia inasema itachukua wiki kadhaa kurudisha uwezo wake kuuza mafuta.

**HALI YA MAFUTA**

Wachambuzi wa habari wanasema kuwa Saudia, inatumia kiasi cha mapipa milioni nne kwa siku na inauza mapipa milioni sita. Hata hivyo, kuondolewa kwa mapipa milioni sita kwa siku katika uchumi wa dunia hakukuleta matokeo makubwa katika soko.

Ni wasiwasi kuhusu bei ya mafuta kwa upande mmoja na thamani za hisa masoko ya Saudia na kwingineko, ambako amana za kampuni zenye hisa kubwa katika mafuta ya Saudia, au benki katika biashara hiyo, iliathirika kiasi. Hata hivyo, haikuchukua muda kurudisha hali ya kawaida.

Katika mazingira ambayo Iran inauza mafuta kidogo tu na kuna wazalishaji wa kati kama Venezuela, nao wako taabani, bei ya mafuta ingeweza kupanda haraka kama hali hiyo ikiendelea.

Rais Trump, katika mshtuko wa kwanza, alizungumzia uwezekano wa kupunguza hifadhi ya mafuta ghafi nchini Marekani, ili bei yake isipande sana. Lakini, soko lilianza kujongea kuwa ya kawaida, wakati pendekezo hilo lilikuwa linaangaliwa.

Ilikuwa msukumo wa kupanda bei kukosa nguvu, siyo kutokana na hakikisho kuwa hapatakuwa na upungufu wa mafuta ghafi...

Nchi nyingine zenye hifadhi kubwa za mafuta ghafi ni Russia, Japan na China. Nazo zilikuwa zinaangalia, kwani dhamira ya hifadhi yao ya mafuta ghafi ni kwa ajali ya matumuzi ya ndani.

Nchi hizo hazina dhamana ya kulinda uchumi wa kimataifa au kuhakikisha uthabiti wake au ukanda wa nchi kama Marekani, ilivyo ushawishi Mashariki ya Kati.

Hivyo, msukumo wa kuachia shehena ya mafuta ghafi iingie katika soko la dunia, ingekuwa lazima kwa Marekani, ili nchi washirika katika maeneo tofauti zisitetereke, wakati Russia ilishindwa kuisaidia Iran ilipowekewa vikwazo kuuza mafuta nje. Badala yake swahiba wake huyo, anauza mafuta zaidi nje sasa.

Dunia ikishuhudia mwisho wa zama 'King Oil' (Mfalme wa Mafuta) ni jambo jema kiuchumi na kiusalama, kwani mataifa mengi yaliyumba pale bei za mafuta zilipopanda kwa haraka.

Kumbukumbu ya miaka ya 1973/74, ni kipindi ambacho wasomi wengi serikalini na sekta binafsi waliingia katika umaskini. Hapakuwapo mbadala baada ya bei ya mafuta kupanda na thamani ya fedha ya nchi kuanza kudidimia. Ila, hapakuwapo mkasa kisiasa hapa.



Wananchi na wanafunzi wakisubiri kuteka maji kwenye bomba la Kijiji cha Mlandala, kinachokabiliwa na uhaba wa majisafi, wilayani Ikungi mkoani Singida juzi, baada ya tangi kupasuka. **PICHA: DOTTO MWAIBALE**

# Bibi adaiwa jaribio kumnyonga mjukuu kisa mtoto wa mbuzi

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MKAZI wa Kijiji cha Sendoo, Halmashauri ya Mji wa Babati mkoani Manyara, Celina Haidau (66), anatuhumiwa kwa jaribio la kumnyonga mjukuu wake mwenye umri miaka saba kwa madai ya kusababisha mtoto wa mbuzi aliyekuwa anamchunga kuliwa na mbweha.

Sendoo anadaiwa kufanya tukio hilo Septemba 23, baada ya mtoto huyo kutoka kuchunga mbuzi wa bibi huyo na kugundulika kuwa mtoto wa mbuzi alikuwa ameliwa.

Msamaria mwema aliyetoa taarifa za tukio hilo, Hamis Seleman, akizungumza na Nipashe, alisema mtoto aliyekuwa anannyongwa amedaiwa kuadhibiwa na bibi huyo kupita kiasi na kufanyishwa kazi ngumu kama kusomba mbolea ya samadi na kuchota maji pipa mbili kwa siku.

"Mtoto huyu pamoja na mdogo wake walitelekezwa na wazazi wao ambao walimwachia bibi huyo," alidai Seleman.

Alidai mtoto huyo alimbaini kufanyiwa ukatili na bibi yake baada ya kumkuta kituo cha kuchotea maji akibeba dumu la maji la lita tano na kushindwa kulibeba kutokana na maumivu aliyokuwa akiyapata.

Alidai kuwa alipomhoji alimweleza tukio hilo na yeye alifanya jitihada za kutoa ripoti ofisi ya kijiji ili mtoto huyo aweze kuepuka manyanyaso.

"Nilipomfikisha ofisini alieleza jinsi alivyopigwa na bibi yake ambaye alitaka kujua kwanini alimuacha mbweha akakila kitoto cha mbuzi na kuonyesha alivyokuwa akinyongwa na bibi huyo," alidai.

Seleman alidai bibi huyo amekuwa akiwatesa watoto hao walioachwa na wazazi wao toka Novemba, 2018.

" Septemba 25, bibi huyu alimpiga mtoto huyu kwa kosa la kumpiga mbuzi mguuni, pia yeye na mdogo wake wamekuwa wakifanyishwa kazi ngumu na kunyimwa haki ya kupata elimu. Bibi alipofikishwa ofisi ya kata alikiri kuwa anawapiga watoto hao na kuuliza mbona hawafi, leo hii ndio watakufa," alidai Msamaria mwema huyo alisema mtoto huyo alikutwa amejaa vidonda vya majeraha na kuvimba tumbo na kichwa, hivyo kwa kushirikiana na ofisi hiyo na ofisa mtendaji walimpeleka Hospitali ya Mrara kwa matibabu na kukabidhiwa balozi kwa ajili ya ulinzi yeye na mdogo wake.

Naye Ofisa Mtendaji wa Kijiji Cha Sendoo, John Mayo, akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo.

# Wanaume Simiyu wavuka lengo kufanyiwa tohara

**Na Happy Severine,** SIMIYU

ZAIDI ya wanaume 60,000 wamefanyiwa tohara salama kwa kipindi cha mwaka mmoja kuanzia Oktoba 2018 hadi Septemba 2019 katika Mkoa wa Simiyu ikiwa ni zaidi ya asilimia 100 ya lengo lililowekwa la kuwafikia wanaume 58,246 kupitia kampeni ya tohara kinga.

Mratibu wa Ukimwi Mkoa, Dk. Hamis Kulemba, alitoa takwimu hizo wakati wa mafunzo kwa waendesha pikipiki za kubeba abiria (bodaboda) wa wilaya za Itilima na Meatu yaliyokuwa na lengo la kuongeza uhamasishaji kwa vijana na wanaume kujitokeza zaidi kufanyiwa tohara.

"Kupitia kampeni ya Tohara Kinga inayoendeshwa na shirika lisilokuwa la kiserikali linalojihusisha na masuala ya afya, IntraHealth International kwa kushirikiana na serikali tulikuwa na lengo la kuwafikia wanaume 58,246, lakini tumevuka na kuwafikia wanaume 63,240 sawa na asilimia 109," alisema Dk. Kulemba.

Alisema kuwa kutokana na mkoa wa Simiyu kuwa na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kwa kiwango cha asilimia 3.9, kampeni hiyo ambayo bado inaendelea mpaka 2021 itafanikisha kupunguza maambukizi mapya kutokana na tohara kuwa kinga kwa zaidi ya asilimia 60.

"Tunashukuru IntraHealth kwa msaada wao wamefanya kazi kubwa, wamehamasisha vijana kujitokeza kufanyiwa tohara na wamejitokeza kwa wingi, tuna imani maambukizi mapya yatapungua kwa kiwango kikubwa," alisema Dk. Kulemba.

Mratibu wa mradi huo kutoka IntraHealth, Dk. Kentgen Evarist, alisema lengo la mafunzo hayo ni kutaka waendesha pikipiki hao kutumia nafasi waliyonayo kwenye jamii kuhamasisha vijana wengi zaidi wajitokeze kufanyiwa tohara.

Dk. Evarist alisema, mradi huo chini ya ufadhili wa Mfuko wa Rais wa Marekani wa kupambana na VVU (PEPFAR) kupitia CDC Tanzania, umepata mafanikio makubwa kwa vijana wengi kujitokeza kutokana na kuelimishwa umuhimu wa tohara kupitia vikundi mbalimbali pamoja na uhamasishwaji.

"Kampeni hii tumekuwa tukiitekeleza katika wilaya za Itilima, Meatu, na Bariadi na tumefanikiwa kwa kiwango kikubwa, bado utekelezaji wake unaendelea tuna uhakika malengo ambayo tulijiwekea kwa muda wa miaka mitano yatafikiwa," alisema Dk. Evarist.

Naye Mkuu wa Polisi Wilaya ya Meatu, Elisante Ulomi, aliwataka waendesha bodaboda hao kutumia nafasi waliyonayo katika jamii kuhamasisha vijana wengi kujitokeza kwenda kufanyiwa tohara.

Charles Masanja mmoja wa waendesha bodaboda kutoka Itilima, alisema mafunzo hayo yamewapa mwanga wa kufahamu mambo mengi kuhusu tohara.

# NBC yazindua kampeni ya kurahisisha malipo

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya NBC leo imezindua huduma yake maalumu ya kidijitali ambayo pamoja na mambo mengine inalenga kurahisisha huduma ya malipo kwa wateja wake wanaofanya miamala ya malipo kwa taasisi mbalimbali ikiwamo malipo ya serikali, umeme na huduma za maji.

Akizungumza wakati wa hafla fupi ya uzinduzi wa huduma hiyo jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi wa Idara ya wateja wa kati na wadogo wa Benki ya NBC, Bw Elibariki Masuke alisema huduma inayohusisha usajili wa chini ya muda wa dakika tano tu na inaondoa kabisa matumizi ya karatasi katika usajili ambao hapo awali ulikuwa ukitumia muda mrefu huku pia ukihusisha mahitaji ya nyaraka nyingi.

"Kupitia huduma hii mteja anachotakiwa ni kufika tu kwenye matawi yetu akiwa na kitambulisho cha uraia kutoka NIDA na ndani ya dakika 5 tu tayari atakuwa amefanikiwa kujisajili sambamba na kupatiwa kadi yake ya ATM na kuunganishwa na huduma ya Simbanking,''

"Na kwa wateja ambao watashindwa kufika kwenye matawi yetu wanaweza kuwatumia mawakala wetu pamoja na mamia ya maofisa wetu watakaokuwa tayari kuwasaidia kufanikisha usajili huo bila gharama yoyote,'' alibainisha.

Kwa mujibu wa Masuke, huduma hiyo ya Kidijitali itawasaidia wateja wanaolipa ankara za maji, ankara za huduma za televisheni na huduma ya kutuma fedha bila kuhitaji kubeba fedha.

Alisema kampeni hiyo inafahamika kama 'Kulipa Inalipa' ikimaanisha kwamba mteja wa benki hiyo atanufaika kwa kufanya malipo kupitia huduma hiyo na kwamba mteja anapojisajili kupitia huduma hiyo ataingia moja kwa moja kwenye droo ambayo kila siku itatoa zawadi ya fedha kiasi kisichopungua Sh. 10,000 kwa mshindi.

Aliongeza kuwa kupitia huduma hiyo wateja wa benki hiyo wanaepushwa na gharama za kutoa miamala kwenye mashine za kutolea fedha za ATM pamoja na huduma ya mwezi ya kuhudumia akaunti zao isipokuwa watatozwa gharama pale tu watakapotumia huduma za dirishani.

Mkuu wa Idara ya Huduma za Kidigitali kutoka benki hiyo, Deogratius Mosha, alitoa wito kwa jamii kufungua akaunti na benki hiyo kwakuwa imefanya mabadiliko makubwa kwa kuwekeza kwenye huduma za huduma za kisasa yakilenga kurahisisha huduma za kibenki kwa wateja wa benki hiyo.



## HABARI DODOMA

# Marufuku wahitimu la 7 kufanyishwa kazi za ndani

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, amepiga marufuku wazazi wenye watoto waliohitimu darasa la saba kuwaruhusu kwenda kufanya kazi za ndani kabla ya matokeo kutoka kwa kuwa inasababisha baadhi yao kushindwa kujiunga na kidato cha kwanza.

Mahenge alitangaza marufuku hiyo jana alipokuwa akizungumza na wazazi wa Kata ya Chang'ombe kwenye ufunguzi wa madarasa ya Shule ya Msingi Chang'ombe 'B' jijini Dodoma ambayo yamejengwa na Mbunge wa Dodoma Mjini, Anthony Mavunde.

Alisema hataki kuona mzazi yeyote anamruhusu mtoto kwenda kufanya kazi za ndani kabla ya matokeo kutoka.

"Sitaki kuona mzazi yeyote anamruhusu mtoto kwenda kufanya kazi hasa kazi za ndani, kwani watoto wengi wamekuwa wakipata ujauzito kabla ya matokeo, hivyo kushindwa kutokujiunga na masomo ya sekondari na matokeo yake kukatisha ndoto zake," alisema.

Aidha, aliwaagiza wakurugenzi wa halmashauri kuhakikisha wanajenga vyumba vya madarasa ili kuondoa usumbufu kwa wanafunzi wanaofaulu kidato cha kwanza kama ilivyojitokeza mwaka jana, ambapo baadhi walichelewa kujiunga na kidato cha kwanza kutokana na uchache wa madarasa.

Alisema kwenye mkoa wake hataraji kuona au kusikia wanafunzi watakaofaulu mwaka huu wanapata usumbufu wa kukosa vyumba vya madarasa.

"Niwaagize wakurungezi wote mhakikishe mnajenga vyumba hivyo ili kuondoa usumbufu huo," alisema.

Alitoa wito kwa wazazi kushiriki shughuli za maendeleo kama zilivyoonyeshwa na Mbunge ambaye amejitolea kujenga vyumba viwili vya shule hiyo.

"Ninawaomba wananchi jitokezeni kwa kuunga mkono kwa vitendo pale wanapojitokeza viongozi kama Mbunge wa Dodoma Mjini, ambaye amejitoa kwa fedha zake kujenga vyumba viwili vya madarasa," alisema.

Mavunde ambaye ni Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, alisema ujenzi wa vyumba hivyo ni miongoni mwa ahadi zake ambazo alikuwa ameziahidi kwa wananchi wakati akiomba kuchaguliwa kuwa mbunge.

Alisema pamoja na kukamilisha ujenzi huo wenye gharama ya Sh. milioni 30 na pia ameanza ujenzi wa jengo la utawala ambalo litatumika kama ofisi ya walimu.

Aliahidi kutoa kompyuta 135 katika shule zote za msingi na sekondari zilizopo kwenye jimbo lake, ambapo tayari kompyuta 85 zimeshatolewa kwa shule za msingi na sekondari.



Mkurugenzi wa kiwanda cha kukamua mafuta ya alizeti cha Zain Oil Mills, Salman Gulamali (kushoto), akimwonyesha Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge (wa pili kushoto), jinsi mashine za kiwanda hicho, zinavyofanyakazi ya kuzalisha mafuta, alipotembelea kiwanda hicho, eneo la Kizota jijini Dodoma juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Chaula aagiza matumizi ya takwimu hospitalini

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Zainabu Chaula, amewaagiza waganga wakuu wa mikoa na wilaya kusimamia watendaji wa hospitali kutumia takwimu kwenye huduma wanazotoa ili kuhakikisha usalama wa wagonjwa.

Dk. Chaula alitoa kauli hiyo jana, alipokuwa akifungua kongamano la tatu la mifumo ya kutathmini na kufuatilia huduma za afya.

Alisema kutumika vizuri kwa takwimu katika utoaji wa huduma za afya, utasaidia kuboresha huduma hiyo na kuhakikisha usalama wa wagonjwa.

"Mfano mgonjwa kaja, ukiwa na kumbukumbu ya takwimu aliumwa nini na akatumia dawa gani labda Panadol, lakini akarudi tena na ugonjwa huo ukiwa na takwimu awali ulimtibu kwa Panadol itabidi ubadilishe," alisema.

Aidha, alihimiza haja ya kuwa na takwimu sahihi ili kusaidia katika kutekeleza mipango ya kuboresha huduma za afya nchini. "Tukiwa na takwimu zisizo sahihi hatuwezi kufika mbali, mfano takwimu zinaonyesha Hospitali ya Mwananyamala inaongoza kwa kuona wagonjwa zaidi ya laki sita, wanafuatiwa na Temeke zaidi ya laki nne na ya tatu ni Tanga, hapo unaweza jiuliza hivi Tanga ni kweli inaipita Hospitali ya Amana."

"Hii inakuonyesha takwimu zinatolewa tu ili mradi na hatuwezi kufika mbali," alisema.

Naye Kaimu Mkuu wa Skuli ya Utawala na Manejimenti katika Chuo Kikuu cha Mzumbe, Dk. Eliza Mwakasangula, alisema Mzumbe kwa kushirikiana na vyuo kadhaa imebaini kuna msisitizo mdogo wa matumizi ya takwimu katika mitaala ya wanaosoma ngazi ya cheti na stashahada. Alisema Mzumbe kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), MUHAS, Taasisi ya Afya ya Ifakara, na Chuo cha Madaktari Ifakara kinafanya utafiti mwaka 2017/2018 katika suala zima la matumizi ya takwimu katika sekta ya afya na kuonyesha kuwa kwenye mitaala ya wanaosoma ngazi ya cheti na stashahada kuna msisitizo mdogo kwenye matumizi ya takwimu.

Alisema matokeo ya utafiti huo pia yalionyesha wafanyakazi hawana utamaduni wa kutumia taarifa wakati wa kufanya maamuzi wana uwelewa mdogo kwa watumishi kwenye suala zima la kuchakata taarifa.

Alisema baada ya kubaini mapungufu hayo, muungano wa taasisi za elimu ya juu na utafiti (CBC) wakishirikiana na Wizara ya Afya wanafanya maboresho mitaala mitano na kuweka msisitizo kwenye suala la matumizi ya taarifa.

# ... Mpwapwa zuio mgodini

**Na Mwandishi wetu,** MPWAPWA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, amepiga marufuku watoto wenye umri chini ya miaka 18 kufanya kazi katika machimbo ya dhahabu yaliyopo kijiji cha Kikuyu wilayani humo.

Kufuatia marufuku hiyo, wazazi na walezi watakaowaachia watoto wao kwenda mgodini watakamatwa wao.

Shekimweri alitoa kauli hiyo juzi katika ziara ya kutembelea machimbo ya dhahabu yaliyopo kijiji cha Kikuyu Kata ya Ipera alipokuwa akizungumza na wachimbaji wadogo.

"Nimepiga marufuku watoto hao kufanya kazi na kuwataka wakasome, tumesisitiza wazazi na walezi watakaowaachia watoto kwenda machimboni na tutawakamata wao," alisema.

Alisema serikali katika kutambua mchango wa wachimbaji wadogo, ameona ni muhimu kuwatembelea na kusikiliza kero zao ili aweze kuzitafutia ufumbuzi.

"Wachimbaji mtambue kuwa serikali ya wilaya ipo tayari kuona mkiendelea na shughuli za uchimbaji ilimradi tu mzingatie sheria, kanuni na taratibu za tasnia ya madini kikamilifu," alisema.

Aidha, aliwataka kuhifadhi mazingira kwa kuwa uchimbaji wa madini holela huchochea ukataji wa miti hivyo.

Katika ziara yake aliyoambatana na Kamati ya Usalama, Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji na Wataalamu kutoka Ofisi ya Ofisa Madini Mfawidhi Mkoa wa Dodoma, Shekimweri alitoa nafasi kwa wataalamu wote kutoa elimu kuhusu masuala mtambuka ya uchimbaji salama pamoja na tamko ya sera za madini.

Aliwaasa wachimbaji hao kutambua na kuenzi azma ya Rais John Magufuli ambaye alizungumza na wachimbaji wote na kuwataka wawe wazalendo kwa kulipa kodi na tozo stahili na kufichua wanaotorosha madini.

Alifafanua kuwa ukaguzi uliofanyika, ilibainika eneo hilo kuwa na ajira za watoto chini ya miaka 18, kutokuwa na vyoo, kuwapo ukataji miti na ufinyu wa huduma hususani majisafi na salama.

Aidha, alibaini uwepo wa wanunuzi na tayari wameanza kufanya biashara kwenye soko kubwa la Dar es Salaam.

Aidha, alitumia nafasi hiyo, kukemea na kumtaka Mkurugenzi wa Halmashauri kuhakikisha wanunuzi na wauzaji hao wana kwenda kuripoti kwake na risiti walizouzia ili kodi na tozo mbalimbali zinazopaswa kutolewa.

Aidha, alieleza kuwa wilaya inakamilisha taratibu za uanzishwaji wa soko la Madini la wilayani na linatarajiwa kuanza rasmi Oktoba Mosi 2019.





# Utaratibu wa kuchimba kokoto, kifusi watajwa

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

KATIKA jitihada za kulinda na kuhifadhi mazingira, serikali imeweka utaratibu wa kuchimba kifusi, mawe, kokoto na matofali ya jasi, kwa ajili ya miradi ya umma na watu binafsi.

Akitoa tamko la serikali kuhusu uratibu wa matumizi ya maliasili zisizorejesheka, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Haji Omar Kheir, alisema utaratibu huo unakusudia kuimarisha utekelezaji na utii wa sheria na uhifadhi wa mazingira.

Alisema serikali imetoa ruhusa ya uchimbaji na usafirishaji wa maliasili zisizorejesheka kwa masharti maalumu yakiwamo kusajiliwa viwanda vyote vya kokoto kulingana na Sheria Na. 3 ya Usimamizi wa Mazingira ya Mwaka 2015.

Aidha, itahakikisha kuwa kokoto zinauzwa kwa wenye stakabadhi ya malipo na si vinginevyo.

Aliyataja masharti mengine kuwa uchumbaji wowote wa maliasili zisizorejesheka usizidi kina cha mita tatu kwenda chini.

Kadhalika miradi au wawekezaji wenye mahitaji ya kifusi, mawe au kokoto watalazimika kumwandikia Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na kuainisha kiwango wanachohitaji na sehemu au eneo atakalokwenda kuchukua.

Waziri Kheir, aliyataja maeneo yatakayotumika kwa uchimbaji mawe kwa Unguja kuwa ni Kibuteni, Zuze Dunga, Umbuji na Ndijani kwa Wilaya ya Kusini.

Machimbo mengine yapo Matemwe, Kidoti Kaskazini Unguja na Wilaya ya Magharibi A watachimba eneo la Nyamanzi, Kisakasaka na kwenye ukanda wa magharibi.

Kwa visiwani Pemba alisema kuwa ni pamoja na Muambe wilayani Mkoani Pujini na Vitongoji Wilaya ya Chakechake na Micheweni Wilaya ya Micheweni.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilisimamisha kwa muda uchimbaji wa kifusi, kokoto, mawe na matofali ya jasi ili kufanya tathmini na kuandaa mpango wa matumizi ya maliasili zisizorejesheka Agosti 27, mwaka 2019.

# Pemba mbioni kusafisha figo

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WIZARA ya Afya Zanzibar ipo katika hatua za mwisho za matayarisho ya chumba kwa ajili ya wagonjwa wanaosafishwa figo.

Naibu Waziri wa Afya, Harusi Suleiman, alisema hayo wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Jimbo la Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliyetaka kujua lini huduma za wagonjwa wanaohitaji matibabu ya kusafishwa figo zitapatikana kisiwani Pemba.

Naibu Waziri huyo, alisema juhudi zimeanza kufanyika ikiwamo kujenga chumba kwa ajili ya kusafisha figo, ambapo taasisi zimekubali kusaidia kugharamia huduma hizo.

Alisema wizara hiyo tayari imepokea mashine nne kwa ajili ya kazi za kusafisha figo ambazo zitawekwa katika Hospitali ya Abdallah Mzee Pemba.

"Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba tumeanza kazi za kujenga chumba ambacho kitatumiwa na wagonjwa wanaohitaji matibabu ya figo katika Hospitali ya Abbdallah Mzee Pemba," alisema.

Alisema, hatua hiyo itasaidia na kuwafanya wagonjwa wenye kuhitaji huduma hizo kupatiwa matibabu yao huko huko Pemba.

"Hayo ndiyo malengo ya wizara yetu kuona kwamba huduma za afya zinawafikia wananchi wote Unguja na Pemba bila ya malipo kwa mujibu wa sera ya Wizara ya Afya," alisema Suleiman.



Mwakilishi wa Jimbo la Mpendae, Muhammed Said Dimwa (kushoto), akizungumza na wageni waliofika katika Baraza la Wawakilishi, Chukwani mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ kuvidhibiti vituo vya watoto

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar iko katika hatua za kukamilisha mchakato wa kuweka mwongozo na utaratibu wa kisheria utakaodhibiti uanzishwaji vituo vya matunzo na kulea watoto.

Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto, Mauldline Castico, alisema hayo wakati akisoma taarifa ya utekelezaji wa ripoti za Kamati za Baraza la Wawakilishi ya Wanawake na Watoto katika kikao cha baraza hilo.

Castico alisema ni muhimu kuwapo kwa mwongozo huo ambao utaonyesha nani anayestahili kuanzisha vituo vya kutunza watoto na sababu zipi za msingi za kuweka huduma hiyo.

Alieleza kuwa hivi karibuni kumejitokeza tabia ya baadhi ya watu kuanzisha vituo vya malezi ya watoto bila ya kufuata utaratibu unaofahamika na kuzingatia sheria. Alisema zipo athari kubwa za kuanzisha vituo vya kulea watoto bila ya kufuata utaratibu na kupata kibali ikiwamo kuwapo uwezekano wa kujitokeza kwa vitendo vya udhalilishaji wa watoto. "Wizara inakusudia kuweka mwongozo unaofahamika kwa mujibu wa sheria kuhusu uanzishaji wa vituo vya malezi ya watoto nchini," alisema.

Hata hivyo, Castico aliitaka jamii kufuata utaratibu wa asili na jadi ambapo mtoto hulelewa na familia pamoja na wazazi na walezi wakiwamo ndugu wa damu. Alisema vituo vya kulelea watoto na matunzo ni suluhisho la mwisho ambapo hufanyika tu baada ya kushindikana kwa taratibu nyingine muhimu.

"Tunataka kuifunza jamii yetu kwamba malezi rasmi ya watoto yanatokana na wazazi wake au familia yake na vituo vya kulea watoto ni suluhisho la mwisho," alisema Waziri.

Aidha, aliikemea tabia ya wanawake kutupa watoto mara wanapojifungua na kusema hilo ni kosa kwa mujibu wa sheria na halikubaliki.

"Wizara ya Wanawake na Watoto inakemea vikali tabia iliyojitokeza ya wazazi kutupa watoto mara wanapojifunguwa ambapo ni kosa kwa mujibu wa sharia na hatupo tayari kuvumilia uovu huu," alionya waziri.

# Kudorora gesi kwakwaza biashara

**Na Hamisi Nasiri,** MTWARA

KUSIMAMA kwa muda mrefu utekelezaji wa miradi ya uwekezaji katika sekta ya gesi asilia mkoani Mtwara kumeathiri kwa kiwango kikubwa biashara ya hoteli na nyumba za kulala wageni mkoani hapa.

Biashara hizo ziliwekezwa kwa kutegemea fursa ya uwapo wa rasilimali ya gesi asilia.

Hayo yamebainishwa na Mwenyekiti wa Chemba ya Wafanyabiashara wenye Viwanda na Kilimo Tanzania (TCCIA) Mkoa wa Mtwara, Saidi Swallah, katika kikao cha kujadili vikwazo vya uwekezaji kwa wawekezaji na wafanyabiashara wa mkoani hapa, kilichowahusisha mawaziri na manaibu waziri wanaohusika na masuala hayo.

Alisema hivi sasa mkoani Mtwara kumekuwa na athari kubwa za kuyumba kwa biashara katika sekta binafsi hasa biashara za mahoteli pamoja na nyumba za kulala wageni na hiyo imechangishwa na kusimama kwa muda mrefu utekelezaji wa miradi ya gesi asilia ambayo serikali iliibua.

Alisema mwaka 2010 na 2014 iliibuliwa miradi ya mafuta na gesi mkoani Mtwara, lakini cha kushangaza baadaye miradi hiyo utekelezaji wake umesimama ghafla.

Swallah alisema kutokana na hali hiyo, imesababisha kutoweka kwa matarajio ya wawekezaji wengi mkoani humo ambao walitegemea uwapo wa miradi ya gesi ambayo wangenufaika nayo kwa kuwekeza vitega uchumi mbalimbali. Alisema baadhi ya wafanyabiashara, biashara zao zimefungwa kwa kukosa wateja, lakini pia wapo wafanyabiashara ambao hivi sasa wameshindwa kurejesha mikopo yao benki kwa sababu ya kushindwa kuendeleza biashara.

Alisema wafanyabiashara walihamasishwa kuwekeza kwa kutumia fursa ya uwapo wa gesi mkoani Mtwara na watu walihamasika na wengine kudiriki hata kwenda kukopa fedha kwenye benki ili kuwekeza kwa matarajio ya miradi ya gesi, lakini mambo yamekwenda tofauti.

"Hata leo hii ukifanya utafiti kwenye sekta hii ya nyumba za kulala wageni na hoteli, utagundua hali ni tete kabisa hata bei ya kulala kwenye hizi nyumba za wageni ni maelewano, lakini hii yote inatokana na kusimama kwa miradi ya gesi," alisema Swallah.

Mawaziri ambao walishiriki kikao hicho ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu-Uwekezaji, Angela Kairuki; Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa na Waziri wa Madini, Doto Biteko.




Mkurugenzi Mtendaji wa Sekta Binafsi nchini (TPSF), Geofrey Simbeye (kushoto), akiteta jambo na Mkurugenzi wa Huduma za wanachama TPSF, Zachy Mbenna, kwenye mkutano na waandishi wa habari (hawako pichani) kuhusu mkutano mkuu wa 19 wa mwaka wa wadau wa sekta binafsi utakaofanyika kesho jijini Dar es Salaam. **MPIGAPICHA WETU**

# Mkutano mkuu kutathmini muundo, utendaji wa TPSF

**Na Mwandishi Wetu**

MAANDALIZI ya Mkutano Mkuu wa 19 wa Mwaka wa Taasisi ya Sekta Binafsi nchini (TPSF) unaotarajiwa kufanyika jijini Dar es Salaam kesho yamekamilika, ambapo wanachama wameombwa kushiriki kwa wingi pamoja na kufanya tathmini ya utendaji na kuangalia muundo wake ili kuendana na wakati.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi hiyo, Godfrey Simbeye, alisema wajumbe watapata nafasi kujadiliana masuala mbalimbali ikiwamo muundo wa taasisi ili kukidhi matarajio ya wadau wote katika sekta za biashara na uchumi.

"Mkutamo huo wa siku moja umelenga kupitia upya muundo wa TPSF na namna ya kuwafikia wanachama wapya ili kwenda sambamba na azma ya serikali ya Serikali ya Rais John Magufuli ya kujenga uchumi wa kati na viwanda ifikapo mwaka 2025," alisema Simbeye. Alisema TPSF kama taasisi inayosimamia na kuunganisha sekta binafsi, inawajibu wa kujitathmini ili kwenda sambamba na malengo ya taifa pamoja na kujiweka katika nafasi nzuri ya kufanikisha malengo hayo.

"Kutokana na umuhimu wa mkutano huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, atakuwa mgeni rasmi ambaye atawakabidhi vyeti wanachama wapya," alisema.

Alisema mkutano huo utatumika kuangalia kwa undani namna ya kukabiliana na changamoto zinazokwamisha uwekezaji nchini hali itakayosababisha kushindwa kutimiza au kufikia azma ya serikali kwa wakati muafaka

"Mambo mengine ambayo yatapewa kipaumbele katika mkutano huo wa siku moja ni pamoja sera ya Tanzania kuelekea uchumi wa kati na viwanda, kukuza utawala bora ndani ya TPSF, kupanua shughuli za utendaji wa TPSF, utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya tabia nchi," alisisitiza Simbeye. Septemba 7, mwaka huu Rais Magufuli aliitaka sekta binafsi kutanua wigo wa huduma zake hususani maeneo ya mikoani ili kuwafikia walengwa na hivyo mkutano wa mwaka huu kwa mujibu wa Simbeye, utaipa kipaumbele ajenda hiyo ambayo ni agizo kutoka kwa Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Biashara (TNBC).

Mkurugenzi wa Huduma za uanachama wa Taasisi hiyo, Zachy Mbenna, alisema mkutano huo utakuwa kama sehemu ya kuleta muunganiko kwa wafanyabiashara nchini.

"Tunaomba wanachama wajitokeze kwa wingi kwani hii ni fursa pekee kwa wadau kukutana na kujadiliana juu ya changamoto mbalimbali ili kuleta matokeo chanya katika sekta ya viwanda na biashara," alisema Mbenna.

Mkutano huo unatarajiwa kuhudhuriwa na taasisi mbalimbali za umma zikiwamo TRA, TBS na wawakilishi kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara.

# RC awezesha sekta za afya, elimu

**Na Hamisi Nasiri,** MASASI

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Gelasius Byakanwa, ametoa msaada wa jumla ya bati 72 ambapo bati 36 kwa ajili ya Shule ya Msingi Mpeta, bati 36 kwa Zahanati ya Mnavila.

Lengo likiwa ni uboreshwaji wa miundombinu ya elimu pamoja na sekta ya afya katika mkoa wake.

Byakanwa alitoa msaada huo jana wilayani Masasi na kukabidhi kwa viongozi na madiwani wa halmashauri ya wilaya ya Masasi.

Alisema wakati akiwa katika ziara zake za kikazi kwenye maeneo mbalimbali ya halmashauri ya wilayani Masasi, alifanikiwa kupita Kijiji cha Mpeta na kukuta Shule ya Msingi Mpeta imejengwa vyumba vya madarasa, lakini havijapauliwa kwa kukosa bati.

Alisema baada ya kukuta miradi hiyo imesimamiwa vema na wananchi, huku bado ikihitaji vifaa hivyo ili iweze kukamilika kwa asilimia 100, ndipo ofisi yake iliguswa na kuamua kutoa ahadi ya kukabidhi bati hizo.

"Wakati nikiwa katika ziara yangu maeneo tofauti wilayani Masasi, nilikuta miradi inayosimamiwa na wananchi ya zahanati na madarasa ikiwa inahitaji bati kwa vile niliahidi hivyo leo ninatoa bati 36 kwa shule ya msingi Mpeta na bati 36 kwa Zahanati ya Mnavila," alisema Byakanwa.

Alisema kupitia jitihada hizo inazozifanya serikali ya mkoa wa Mtwara kwa kuwaunga mkono wananchi kwa kutoa bati hizo itaongeza hamasa kwa wananchi hao kuendelea kujitolewa katika shughuli za kimaendeleo kwenye maeneo yao.

Alisema ofisi ya mkuu wa mkoa itaendelea kushirikiana na wananchi kwenye maeneo mbalimbali kufanikisha miradi ya maendeleo kwa kushiriki moja kwa moja sambamba na kuongeza nguvu miradi inayosimamiwa na wananchi wenyewe.

Alisema katika bati hizo 72, bati 36 amezitoa kwa ajili ya Shule ya Msingi Mpeta na bati 36 ni kwa Zahanati ya Mnavila na ahadi yake ni kutoa bati zaidi ya 100, ambapo maeneo mengine pia wanauhitaji wa vifaa kama hivyo.

## Mbwa, paka 300 wafugwa

INATOKA UK. 3

ulikuwa na kibali maalum cha kuingia humu. Kila anayeingia humu lazima afuate taratibu za kupata kibali."

Mkurugenzi huyo alimuuliza ni utaratibu gani unapaswa kufuatwa kwa ajili ya kupata kibali ndipo akasema: "Unapiga simu kabla ya kuingia humu na kama kuna nafasi tunakuruhusu uingie."

Baada ya kujibiwa hivyo, mkurugenzi huyo aliuliza: "Unaelewa nilichokisema awali? Tunaamini eneo na nyumba hii ni mali yetu, mpigie simu mmiliki aje, hatusubiri nje kwa kuwa hapa ni kwetu wewe mwambie mhusika aje."

Hata hivyo, aliwataka kusubiri nje ya geti wakati anafuatilia kama wana kibali cha kutembelea eneo hilo na baada ya majibizano ya muda mfupi, mkurugenzi na timu yake waliingia kwenye nyumba hiyo na kujionea paka wakiishi ndani na mbwa eneo la nje.

Akizungumza akiwa ndani ya eneo hilo, Mwakibibi alisema mara nyingi halmashauri imewatafuta wahusika wa nyumba hiyo na wanazima simu, huku wakidai waliuziwa na Manispaa ya Temeke.

"Tumegundua nyumba hii inatunza mbwa na paka. Nyumba ya serikali inatunza mbwa na paka zaidi ya 300," alisema.

Mwakabibi alisema uchunguzi uliofanywa na manispaa hiyo ulibaini kuwa nyumba hiyo inamilikiwa kihalali tangu mwaka 2000 baada ya kukabidhiwa na Jiji la Dar es Salaam.

Aidha, alisema iliuzwa kinyemela na mtu asiyejulikana na hakuna kodi yoyote ya pango inayolipwa kwa manispaa hiyo.

Kijana aliyekutwa akiwahudumia wanyama hao, alisema lengo la kuwakusanya wanyama hao ni kwa ajili ya kupunguza wanyama wanaozagaa mtaani.

"Wazo lilikuwa kuwasaidia wanyama walioko nje kuwapunguza, tukapata hili eneo na nipo zaidi ya miaka mitano. Nilianza kwa kujitolea na tunaelimisha watu kuwa tunaisaidia nchi yetu," alisema.

Viongozi hao wakiwa eneo hilo, walisema wanaodaiwa kumiliki eneo hilo walipigiwa simu na kuahidi kufika ndani ya saa mbili, lakini hawakufanya hivyo na baadaye simu zilizimwa.

# Majaliwa aiagiza Tamisemi kuifuatilia Njombe, Tanga

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amemwagiza Naibu Waziri Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) afuatilie sababu za mikoa ya Tanga na Njombe kutotekeleza sheria ya kutoza asilimia tano ya ushuru unaotokana na mazao ya misitu.

Alisema kampuni zinazonunua nguzo lazima zihakikishe zinazingatia sheria ya nchi ikiwamo ulipaji wa kodi zilizowekwa kwa mujibu wa sheria na kampuni zote zilizonunua nguzo bila ya kulipa kodi zifuatiliwe na zilipe kodi yote waliyoikwepa.

Waziri Mkuu ameyasema hayo jana alipotembelea kiwanda cha kutengeneza nguzo za umeme cha Qwihaya kilichoko Mafinga wilayani Mufindi akiwa katika siku ya tatu za ziara yake ya kikazi mkoani Iringa.

"Naibu Waziri Tamisemi hakikisha unakwenda mkoani Njombe na uanze kuzungumza na mkuu wa mkoa, tunataka kujua kwa nini hawajaanza kutekeleza sheria ya kutoza asilimia tano ya ushuru unaotokana na mazao ya misitu hali iliyosababisha wanunuzi kukimbilia huko na kuacha kununua mazao hao katika mkoa wa Iringa."

"Tunataka tujue ni nani huyo anayewakataza wasilipe kodi na tuangalie anauhusiano gani na viongozi wa mkoa huo. Ukaangalie kampuni hizo zinauhusiano gani na viongozi hao hadi wasilipe kodi na tutajua kama kampuni hizi ni zao au za ndugu zao."

Waziri Mkuu alisema serikali itahakikisha inawabana wafanyabiashara wote walionunua nguzo kwenye mikoa hiyo ambao hajalipa asilimia tano ya ushuru unaotokana na mazao ya misitu ili waweze kulipa kiasi chote walichokikwepa.

Alisema serikali inahitaji kodi kwa ajili ya maendeleo ya wananchi na haoni sababu ya mikoa hiyo kushindwa kutoza kodi iliyowekwa kwa mujibu wa sheria. Kitendo cha mikoa hiyo kutotoza kodi hakikubaliki na wafanyabiashara wote waliochukua nguzo bila ya kulipa kodi hiyo watalipa kodi yote kuanzia walipoanza kuchukua nguzo.

Waziri Mkuu alisema serikali imeweka mikakati ya wafanyabiashara wafanye biashara zao katika mazingira bora na kwa kuzingatia sheria za nchi na pia Rais Dk. John Magufuli amezuia nguzo zote za umeme kuagizwa kutoka nje ili kuwawezesha wafanyabiashara wa ndani kuuza nguzo pamoja na wananchi kupata ajira.

"Hata tulipokuwa tunanunua nguzo kutoka nje zilikuwa zinatoka hukuhuku na walichokuwa wakifanya ni kuzichukua huku na kuzipeleka nchi jirani na kuziweka kwa wiki kisha wanabadilisha vibao na kuzirudisha tena nchini."

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alimweleza Waziri Mkuu kwamba wateja wa mazao ya misiti wameanza kupungua na kwenda mikoa ya Tanga na Njombe kwa kuwa katika mikoa hiyo haijaanza kutekeleza sheria ya kutoza asilimia tano ya ushuru unaotokana na mazao ya misitu, hivyo ameiomba serikali iwasaidie.

Meneja wa kiwanda cha kutengeneza nguzo za umeme cha Qwihaya, Benedicto Mahenda, alisema kiwanda hicho kilianzishwa 2007 kwa ajili ya uchakataji wa mbao na 2016 kilianza kuzalisha nguzo za umeme wakiwa na mtambo wenye kuzalisha nguzo 100 kwa siku. Kiwanda kimeajiri watumishi 350.

Meneja huyo alisema katika kuitikia wito wa Rais John Magufuli wa kujenga uchumi kupitia sekta ya viwanda, walifanya mabadiliko kwa kujenga kiwanda kikubwa na cha kisasa cha kuzalisha nguzo za umeme chenye uwezo wa kuzalisha nguzo 1,500 kwa siku.

Alisema malighafi za kiwanda hicho wanazipata kutoka katika shamba la miti la Sao Hill lililoko chini ya Wakala wa Misitu Tanzania (TFS) na kwenye mashamba ya wakulima wadogo. Soko kubwa la bidhaa zao ni Tanesco kupitia utekelezaji wa miradi ya REA.



Mfanyakazi wa Benki ya CRDB tawi la Ubungo, Andrew Babu (katikati), akiwa chini ya ulinzi wa askari polisi katika Mahakama ya Kisutu jijini Dar es Salaam jana, akikabiliwa na kesi ya utakatishaji fedha. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Wanaume waongoza matukio ya kujiua

INATOKA UK. 3

alisema.

Vile vile, alisema sababu nyingine za watu kujiua ni upatikanaji holela wa silaha, unywaji wa vidonge na kushauri serikali kuchukua hatua.

Dk. Swai alisema ipo haja ya kudhibitiwa kwa utoaji wa dawa za binadamu katika maduka kwa kutolewa kwa kibali cha daktari.

"Udhibiti katika matumizi ya silaha pia utasaidia kupunguza matukio ya kujiua," alisema.

Alitoa ushauri pia kwa wanywaji wa pombe wanapokuwa kwenye msongo wa mawazo kuacha kwa kuwa anakuwa kwenye hatari ya kutoa uhai wake kwa kuchukua maamuzi magumu.

Akizungumzia takwimu za vifo, alisema matukio ya kujiua yanachukua nafasi ya pili kwa vifo vya vijana. Alisema wanaoongoza kwa kujiua wako kwenye umri wa miaka 15 hadi 29 kwa sababu ya changamoto wanazozipitia hasa wanapokuwa katika umri huo.

Alisema kujiua kunazuilika kwa kiasi kikubwa na jamii inatakiwa kujua namna ya kuzigundua dalili za awali na kuchukua hatua.

Naye Mwenyekiti wa Chama cha Wataalamu wa afya ya akili, Dk. Isaack Lema, aliwashauri wanaume wanapokutana na msongo wa mawazo wasikae kimya na kuumia wenyewe, ni bora walie ili kuondoa uchungu.

Pia alishauri wakutane na wataalamu ili kuwapatia ushauri na kujiepuka kujiua.

Alisema mtu anapokabiliana na msongo wa mawazo anakuwa na afya nzuri ya akili na kuendelea na majukumu yake ya kila siku.

Alisema maeneo ya kazi ni muhimu watu kuzingatia afya ya akili kwa kuwa mtu anatumia muda mrefu kufanyakazi kuliko anapokuwa nyumbani.

"Unapokuwa kazini kuna mambo mbalimbali yanajitokeza, tutafurahia kazi tunazozifanya na huduma tunazozitoa na pia itakapotokea umepata msongo wa mawazo tujitahidi kukabiliana nao," alisema.

Dk. Lema alisema mtu anaposhindwa kukabiliana na msongo wa mawazo husababisha kutaka kuacha kazi ama kuzalisha kiwango kidogo au wengine kufikiria kubadilisha kazi.

Alisema pia wanatoa ushauri kwa wenye matatizo ya afya ya akili na wenye changamoto ya unywaji pombe wa kupitiliza na kurudi katika afya njema.

# Mawaziri walalamikiwa nguzo za umeme kuuzwa

**Mwandishi Wetu,** MTWARA

MAWAZIRI na manaibu waziri saba waliopo kwenye ziara ya mikoa ya Ruvuma, Mtwara na Lindi kusikiliza matatizo ya wawekezaji na wafanyabiashara, wamelalamikiwa na wananchi kuuziwa nguzo za umeme na kutozwa tozo nyingi kwenye bidhaa moja.

Wakizungumza katika mkutano kati ya mawaziri hao, wawekezaji na wafanyabiashara, uliofanyika mkoani Mtwara, baadhi ya wawekezaji hao wamelalamikia kitendo cha kutozwa tozo zaidi ya moja kwenye bidhaa moja hali inayowakwamisha kibiashara.

Mmoja wa wafanyabiashara wa samaki, Lazaro Atanas, alitoa mfano samaki aina ya pweza ambao amedai wanatozwa tozo tano kwa kilo moja.

Alidai wanailipa Wizara ya Uvuvi Sh. 5,000, Mamlaka ya Mapato (TRA), Sh. 950, Manispaa Sh. 150, mionzi Sh. 35 na ushuru wa bandari Sh. 8,000, wakati yeye anauza samaki huyo kwa Sh. 5,250.

Pia, alidai tozo zote ni Sh. 384,000 kwa kilo 50 za pweza ilhali mfanyabiashara anapata Sh. 262,500 hivyo tozo zinazidi gharama halisi anayopata mfanyabiashara baada ya mzigo kufika sokoni.

Kuhusu suala la umeme wamelalamikia kitendo cha kuuziwa nguzo za umeme wakati serikali ilishapiga marufuku swali ambalo lilijibiwa na Naibu Waziri wa Nishati, Subira Mgalu ambaye amewatoa wasiwasi wafanyabiashara hao na wananchi wa mkoa huo kuwa serikali ilishatoa tamko kuwa hakuna mwananchi atakayeuziwa nguzo.

"Tutahakikisha tunasimamia maagizo tunayoyatoa kwa kuwa lengo la serikali ni kuboresha maisha ya wananchi wanyonge na siyo kuwakandamiza," alisema Mhe Mgalu.

Pia kuhusu suala la korosho, ufuta na mbaazi, wakulima wamelalamikia mfumo wa stakabadhi ghalani ambao baadhi yao wameuza mazao yao kwa mfumo huo, lakini hadi leo hawajalipwa fedha zao, wakati wakiwauzia wanunuzi wengine wanalipwa papo hapo na bei nzuri.

Akijibu malalamiko hayo na changamoto nyingine za kibiashara zilizoibuliwa na wafanyabiashara na wawekezaji hao, Waziri wa Viwanda na biashara, Innocent Bashungwa, alisema wizara zimejipanga vizuri kwa kushirikiana na vikao vya wadau kuhakikisha msimu unaokuja changamoto yoyote iliyojitokeza katika msimu uliopita haitajirudia tena.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Mungano na Mazingira), Mussa Sima, aliitaka mikoa yote kufanya tathimini ya mazingira kimkakati na wizara imetoa muongozo wa kuandaa na tayari amemwagiza Mkurugenzi wa NEMC kinawafikia wakuu wa mikoa wote.

Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Angeline Mabula, alisema katika kumuunga mkono Rais na azma yake ya kufikia uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda, Wizara ya Ardhi imezitaka halmashauri zote kuweka utaratibu wa uandaaji mazingira wezeshi kwa wawekezaji nchini kwa kupima au kutenga maeneo ya uwekezaji na kuweka miundombinu yote muhimu kwa kushirikiana na wizara husika.

Kwa upande wake, Waziri wa Nchi-Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji), Angellah Kairuki, alisema serikali imesikia kero zote na changamoto zinazowakabili na zitafanyiwa kazi haraka iwezekanavyo.

Aliwaeleza kuwa serikali itaangalia ni namna gani inaweza kuwa na ofisi za mikoa siku za usoni, lakini kwa sasa ina ofisi katika ngazi ya kanda. Lengo la Ofisi ya Waziri Mkuu (Uwekezaji) na TIC ni kuwasogezea wawekezaji huduma karibu zaidi ili waweze kuwa na ufanisi zaidi na kuwaondolea usumbufu.




Mkurugenzi Mkuu wa Bank Of Africa, Joseph Iha (katikati) akiongea na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu benki hiyo, kuongezewa mtaji wa Sh. bilioni 22.9 kutoka Bodi ya Benki hiyo, kwa ajili ya kuimarisha biashara zake nchini, wengine pichani (kushoto) Naibu Mkurugenzi Mkuu, Wasia Mushi, (kulia) ni Naibu Mkurugenzi wa kuendeleza biashara za benki hiyo, Samir Yassine. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Mshtakiwa akana kumsaidia Malinzi

INATOKA UK. 3

Katika ushahidi wake huo, alidai kuwa hajawahi kuhusika na malipo ya Malinzi katika benki nyingine yoyote kwa sababu alikuwa mtia saini wa benki zote za Stanbic pekee.

"Mheshimiwa hakimu katika hundi zilizoletwa hapa mahakamani kama kielelezo, nimetia saini hundi mbili na nyingine sijui nani aliyesaini (aliyetia saini). Sikuwahi kupata maelekezo yoyote kutoka kwa Malinzi akiniomba nimpatie fedha na kwamba sikuwahi kuandika hundi ya kumlipa mshitakiwa huyo wa kwanza," alidai Mwanga.

Alidai kuwa anatambua kwamba Malinzi anaidai TFF kwa sababu wafanyakazi walioko kwenye kitengo cha uhasibu wanajua kwamba Malinzi anadai.

Pia alidai mara ya kwanza kwenda benki ya Stanbic alikwenda na Hellen Adam ambaye ni mhasibu wa TFF na si washitakiwa Mwesigwa na Malinzi.

Mshtakiwa huyo aliomba mahakama hiyo imwachie huru kwa sababu hakuwahi kushirikiana na Mwesigwa kumsaidia Malinzi kujipatia fedha yoyote kama mashtaka ya utakatishaji fedha yanavyodai.

Mbali na Malinzi na Mwesigwa na Mwanga, washtakiwa wengine katika kesi hiyo ni Karani Flora Rauya.

Katika kesi hiyo ya jinai namba 213 ya mwaka 2017, washtakiwa hao wanakabiliwa na mashitaka 20 yakiwamo ya kula njama, kughushi, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu na utakatishaji wa Dola 173,335.

# Stanbic yatoa bil. 177/- kuwezesha miundombinu

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Stanbic imetoa Sh. bilioni 177 kufadhili miradi mbalimbali ya miundombinu nchini ikiwamo barabara, maji na umeme.

Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Ken Cockerill, amesema Stanbic ina nafasi kubwa katika kuchangia Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (FYDP II), ambao unalenga kuinua ukuaji wa viwanda na kuleta maendeleo ya jamii na uchumi kwa ujumla.

"Miundombinu ndio ngao ya maendeleo endelevu na kukuza ushindani. Kwa kuzingatia hilo tunafurahi kuwa mstari wa mbele katika kuziba pengo la ukosefu wa fedha za kuwekeza kwenye miundombinu ambayo ni muhimu katika kuleta maendeleo nchini Tanzania," alisema.

Cockerill alisema uchangiaji wa sekta binafsi katika ujenzi wa miundombinu ndio suluhu ya matatizo yanayokabili sekta mbalimbali ikiwamo wafanyabiashara na uwekezaji huo kuchangia kuboresha nguvu kazi, pamoja na kukuza uchumi wa Tanzania na bara la Afrika kwa ujumla.

Serikali ya Tanzania imetoa zaidi ya Sh. trilioni 12.2 (USD 5.3 billion) kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambayo inahusisha ujenzi wa Standard Gauge Railway (SGR), bomba la mafuta kutoka Uganda-Tanzania (Crude Oil Pipeline) na ujenzi wa kituo cha tatu cha kisasa katika Uwanja wa Ndege wa Taifa - Julius Nyerere International Airport Terminal III.

Kwa upande wake, Mkuu wa Huduma za kibenki za Mashirika na Uwekezaji wa Benki ya Stanbic, Manzi Rwegasira, alisema Tanzania iko katika safari ya kuziba pengo la upatikanaji wa miundombinu, jambo ambalo ni ngao katika kufanikisha uchumi wa kati wa viwanda ifikapo mwaka 2025.

"Idadi ya watu nchini Tanzania inakuwa kwa kiwango cha milioni 1.6 kila mwaka na tunakadiria kufikia watu milioni 67 mwaka 2025 na milioni 77 ifikapo mwaka 2030. Hivyo ni muhimu kuwa na miundombinu ya kisasa ambayo itakidhi mahitaji ya watu hao na maendeleo ya kiuchumi.

Alisema ushirikiano kati ya sekta binafsi kama benki ya Stanbic na serikali ndio chachu ya maendeleo jumuishi nchini.

Takwimu za mwaka 2018 kutoka Benki Kuu (BoT), zinaonyesha kuwa uchumi wa Tanzania unakuwa kwa kiwango cha asilimia 6.6, hivyo maendeleo ya miundombinu yatachangia moja kwa moja ongezeko la kiwango hicho. Mwaka huu, uchumi unategemewa kukua kwa asilimia 7.1, huku miundombinu kama barabara, bandari na reli zikitabiriwa kuongeza pato la taifa kwa kasi.

Tangu mwaka 2018 benki ya Stanbic imetoa zaidi ya Sh. bilioni 300 kufadhili kampuni mbalimbali za Tanzania katika sekta za kilimo, viwanda, maliasili na taasisi za serikali.

**TANGAZO**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA / MASHAMBA

**VIWANJA/NYUMBA.,** Hekari 25 zinauzwa Kisongo Arusha @Mil12. Heka 100 @Mil 8 Meserani Arusha. Kisongo.20x20 mil 3.3, 20x40 mil25. Nyumba inauzwa Usariver self ya bedroom4 mil70, hati ipo. Wasiliana na 0755 907 520.

**NYUMBA INAUZWA,** NYUMBA INAUZWA SINZA LION KUELEKEA KWA MWAIBULA NYUMA YA DEFRANCE HOTEL, BLOCK E PLOT No. 665, 288 SQM. MAWASILIANO: 0713 525954 / 0787 822000.

**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO**

## KUPOTEA KWA CHETI



**NAIMA HASSAN KYOMILE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye **index namba S0342/0035** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2016 katika Shule ya Sekondari Shabaan Robert.

Yeyote atakekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/SEL/RB/333316/2019/2019**

115434702

## KUPOTEA KWA CHETI



**ELIZABETH DAVID** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye Index no S0329-0017 Kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa November 2015 katika shule ya Sekondari MAKUMIRA.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu naye.

Polisi taarifa:
MWA/IGO/RB/287978/2019.

115435702

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

TANZANIA CHINA TRADE & TOURISM DEVELOPMENT LTD anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya FEKON yenye namba za usajili MC266CFG.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/DOD/RB/327773/2019.**

115435402

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu, OMARY MANYAMA MKUGE anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T.637 DEL,

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilichopo karibu kwa

**KUMB: SRT/RB/1461/2019.**

115435802

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA MJINI BUKOBA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 71/2019**

Msimamizi wa mirathi SAMSON AMOS LAWRENCE

Msimamizi wa mirathi ya marehemu WILLIAM AZIRON MULES

Kwa kuwa SAMSON AMOS ameomba kufungua shauri la mirathi katika mahakama hii leo tarehe 19/09/2019

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 21/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

215435202

## KUPOTEA KWA CHETI



**Mwajuma Abubakari** anatangaza kupotelewa kwa cheti cha Kidato cha nne Shule ya Secondari Msangeni chenye Index No **S-787-0014** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa 2001 Yeyote atakaye kiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa polisi: **MOS/RB/2934/2019**

115435502

## KUPOTEA KWA CHETI




**MARYAM SALEH MSEAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0255/0054 kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2012 katika shule ya Sekondari St. Christina Girls (Tanga). Yeyote atakekiona atoe taarifa kituo chochcoe cha Polisi.

Polisi Taarifa:
**DAR/MSI/RB/324884/2019**

115435102

## KUPOTEA KWA CHETI



**DANIEL MLIMUKA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.3811-0026** kilichotolewa na OVERLAND HIGH SCHOOL mwaka 2013.

Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**KW/RB/8299/016.**

115434702

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/03)**

**Mahakama ya Mwanzo ya ..........ARUSHA MJINI**

**Wilaya ya..................... ARUSHA**

**MADAI NAMBARI...................... 338 YA 2019**
**amdai**
**Mdai........................................ EMMANUEL GWAKISA**
**Mdaiwa ....................................JACKSON BUZBONA**
**Kwa ..........................................JACKSON BUZBONA**

**Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/wameleta madai yake/yao kwamba /eleza habari za Madai:-**

**UNATAKIWA KUFIKA MAHAKAMANI KWA AJILI YA MADAI YA 2,000,000/=**

Kwa hiyo unahitajiwa/mnahitajiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii siku ya JUMANNE tarehe 1-10-2019 saa 2:30 asubuhi/alasiri kwa kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kukatwa shauri hilo, ni lazima kuleta mashahidi wako/wenu na hati zote zinazohusu shauri hilo kwa ajili ya kujitetea katika shauri hilo.

Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhudhuria siku iliyotajwa hapo juu, mahakama ikidhibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa shaurini hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa /mmeshindwa.

Hati iliyotolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 20-09-2019.

115434902

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA- MWANZA**

**SHAURI NA 258 LA 2019**

**LEAH JAPHET ALFAYO................. MUOMBAJI**

**DHIDI YA**

1. **TANZANIA POSTAL BANK**
2. **JAGA AUCTION MART LTD**
3. **ADVERA KAZIMIL PAUL...............WADAIWA**

**WITO WA KUITWA MAHAKAMANI**

4. **KWA ADVERA KAZIMIL PAUL**

Unafahamishwa kwamba mleta maombi hapo juu amefungua shauri/ombi dhidi yako katika baraza la ardhi na nyumba mkoa wa mwanza, ombi hili limepangwa kutajwa tarehe 30.09.2019 katika chumba cha baraza barabara ya posta jengo liko mkabala na mahakama kuu ya biashara, Tanzania

Kwa hivyo unatakiwa kuhudhuria katika baraza siku hiyo wewe mwenyewe, wakili wako au mtu mwingine anayeruhusiwa kisheria

KAA- Ukijua kwamba kushindwa kufika, baraza litasikiliza ombi hilo na kutoa uamuzi bila wewe kuwepo

Imetolewa nami kwa Amri na chapa ya baraza leo tarehe 26/08/2019

115434802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No; 194/2019**

**Ombi la BONIFACE BALTAZARY KINENEKO Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu PENDO ADOLF MANYAMA.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 08/10/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 24/09/2019.

115435002

**JAMHURI WA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

**Katika Mahakama ya Mwanzo DODOMA MJINI**

**Usimamizi wa Mirathi No. 70/2019**

**Ombi la ABDUL SAID NJAITE kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu AHMED SAID NJEITE**

Watu wote wanaodai kuwa na mahusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja kuhudhuria kesi wakitaka mnano tarehe 15/10/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.

Wosia ya Marehemu huyo upo Mahakamni waweza kukaguliwa. Tarehe 23/09/2019.

115434002

## VYETI KIMEPOTEA



**HILDAGARDE JAMES CHEGE** anatangaza kupotelewa na vyeti vya shule, O'Level, Advanced, Cheti cha Jeshi na Cheti cha kuzaliwa No. **SO297-0029, SO3333-0628, AKD-4640 na 1.574/2012.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.taarifa ya polisi: **DOD/DOD/RB/316275/2019.**

115434102

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**CLEMENT DAID MANYAFU** anatangaza kupotelewa na kadi ya GARI aina ya MASSEY FERGUSON yenye namba za usajili T521BZR chasisi Na.h107202 Engini Na. H10723.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi:
**DOM/DOD/RB/327574/2019.**

115435302

## KUPOTEA KWA CHETI



**BENEDICT M. SEMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato nne chenye index namba **S.686/0016** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 1997 katika shule ya Sekondari Chato.

Yeyote atakaekion atoe taarifa kituo chochocte cha Polisi. Polisi Taarifa: **DAR/STA/RB/324603/2019**

115430502

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# MESSI AZUA HOFU BARCELONA




**BARCELONA,** Hispania

AFYA ya nahodha wa Barcelona, Lionel Messi, bado haijulikani baada ya kurejea kwenye orodha ya wachezaji majeruhi wa klabu hiyo.

Messi alikua sehemu ya kikosi kilichoanza dhidi ya Villareal kwenye Uwanja wa Nou Camp, na ulikua mchezo wake wa kwanza kufanya hivyo tangu alipopona majeraha ya nyama za paja.

Mshambuliaji huyo mwenye umri wa miaka 32, aliumia mguu na inakua bahati mbaya kwake, kwani amekumbwa na mkasa huo, akiwa ametoka kutwaa tuzo ya mchezaji bora wa dunia wa FIFA.

Hata hivyo, Barcelona walifanikiwa kuchomoza na ushindi wa mabao 2-1, yaliyofungwa na Antoine Griezmann na Arthur, huku bao la Villarreal lilifungwa na kiungo, Santi Cazorla.

Kocha wa Barcelona, Ernesto Valverde, alithibitisha kuumia kwa Messi mara baada ya mchezo huo, kwa kuwaambia waandishi wa habari kuwa, mshambuliaji huyo hakupata maumivu makubwa.

"Amepata maumivu kidogo, unajua tukio lolote linalompata Messi kila mmoja analipokea kwa mshtuko mkubwa, tutaangalia afya yake," alisema Valverde.

Hata hivyo, kocha huyo hana uhakika kama Messi atakuwa fiti kwa ajili ya mechi za wikendi hii.

# Kocha Cameroon aahidi ubingwa 2021

**YOUNDE,** Cameroon

KOCHA mpya wa kikosi cha Cameroon, Toni Conceicao, amejinasibu kuwa tayari kwa mapambano ya soka la Afrika, ili kufikia lengo la kutwaa ubingwa wa bara hilo, kupitia fainali za AFCON 2021.

Conceicao alitangazwa kuwa kocha mkuu wa kikosi cha Cameroon mwishoni mwa juma lililopita, akichukua nafasi ilioachwa wazi na Clarence Seedorf, aliyetimuliwa Julai, baada ya kushindwa kufikia lengo la kuipa mafanikio ya kutwaa ubingwa wa AFCON 2019, Simba hao wasiofugika.

Kocha huyo kutoka nchini Ureno, amesema jukumu lililo mbele yake ni kubwa, lakini anaamini kwa ushirikiano anaoutarajia kutoka kwa viongozi wa shirikisho la soka la nchi hiyo pamoja na wachezaji wake, atafanikiwa.

"Kila kazi ina changamoto zake, unachotakiwa kufanya ni kupambana bila kukata tamaa, huku ukitegemea ushirikiano kutoka kwa viongozi na wachezaji watakaounda kikosi kwa ajili ya mapambano," alisema kocha huyo aliyewahi kukinoa kikosi cha klabu ya CFR.

"Nitahakikisha kila mmoja anawajibika kwa nafasi yake, japo mwisho wa siku nitatazamwa mimi kama shujaa ama muhanga wa kushindwa, lakini nina uhakika kazi itafanyika na itaonekana,"

"Hii nafasi ni ya kipekee kwangu, ninahitaji kuitendea haki kadri nitakavyoweza, najua wananchi wa Cameroon wanafahamu raha ya kuwa bingwa wa michuano mikubwa kama AFCON."

Conceicao, atasaidiwa na gwiji wa Cameroon, Francois Omam-Biyik, ambaye alikua sehemu ya kikosi kilichotwaa ubingwa wa AFCON mwaka 1988.

Naye mlinda mlango wa zamani wa klabu ya Deportivo La Coruna ya Hispania na Metz ya Ufaransa, Jacques Songo'o, atakuwa sehemu ya benchi la ufundi la Cameroon.

Benchi jipya ya ufundi la Cameroon likiongozwa na Conceicao, litaanza kazi yake Novemba katika mchezo wa kuwania kufuzu fainali za Afrika, dhidi ya Cape Verde.

Cameroon watakua wenyeji wa fainali zijazo za Afrika (AFCON 2021), na azma yao kubwa ni kubakisha ubingwa wa fainali hizo nyumbani kwao.





# *Owen afunguka tofauti kati yake na Shearer*

**LONDON,** England

SASA imefichuka kwamba, ugomvi kati ya nyota wa zamani wa Timu ya Taifa ya England, Michael Owen na Alan Shearer ni kwa sababu ya mechi ya mwisho ya Newcastle United ya msimu wa 2008/09.

Owen katika kitabu chake alichokitoa hivi karibuni, amebainisha kwamba, alikataa kucheza mechi hiyo na ndio iliyosababisha yeye na Shearer kuingia kwenye ugonvi.

Newcastle walikuwa wakihitaji pointi moja tu ugenini kwa Aston Villa ili kubaki kwenye Ligi Kuu England, lakini walishuka baada ya Damien Duff kujifunga na kuharibu mipango yote.

Kipindi hicho, Shearer alichukua majukumu kwenye kikosi hicho katika mechi nane za mwisho, wakati Owen hakuwa bize sana kwa sabbu mkataba wake ulikuwa unakwisha, hivyo alikuwa akielekea kuwa mchezaji huru mwishoni mwa msimu huo.

Jambo hilo lilimkasirisha Shearer kwa sababu alimwona Owen alikuwa akijijali yeye binafsi kuliko kuiokoa timu isishuke daraja.

Na baada ya kuzindua kitabu chake na kisha Owen kusema kujiunga Newcastle United lilikuwa kosa kubwa alilowahi kulifanya kwenye maisha yake, jambo hilo limemfanya aanze kurushiana maneno na gwiji mwenzake wa England, Shearer.

Owen alisema: "Tulikuwa marafiki kwa miaka kibao. Ukweli, moja ya sababu zilizonifanya niende Newcastle ni kucheza na Alan Shearer".

Baada ya hapo, akafichua sababu ya kutibuana kwao, akisema: "Ilikuwa kwenye mechi ya mwisho ya msimu. Yeye alidhani mimi nitacheza, lakini nilikuwa na majeruhi ya korodani.

## HABARI MICHEZO

# Arsenal kuivaa Liverpool Kombe la Ligi

**LIONDON,** England

BAADA ya mechi za mzunguko wa tatu wa Kombe la Carabao, Manchester United imepangwa kukutana na Chelsea kwenye mzunguko unaofuata, huku Liverpool ikipangwa kucheza na Arsenal.

Mchezo huo uliochezwa usiku wa kuamkia jana kwenye Uwanja wa Old Trafford ulishuohudia United wakianza kupata bao la kuongoza dakika ya 68 kupitia kwa Greenwood, kabla ya Matheson hajaisawazishia Rochdale dakika 75.

Matokeo hayo yalizifanya timu hizo kupigiana penalti, na ndipo Manchester United walipoibuka kidedea na kusonga mbele.

Mchezo wa mzunguko wanne, United watasafiri hadi jijini London kuwakabili Chelsea, ambao pia walifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 7-1 dhidi ya Grimsby Town.

Wao Liverpool na Arsenal wataanza kwenye mchezo utakaopigwa kwenye Uwanja wa Anfield mwezi ujao.

Mabingwa watetezi wa michuano hiyo Manchester City wamepangwa kuikabili Southampton kwenye Uwanja wa Etihad, huku Aston Villa yenye itakutana na Wolves.

**Michezo mingine ya mzunguko wanne wa nne ni:.**

| | | |
|---|---|---|
| **Oxford** | **Vs** | **Sunderland** |
| **Crawley Town** | **Vs** | **Colchester** |
| **Burton** | **Vs** | **Leicester** |
| **Everton** | **Vs** | **Watford** |






# POCHETTINO ATAJWA KUMRITHI ZIDANE

**MADRID,** Hispania

WAKATI kocha wa Real Madrid, Zinedine Zidane, nafasi yake bado ikiwa shakani kufuatia mvutano unaoendelea kwenye vikao vya uongozi wa klabu hiyo, Mauricio Pochettino, ametajwa kuwa anawaniwa na miamba hao wa dimba la Santiago Barnabeu.

Zidane alianza kujadiliwa na kuwagawa viongozi wa juu, kufuatia matokeo ya kupoteza mchezo dhidi ya Paris Saint-Germain (PSG) juma lililopita, kwa kufungwa mabao 3-0.

Taarifa mbalimbali zimekuwa zikieleza kuhusiana na kipigo hicho na hali ya usalama wa kibarua cha Zidane huko Bernabeu, ambapo meneja wa zamani wa wababe hao wa Bernebau, Jose Mourinho, ambaye kwa sasa hana kazi aliripotiwa angerudishwa kuchukua mikoba.

Kocha wa Tottenham, Pochettino anapewa nafasi kubwa ya kumrithi Mfaransa huyo, ambaye alikubali kurejea Santiago Bernabeu, miezi michache kabla ya msimu wa 2018/19 kufikia kikomo.

Kwa mujibu wa gazeti la The Mirror, Pochettino ndiye anayepewa nafasi kubwa ya kwenda kuchukua mikoba huko Bernabeu, wakiamini kwamba hata mshahara wake hautakuwa mkubwa sana, na inakadiriwa huenda akakubali kulipwa pauni milioni 8.5 kwa mwaka.

Spurs ya Pochettino ilikuwa kwenye ubora wake msimu uliopita ikifika fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya na kufungwa na Liverpool huko Madrid, na mabosi wa Los Blancos wanaamini itakuwa vema kama atakwenda kumbadili Zidane huko Bernabeu.

# *Puyol akataa majukumu Barca*

**BARCELONA,** Hispania

BEKI na nahodha wa zamani wa Barcelona, Carles Puyol, amekataa nafasi ya kuwa meneja utawala wa klabu hiyo, baada ya kuondoka kwa Pep Segura, Julai mwaka huu, kufuatia matatizo ya kifamilia.

Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu, amethibitisha alikua na mpango wa kufanya kazi na gwiji huyo kuanzia mwezi huu, lakini alipomfikishia taarifa za uteuzi, alizikataa.

Bartomeu amesema, aliamini Puyol angekua mtu sahihi katika upande wa utawala, kufuatia mchango wake mkubwa aliowahi kuutoa klabuni hapo, akiwa kama mchezaji kuanzia mwaka 1999 hadi 2014.

"Nimefikiria kwa kina kuhusu ofa ya klabu yangu, nimeona si kwa wakati huu, ninamshukuru kila mmoja aliyechangia mawazo ya kuniteua," ameandika Puyol kwenye ukurasa wake wa Twitter.

"Haikua rahisi kukataa nafasi hiyo, lakini imenilazimu kutokana na sababu mbalimbali, nitaendelea kuiheshimu na kuipenda klabu yangu na ninaamini ipo siku nitarudi kuiongoza kwenye nafasi yoyote."

Endapo Puyol angekubali kuchukua nafasi ya utawala klabuni hapo, angefanya kazi na rafiki zake Eric Abidal ambaye ni mkurugenzi wa michezo, sambamba na mkurugenzi wa soka la vijana Patrick Kluivert.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# WENGER AFUNGUKA ANAITAMANI UNITED

Mfaransa huyo asema ni ndoto waliyonayo ya makocha wengi ...

**LONDON,** England

KOCHA Arsene Wenger amebainisha kuwa kupata nafasi ya kuifundisha Manchester United ni 'kazi ya ndoto' na ni wazo linalotakiwa kuendelezwa kuhusu utamaduni wake.

**Mkongwe huyo wa Arsenal ambaye bado hajapata timu nyingine ya kufundisha, ameweka wazi maoni yake kuhusu anavyotamani kutua kwa mahasimu wake wa zamani, na Mfaransa huyo ameeleza kwamba anatamani kurithi kibarua hicho cha Ole Gunnar Solskjaer.**

"Kufundisha Manchester United ni ndoto aliyonayo kila kocha. Ninajiamini, nina uwezo, na uko sahihi, nina mawazo," Mfaransa huyo aliiambia Fox Sports Asia.

Aliongeza kuwa ni jambo lisilowezekana kwa kocha ambaye alidumu kwa muda mrefu na kupewa heshima, Sir Alex Ferguson ninaweza kutua kwenye kiti hicho cha klabu kubwa cha kuiongoza Old Trafford.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 69, lakini alijitokeza hadharani na kueleza mawazo yake kwamba anaamini United inaweza kurejea katika hadhi yake kwa kusajili wachezaji wapya wenye uwezo wanne.

"Wanahitaji, kwa mawazo yangu wanatakiwa kusajili wachezaji wanne wa kikosi cha kwanza, watarudi kwenye ushindani. Lakini kwa kuendelea kutumia wachezaji waliopo, kikosi hicho kitazidi kukumbana na changamoto mbalimbali. Hawako mbali na wengine kama watu wanavyofikiria.

United imeanza msimu huu kwa kupata changamoto ya kucheza kiwango cha chini na kuifanya kuwa kwenye nafasi ya nane katika msimamo wa Ligi Kuu England.

Juzi usiku ilipata wakati mgumu wa kuiondoa Rochdale katika mashindano ya Kombe la Carabao, na kulazimika kufika hatua ya matuta baada ya kutoka sare ya bao 1-1.

Wenger ameweka wazi kisu chake na hakuamua kupepesa macho kuhusiana na kiwango na kikosi cha United kinavyocheza.

"Timu inavyocheza haina muunganiko, haina muunganiko katika kushambulia. Kunaoneka kuwa na timu tu, lakini inahitajika mtu wa kuwafundisha na kuwaendeleza. Kama nilivyosema, wachezaji wanne wakisajiliwa wanaweza kusaidia changamoto iliyopo. Na kumaliza tatizo," alisema.

Wenger aliamua kustaafu kuifundisha Arsenal mwisho wa msimu wa 2017-18 baada ya kudumu klabuni hapo kwa muda wa miaka 21.

## ZISIKUPITE

### MADRID YAMTAKA ERIKSEN

REAL Madrid wameweka wazi kuwa wanataka kumsajili kiungo wa Tottenham na Timu ya Taifa ya Denmark, Christian Eriksen (27), kwa kumpa mkataba wa awali katika dirisha dogo la Januari na baadaye kumnasa kocha wa Spurs, Mauricio Pochettino. ***(Mirror)***

### SPURS YAPATA HOFU

MABOSI wa Tottenham wanahofu kuwa kiungo wao, Christian Eriksen, atakataa kuuzwa katika dirisha dogo la usajili la Januari, ili aweze kuondoka kama mchezaji huru katika kipindi cha majira ya joto mwakani. ***(Mail)***

### ALLEGRI KUMRITHI POCHETTINO

KOCHA Massimiliano Allegri, ambaye aliamua kupumzika kufundisha soka kwa muda wa mwaka mmoja baada ya kuondoka Juventus Mei mwaka huu, anatarajia kuingia katika mchakato wa kurithi nafasi ya Pochettino endapo ataondoka Tottenham. ***(Sun)***

### MANDZUKIC ANUKIA UNITED

STRAIKA wa Juventus na Timu ya Taifa ya Croatia, Mario Mandzukic (33), amekacha ofa ya thamani ya pauni milioni 7 ya kujiunga na klabu moja ya Qatar baada ya kuwa na nafasi ya kusajiliwa na Manchester United katika dirisha dogo la usajili la Januari. ***(Mail)***

### SPURS KUMBAKISHA KANE

MWENYEKITI wa Tottenham, Daniel Levy, anajiandaa kutangaza dau la juu la thamani ya Harry Kane (26), kuwa ni pauni milioni 250, kwa klabu yoyote itakayomhitaji nyota huyo wa Timu ya Taifa ya England kubakia klabuni hapo ikiwa ni msimu mwingine bila ya Spurs kushinda taji lolote. ***(Telegraph)***

### IBRAHIMOVIC SOKONI

KLABU ya Boca Juniors inajiandaa kuwasilisha ofa ya kumsajili straika wa zamani wa Timu ya Taifa ya Sweden, Zlatan Ibrahimovic (37), ambaye sasa anaichezea klabu ya LA Galaxy ya Marekani. ***(AS)***

### HAALAND ANUKIA ENGLAND

STRAIKA wa Red Bull Salzburg na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland (19), anahusishwa na mpango wa kuhamia katika Ligi Kuu England baada ya kufunga hat-trick katika mechi ya mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

### BRUYNE APEWA MCHONGO

KOCHA wa zamani wa Manchester City, Hein Vanhaezebrouck, ambaye alimfundisha, Kevin de Bruyne (28), amemtaka nyota huyo kujiunga na klabu ya Paris St-Germain kama anataka kushinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Het Nieuwsblad via Sun)***

### XAVI AMTAJA STERLING

MCHEZAJI mkongwe wa Barcelona, Xavi, ambaye sasa anafundisha klabu moja huko Qatar, amemtaja mshambuliaji wa Manchester City, Raheem Sterling (24), kuwa chaguo sahihi. ***(Mail)***

### UNITED KUJENGWA UPYA

MAKAMU Mwenyekiti Mtendaji wa Manchester United, Ed Woodward, anafanya mazungumzo na wamiliki wa klabu hiyo, familia ya Glazer kuhusu kutaka kutekeleza "utamaduni" wa klabu hiyo ili kuleta mabadiliko. ***(Express)***

## Mchenga, Tamaduni zatinga fainali Bballs King

**Na Sabato Kasika**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Sprite Bball Kings, timu ya Mchenga Bball Stars imefanikiwa kutinga fainali ya michuano hiyo baada ya kuichapa Flying Dribblers vikapu 102-72.

Kwa ushindi huo, sasa Mchenga Bball Stars itakutana na Tamaduni kwenye mchezo wa fainali, ambayo nayo imeiondoa KG Dallas katika mashindano hayo kwa kuifunga vikapu 116-65.

Katika mchezo wa nusu fainali ya kwanza, Mchenga Bball Stars iliibugiza Flying Dribblers vikapu 99-71 wakati Tamaduni kwa upande wake iliwachapa KG Dallas vikapu 99-76.

Msemaji wa mashindano hayo, Goza Chuma, alisema kuwa fainali za Sprite Bball Kings 2019 itachezwa baada ya wiki mbili zijazo ili kuzipa timu hizo zilizofuzu hatua hiyo muda wa kutosha wa kujiandaa na mchezo huo.

"Katika fainali kutakuwa na michezo mitano ili kupata bingwa, lakini timu itakayofungwa michezo mitatu, itakuwa ni nafasi ya kumtangaza bingwa wa Sprite Bball Kings 2019," alisema Chuma.

Mashindano hayo yameandaliwa na East Africa Televisheni na East Africa Radio kwa lengo la kuibua vipaji vya mchezo nchini na kuuendeleza na kupata umaarufu kama ilivyo michezo mingine.

"Vyombo hivi vya habari vinaung292anisha nchi za Afrika Mashariki kwa kuwalenga zaidi vijana kuanzia miaka 18 hadi 35 ili kuwahabarisha, kuwaburudisha na kuwaelimisha kupitia vipindi mbalimbali," alisema.

## Pamba yatamba kuimaliza Geita FC

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

KOCHA Mkuu wa Pamba FC, Muhibu Kanu, amesema kuwa anakiamini kikosi chake kitapata matokeo mazuri katika mchezo wa Ligi Daraja la Kwanza dhidi ya Geita Gold FC utakaochezwa keshokutwa Jumamosi kwenye Uwanja wa Nyamagana jijini hapa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kanu, alisema kuwa wachezaji wake wamefanya maandalizi mazuri kuelekea mchezo huo na wamejipanga kuondoka na pointi tatu ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kurejea kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara msimu ujao.

Kanu alisema kuwa wamecheza mechi mbalimbali za kirafiki, kwa lengo la kuwapa uzoefu wachezaji wake na kuwaimarisha kukabiliana na ushindani uliopo kwenye ligi hiyo.

Aliongeza kuwa kikosi chake kinaundwa na wachezaji chipukizi na wazoefu wakiwamo Gaudence Mwaikimba na Nizar Khalfan, nyota wa zamani wa Yanga na Timu ya Taifa (Taifa Stars), hivyo hana hofu na mchezo huo wa Jumamosi.

Katika kujiweka imara kuelekea ligi hiyo, Pamba FC ilicheza mechi mbalimbali za kirafiki, ikiwamo dhidi ya Yanga ya Dar es Salaam ambayo ilimalizika kwa sare ya bao 1-1.

# FAILUNA UWANJANI DOHA MASHINDANO YA DUNIA

**Na Mwandishi Wetu**

MWANARIADHA Mtanzania Failuna Matanga anatarajia kukimbia katika mbio za kilomita 42 zitakazofanyika leo mjini Doha, Qatar, ikiwa ndio ufunguzi rasmi wa mashindano ya riadha ya dunia, imeelezwa.

**Watanzania wengine waliofuzu kushiriki mbio hizo ambazo zitarushwa mubashara katika king'amuzi cha Dstv ni pamoja na Alphonce Simbu, Stephano Huche na Augustino Sulle, ambao wako chini ya kocha mkongwe, Andrew Panga.**

Wanariadha hao watatu, wanaume wao watakimbia mbio hizo za kilomita 42 ifikapo Oktoba 5 mwaka huu.

Mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Riadha Duniani (IAAF), yanatarajiwa kujumuisha wanariadha kutoka nchi mbalimbali duniani.

Mkurugenzi Mtendaji wa MultiChoice Tanzania, Jacqueline Woiso, alisema kuwa DStv itaonyesha mbio hizo mubashara kupitia SuperSport channel namba 13.

"Kama kawaida yetu hatutaki wateja wetu na Watanzania kwa jumla wakose burudani ya michuano mikubwa ya dunia kama hii, hivyo tumehakikisha kuwa watashuhudia mashindano haya kupitia Dstv," alisema Woiso.

Aliongeza kuwa hii ni fursa ya Watanzania kuwashuhudia wawakilishi wao wakipeperusha vema bendera ya nchi katika mashindano hayo na anaamini watarejea na medali.

Alisema kuwa wanariadha hao wa hapa nchini wanaoshiriki mashindano hayo ni wazoefu, hivyo tunatakiwa kuwaombea Mungu watimize malengo yao.

"Kushiriki kwa wakimbiaji hao nguli kunaleta matumaini ya Tanzania kufanya vizuri hasa ikizingatiwa kuwa ni wanariadha wazoefu na wameshawahi kufanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa ikiwamo Mumbai Marathon, ambapo Simbu alishinda medali ya dhahabu," alisema Woiso.



Baadhi ya wachezaji wa timu ya gofu ya Lugalo kutoka jijini Dar es Salaam, wakijiandaa kufanya mazoezi kwa ajili ya kushiriki mashindano yanayotarajiwa kuanza leo kwenye Uwanja wa Chuo cha Polisi Moshi. **PICHA: SELEMANI SEMUNYU**

# *KMKM, Kipanga FC hapatoshi Z'bar*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya 'Mabaharia' wa KMKM wanatarajia kuwakaribisha 'Maafande' wa Kipanga katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Mao Tse Tung kuanzia saa 10:00 jioni.

KMKM watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya kushinda mechi zake mbili zilizopita, wakati Kipanga ina pointi nne kutokana na kushinda mchezo mmoja na kutoka sare mara moja.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa KMKM, Ame Msimu, alisema mipango yake ni kuhakikisha hapotezi mchezo wa leo kwa kuwaandaa wachezaji wake kufunga idadi kubwa ya mabao.

Msimu alisema kuwa anahitaji kuona wanapata ushindi mnono ili waweze kukaa katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo za juu kwa upande wa visiwani hapa.

Kocha huyo aliongeza kuwa anamatumaini makubwa ya kuutetea ubingwa wanaoushikilia licha ya kufanya vibaya katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Naye Kocha Mkuu wa Kipanga, Rashid Lato, alisema timu yake ina uhakika itafanya vizuri katika mchezo huo na wachezaji hawana hofu licha ya KMKM kuwa na uzoefu katika ligi hiyo.

"Wachezaji wamejipanga na hawana hofu juu ya mchezo huo, licha ya KMKM kuwa ni wazoefu katika Ligi Kuu, lakini mpira hauna uzoefu, matokeo yoyote yanaweza kutokea uwanjani, lakini sisi tunataka alama tatu," Lato alisema.

Ligi hiyo inatarajiwa kuendelea tena kesho kwa katika viwanja vitatu tofauti, Zimamoto itakutana na Chuoni wakati KVZ itaumana na Jamhuri huku Selem View ikiwakaribisha Machomane.



Wenger afunguka anaitamani Utd
UKURASA 30



Wachezaji wa Simba kutoka kushoto, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr', Sharaff Shiboub na Meddie Kagere, wakionyesha ishara ya kutafuna mua katika mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba. Simba ilishinda mabao 3-0. **PICHA: SIMBA SC**

# Simba yafuta uteja Kaitaba kibabe

## ●●● Ni baada ya kuwachapa Kagera Sugar mabao 3-0 na kurejea kileleni...

**Na Adam Fungamwango**

KILELENI! Mabingwa watetezi Simba wamemaliza "uteja" wa kufungwa na Kagera Sugar baada ya kupata ushindi wa mabao 3-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba.

**Mabao mawili ya mshambuliaji Mnyarwanda Meddie Kagere na Mohammed Hussein "Zimbwe Jr" yaliifanya Simba kuvunja mwiko wa kutoifunga Kagera Sugar katika mechi tatu mfululizo za Ligi Kuu Tanzania Bara.**

Mara ya mwisho Simba kuifunga Kagera Sugar ilikuwa ni Januari 22 mwaka jana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2017/18, ambayo ilichezwa kwenye Uwanja wa Kaitaba, kwa mabingwa hao watetezi kupata ushindi wa mabao 2-0 yaliyofungwa na Said Ndemla na John Bocco.

Tangu hapo si tu Simba ilikuwa ikishindwa kupata ushindi kwenye Uwanja wa Kaitaba, lakini pia ilikuwa ikishindwa kuifunga Kagera Sugar hata walipoikaribisha jijini Dar es Salaam na mara zote iliambulia vipigo.

Ilifungwa bao 1-0 katika mechi ya mzunguko wa pili kwenye Uwanja wa Taifa, msimu uliopita, halafu ikapoteza michezo yote miwili ya msimu ulipita, ilifungwa mabao 2-1 walipokuwa ugenini na ilipowavaa kwenye Uwanja wa Uhuru jijini Dar es Salaam ilifungwa goli 1-0.

Ushindi huo wa jana ni wa tatu mfululizo kwa msimu huu na umeifanya Simba kurejea tena kileleni katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara ikiwa na pointi tisa.

Dalili za kuondoka na ushindi zilianza mapema dakika ya nne kupitia kwa Kagere ambaye amefunga kwenye mechi zote tatu mfululizo za ligi alizocheza.

Kagere alifunga bao la kwanza kwa kichwa baada ya kazi nzuri ya Ibrahim Ajibu kuwahadaa mabeki wa Kagera Sugar, kabla ya kumpa pasi, Deo Kanda aliyepiga krosi iliyomaliziwa na mfungaji huyo. Zimbwe Jr ambaye katika mechi ya mwisho ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu uliopita alijifunga bao na kuipa ushindi wa bao 1-0 Kagera Sugar, aliipatia Simba bao la pili kwa shuti dhaifu la pembeni, baada ya pasi ya kisigino kutoka kwa Kagere dakika ya 35.

Kipindi cha pili ni kama Simba iliingia kulinda zaidi ushindi, ikishambulia kwa kushtukiza na kuwaacha Kagera Sugar wakitawala muda mwingi wa mchezo.

Dakika ya 78, Kagere tena, aliipatia Simba bao la tatu kwa penalti na la tano kwa mfungaji huyo msimu huu, iliyotokana na winga machachari wa timu hiyo, Miraji Athumani, aliyeingia kipindi cha pili kuchukua nafasi ya Ajibu aliyeangushwa na beki mzoefu, Juma Nyosso kwenye eneo la hatari.

Wenyeji waliendelea kulisakama lango la wageni wao, lakini mabeki wa Simba wakiongozwa na Paschal Wawa na Tairone Santos da Silva walikaa imara kuondoa hatari zote.

Baada ya mechi ya jana, Simba itasafiri kuelekea Musoma, Mara kuwafuata wenyeji wao Biashara United katika mchezo mwingine wa ligi hiyo utakaochezwa keshokutwa Jumapili.

Katika mechi nyingine ya ligi hiyo iliyochezwa jana kwenye Uwanja wa CCM Samora mjini Iringa, wenyeji Lipuli FC walilazimishwa sare ya mabao 2-2 na Mbeya City.

# Yanga yatamba haina wasiwasi

**Na Somoe Ng'itu**

KIKOSI cha Yanga cha jijini Dar es Salaam, kimetua kamili kwenye ardhi ya Ndola nchini Zambia tayari kuwakabili wapinzani wao Zesco, huku uongozi wa klabu hiyo ukisema kuwa hawana wasiwasi wowote kuelekea mchezo huo wa marudiano.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alisema kuwa kikosi cha timu hiyo kiko kwenye mazingira salama na mipango ya kuhakikisha wanashinda mchezo wao wa marudiano inakwenda vizuri.

Mwakalebela alisema kuwa wachezaji wote wako katika hali nzuri, wanaamini watatimiza malengo waliyoyaweka ya kushinda mechi hiyo na kusonga mbele katika mashindano hayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Alisema kuwa morali ya kila mchezaji iko juu na kilichobakia ni kusubiri muda wa "mtangane" huo kuanza.

"Tulifika salama Ndola, kwa upande wa uongozi, tumeendelea kujipanga vema kuhakikisha malengo yetu yanatimia, kila kitu kinakwenda sawa sawa, hatuna wasiwasi, benchi la ufundi nalo linafanya kazi yake, matarajio ni kupata ushindi Jumamosi na si matokeo mengine," alisema Mwakalebela.

Naye kiungo wa timu hiyo Mzanzibari Feisal Salum "Fei Toto" alisema kuwa kikosi cha Yanga kimejipanga kupambana "kufa au kupona" katika mchezo huo, na wamejiandaa kukutana na ushindani.

"Kwanza tunamshukuru Mungu tumefika Ndola salama, tunawaahidi mambo mazuri mashabiki wetu wa Yanga, wajiandae kuja kwenye Uwanja wa Ndege kutupokea kwa mbwembwe," alisema Fei Toto.

Wakati huo huo, kikosi cha Azam FC, kiliondoka mjini Harare nchini Zimbabwe na kuelekea Bulawayo ili kuwafuata wenyeji wao katika mchezo wa marudiano wa Kombe la Shirikisho Afrika utakaochezwa kesho dhidi ya Triangle United.

Kocha Mkuu wa Azam FC, Etienne Ndayiragije, aliliambia gazeti hili kuwa wamejiandaa vizuri kuelekea mchezo huo licha ya hali ya kubadilika na kuwa ya baridi hapo jana.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002 >